ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe	- Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	- Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	- Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	- Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	- Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	- Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	- Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	- Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	- Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	- Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	- Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	- Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	- Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	- Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	- Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	- Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	- Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	- Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	- Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Pili – Tarehe 20 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Kny: Hamza Hassan Juma Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, kwaniaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, naomba kuwasilisha mezani hati ya maoni juu ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 101

Utekelezaji wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Hivi karibuni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umetimiza miaka 47 tangu kuasisiwa kwake. Lakini wananchi wengi wamekuwa wakilalamika juu ya utekelezaji wake.

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuitisha Kura ya Maoni, ili wananchi waeleze kama unafaa kuendelea kama ulivyo hivi sasa au laa?

(b) Je, hadi hivi sasa ni mambo mangapi yameainishwa kuwa ni kero za Muungano huo?

(c) Je, ni mambo mangapi kati ya hayo yameshatatuliwa na mangapi bado hayajapata ufumbuzi?.

.

(d) Je, wananchi watarajie kupatiwa ufumbuzi lini mambo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Ni kweli Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliofanyika mwezi wa Aprili mwaka 1964 na kuzaliwa Jamhuri ya Muungano Tanzania na sasa umetimiza miaka 47, ambapo sherehe za kutimiza miaka hiyo zimefanyika kwa mafanikio makubwa katika Uwanja wa Amani Mjini Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wote kwa kuadhimisha siku hiyo ya Muungano wetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa majibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kuwa serikali zetu zimechukua hatua ya kuanzisha mchakato wa kuifanyia mabadiliko Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo itawashiurikisha wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kutoa maoni yao kwa uwazi kuhusu marekebisho hayo ya Katiba.

   Kwa kuwa Katiba ndio dira ya uongozi wa nchi yetu. Hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra wakati huu tunaelekea kwenye mchakato wa marekebisho ya Katiba. Kwani mara baada ya marekebisho hayo suala la Kura ya Maoni limezingatiwa, ili kutoa fursa kwa wananchi wa pande mbili za Muungano wetu kuridhia Katiba hiyo. Mhe. Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wajitokeze kwa wingi wakati utakapofika kwa ajili ya kutoa maoni yao.

b) Mhe. Spika, ni mambo kumi na tatu (13) ndiyo yaliyoainishwa kwa sasa kuwa ni kero za Muungano na kuwasilishwa katika Kamati ya Pamoja ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais chini ya Mwenyekiti Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, Kamati ya Pamoja haifungiki kushughulikia kero nyengine kama zitajitokeza.

c) Mhe. Spika, vikao vya kujadili kero za Muungano vimeanza mnamo mwaka 2006, ambapo jumla ya vikao 6 vimeshafanyika na mambo 8 yameshapatiwa ufumbuzi na 5 bado yanaendelea na kujadiliwa.

d) Mhe. Spika, naomba kueleza kwamba kwa kero zilizobakia mazungumzo yanaendelea vizuri, hasa katika ngazi za kisekta na tunatarajia kero zitapatiwa ufumbuzi kwa kadri mazungumzo yanavyoendelea. Dhamira ya serikali zetu kuongeza kasi ya kushughulikia kero hizo, ili ufumbuzi upatikane mapema iwezekavyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake ameeleza ni mambo kumi na tatu (13) ndiyo yaliyoainishwa kama ni kero za Muungano, manane (8) yamefanyika na matano (5) bado. Je, Mhe. Waziri unaweza kutueleza hayo mambo kumi na tatu (13) ni yepi na hayo matano (5) yaliyobakia ni yepi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba mambo yote ya kero za Muungano yalikuwa ni kumi na tatu (13) na hivi sasa kati ya hayo manane (8) yamepatiwa ufumbuzi na matano (5) yanaendelea kujadiliwa.

Kwa hivyo, kwenye hayo manane mawili tayari yamepata hati rasmi ya utekelezaji ikiwemo Tume ya Haki za Binadamu kuweza kufanyakazi zake Zanzibar, Utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* ya mwaka 2003 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uwezo wa Zanzibar kuweza kujiunga na *International Maritime Organization*.

Mambo ambayo yamapata ufumbuzi na bado hayajapata hati ya utekelezaji ni pamoja na:-

1. Mgawanyo wa Fedha zinazotokana na Misamaha ya Madeni ya Nje, hadi hivi sasa Zanzibar imepata jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 15.12 katika misamaha hiyo.

2. Uwezo wa Zanzibar kukopa nje ya nchi. Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Fedha Zanzibar zimeagizwa kuandaa utaratibu mzuri utakaoondolea urasimu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupata mikopo ya nje.

3. Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa kodi mara mbili. Kwa kweli imekubalika kwamba bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kifedha kupitia kituo chochote cha Forodha, zitahesabika kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. Kodi ya Mapato imekubaliwa kuwa Sheria ya Kodi ya Mapato inayohusu mishahara irekebishwe, ili mapato hayo yaweze kuwasilishwa sehemu ambayo watumishi wa Jamhuri ya Muungano wanafanyakazi. Sheria ya *Withholding Tax* ifanyiwe marekebisho, ili mapato yanayokusanywa kutoka kampuni au mashirika yalioko Zanzibar yabaki Zanzibar na yale yanayokusanywa Tanzania Bara yabaki Tanzania Bara.

5. Usajili wa magari, imekubaliwa kuwa gari zinazosajiliwa na zinazotaka kusajiliwa upande wowote wa Muungano, zitahesabiwa kuwa gari hizi zimesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6. Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Kwa kweli tayari mawazi wanaohusika katika masuala ya uvuvi kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wameweka saini kuhusu Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu na kazi za utoaji wa seleni zinafanyika kwa pamoja katika kipindi hiki cha mpito ikisubiriwa kuridhiwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu na Baraza lako Tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, bado mchakato unaendelea ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweza kuwasilisha kwenye kikao chako cha Baraza sheria hii.

Mhe. Spika, kwa mambo ambayo yanaendelea kujadiliwa ni haya yafuatayo:-

(i) Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki
(ii) Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.
(iii) Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje.
(iv) Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano na
(v) Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri aliki kwamba zipo kero za Muungano na zipo zilizoshughulikiwa na nyengine bado.

Mhe. Spika, wakati ulipofanyika Muungano huu kulikuwa na viongozi wawili waliokubaliana na yule wa Zanzibar akawa ni Makamo wa Kwanza wa Rais wa Tanzania, kwa sababu cheo hiki kilifutwa. Naomba kuumuliza Mhe. Waziri ni nani mwenye uwezo wa Kikatiba kuiwakilisha Zanzibar katika mazungumzo ya kero za Muungano na matatizo yote ya Muungano?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, mwenye uwezo wa kuwakilisha kero za wananchi wa Zanzibar kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, katika kukasimu madaraka yake Mhe. Rais amekubali Tume yetu ya Pamoja kwa upande wa Zanzibar ikiongozwa na Makamo wa Pili wa Rais, ili tuwasilishe kero zetu kupitia Kamati ya Pamoja kama makubaliano yalivyofanyika katika Jamhuri nzima ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lake Mhe. Waziri kwa kuwa amekubali kwamba suala la biashara kulipa mara mbili tayari lilikuwa limeshakubalika katika kuondoa kero. Je, Mhe. Waziri ataliambia nini Baraza hili tukufu kuwa wizara yake italisimamia na kuliondoa mara moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tayari makubaliano yamefikiwa kwa bidhaa zitakazoingia sehemu yoyote ya Jamhuri yetu ya Muungano, basi bidhaa hizo zitahesabiwa tayari zimeingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala hazipaswi kulipiwa kodi mara mbili.

Vile vile kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo suala hili amelieleza sana na amesema atachukua hatua kali kwa wale wote watakaowabughudhi wafanyabiashara wa Zanzibar. Kwa hivyo, serikali itakuwa macho kulishughulikia jambo hili. *(Makofi)*

Nam. 68

Mradi wa Michirizi Magomeni

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante pamoja na kwamba suala la utekelezaji wa mradi huu niliouzungumzia hapa tayari umeelezwa ndani ya Bajeti Kuu ya Serikali. Lakini kwa faida ya wananchi naomba Mhe. Waziri anijibu swali langu.

Kwa kuwa ukamilishaji wa Maandalizi ya Mpango wa Utekelezaji wa Mradi wa Michirizi Awamu ya Tatu chini ya Ufadhili wa Benki ya Dunia tayari yamekamilika. Na kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ulitarajiwa kuanza mapema mwaka 2011, na hadi sasa bado haujaanza.

Je, Mhe. Waziri, nini matarajio ya serikali katika mradi huu muhimu kwa wananchi wa Magomeni, Sogea, Mwantenga na Sebleni.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Mjumbe, kwa kukiri kwamba swali hii limepata jibu fasaha kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na

Mipango na Maendeleo kwenye Hotuba ya Bajeti. Mhe. Spika, ni kweli kabisa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ametoa maelezo ya ufasaha kabisa katika mradi huu na pia naomba nimpongeze sana, kwa sababu mimi nilipoona nikasema hapa tayari mradi umeshatandikwa vizuri na Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mradi huu unao matarajio makubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa vile mradi huu muhimu utawagusa wananchi katika maeneo yao ya makaazi moja kwa moja hasa wananchi wa Magomeni, Sogea, Mwantenga na Sebleni.

Vile vile Mhe. Spika, Mradi huu wa Uimarishaji wa Huduma za Mji wa Zanzibar (*ZUSP*) una lengo la kuimarisha uwezo na Miundombinu katika maeneo ya Baraza la Manispaa na pia uimarishaji wa Mabaraza ya Miji ya Chake Chake, Mkaani na Wete. Mradi huu kama ilivyoelezwa umepangiwa jumla ya US$ 38 milioni sawa na shilingi za Kitanzania Bilioni 58 ikiwa ni mikopo kutoka Benki ya Dunia.

Mkataba wa Utekelezaji wa mradi ulitiwa saini tarehe 6 Aprili, 2011 na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi wa Julai, 2011.

Mradi huu utahusisha ujenzi wa michirizi, uwekaji wa taa za barabarani katika baadhi ya maeneo. Usombaji wa taka ngumu ikiwa pamoja na ujenzi wa majaa ya kusanyaji taka.

Mradi huu utawanufaisha sana wakaazi wamaeneo ya Baraza la Manispaa ikiwa pamoja na mitaa hiyo niliyoitaja kwa kuondoa kero ya kutuwama kwa maji, kuimarisha uchukuwajiwa taka ngumu, kupunguza athari za kimazingira na kuimarisha afya na ustawi wa jamii kwa wananchi wote kwa ujumla. Ahsante.

Nam. 9

Serikali Kuifanyia Marekebisho (*One Stop Centre*)

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu sasa kumekuwa na matatizo mengi ya *ZIPA* yanayosababishwa na kutoweza kuwa na kituo kimoja cha kumaliza maandalizi yote (*one stop centre*) kwa wawekezaji wa ndani na nje.

(a) Je, kuna marekebisho gani yaliyofanywa kurekebisha hali hiyo?

(b) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa unaoonesha kuwa matatizo hayo yanaweza kurekebishika?

(c) Je, serikali imeweka mikakati na motisha kwa kiasi gani kwa lengo la kuwapata wawekezaji wa viwanda, kilimo na uvuvi badala ya kujenga hoteli za kitalii pekee.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 9 lenye kifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, katika Baraza lako tukufu la mwezi Januari mwaka 2011 tulitoa majibu ya swali Nam. 27 yenye kifungu (a) na (b) linaloshabihiana sana na swali hili.

Katika majibu hayo, nilitoa maelezo mafupi juu ya dhana ya "*One Stop Centre*" na kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, kiini cha tatizo cha utekelezaji wa dhana hiyo inatokana na mapungufu yaliyomo katika Sheria zinazosimamiwa na taasisi mbali mbali za hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nikiri kuwa mwenendo wa marekebisho ya sheria zinazohusika ili kuondoa hali hiyo haiyendani na kasi ya mabadiliko inayolengwa, hata hivyo azma ya kila taasisi ya kurekebisha Sheria na Kanuni zinazohusika ipo. Hivyo inadhihirishwa na hatua zilizokwishachukuliwa na taasisi hizo, ambazo ziko katika hatua mbali mbali kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Ardhi (*Land Tenure Act*) ya 1992 imefanyiwa marekebisho katika mwaka 2010 na marekebisho hayo yanaipa nguvu, pamoja na mambo mengine, Sheria ya Uwekezaji kupendekeza mambo yanayohusiana na ardhi kukodishwa kwa mwekezaji, kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 19 cha sheria hiyo.

(ii) Marekebisho ya mwaka 2010 ya Sheria ya Kodi (*Income Tax Act*) ya 2004 yanatoa fursa kwa Afisa wa Kodi kufanya kazi moja kwa moja na Mamlaka ya *ZIPA* juu ya mambo ambayo sheria hiyo imeyatolea maamuzi na kwamba utekelezaji wake unataka uratibu wa taasisi hizo mbili.

(iii) Kuna mapendekezo ambayo yako katika hatua za awali kuifanyia marekebisho Sheria ya Uhamiaji, ambapo pamoja na mambo mengine ya kitaifa, suala la utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji juu ya kuharakisha maamuzi yanayohusu ukaazi kwa wawekezaji wageni limezingatiwa.

(b) Mhe. Spika, naomba nikiri kuwa hakuna utafiti wa kitaalamu uliofanywa, ukiachia ule wa awali wakati wa kuzingatia dhana nzima ya kukaribisha uwekezaji vitega uchumi kutoka nje. Hii ni kwa sababu tatizo limebainika katika hatua ya utekelezaji wa majukumu ya kitaasisi, ambayo ni maelekezo ya sheria. Sheria zikirekebishwa tunaamini kuwa dhana hiyo itatekelezeka bila ya matatizo yoyote.

(c) Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tunaazisha harakati za kuwakaribisha wawekezaji hapa Zanzibar, tuliamini kuwa uwekezaji kwa sekta mbali mbali utakwenda sambamba kama tulivyopanga. Hata hivyo, hali ya uwekezaji katika sekta ya viwanda, uvuvi na kilimo cha biashara haikuwa nzuri kutokana na sababu mbali mbali.

Kutokana na hali hiyo, serikali imejiandaa kuifanyia marekebisho Sheria ya Uwekezaji (*ZIPA*) kwa lengo la kutoa fursa za sekta hizo. Kadhalika, serikali imeunda wizara kamili inayoshughulikia masuala ya uvuvi kwa nia ya kutoa msukumo zaidi. Kwa sehemu kubwa tunaamini juhudi hizo zitasaidia sana katika kupata wawekezaji katika sekta hizo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kuwa tunao wawekezaji wa ndani na nje na nchi nyingi hutoa fursa au upendeleo kwa wawekezaji wa ndani. Je, ni fursa gani ambazo *ZIPA* hutoa kwa wawekezaji wa ndani, ili kuweza kushajihisha wengine kuwekeza ndani ya nchi?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ukiipitia Sheria ya Uwekezaji kwa kweli imetoa fursa kwa wawekezaji wote kwenye sheria hiyo regardless kwamba yeye ni wa ndani au nje na hayo ni maeneo ya mapungufu katika sheria, ndio maana wawekezaji wetu wa ndani wanashindwa kushindana na wawekezaji wa nje.
Kwa hivyo, kama nilivyosema awali kwamba sheria hiyo tunataka tuifanyie marekebisho, ili kutoa fursa kwa sekta nilizozitaja pamoja na wawekezaji wetu wa ndani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba Sheria ya Uwekezaji au *ZIPA* ina mapungufu na hivi sasa

tumo kwenye kutekeleza MKUZA kwa ajili ya kuwaondolea wananchi wetu umasikini na Sekta ya Viwanda ni moja ambayo inaweza kuwapunguzia wananchi umasikini. Vile vile sheria hivi sasa ina upungufu na wawekezaji wa ndani wanapata usumbufu. Je, Mhe. Waziri atawasaidia vipi wale wawekezaji kwa ajili ya kuwaondolea usumbufu na waweze kuwekeza na wananchi wetu wa Zanzibar wapate ajira, ili kuwapunguzia umasikini.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza ningemuomba Mhe. Mjumbe kuwa hawa wawekezaji ambao wanataka kuwekeza kwenye Sekta ya Viwanda ni dhahiri kwamba wangekuja kuniona nikiwa pamoja na Mhe. Waziri wa Viwanda na Masoko, ili tukaweza kuwasaidia na wala tusisubiri mpaka sheria tukairekebisha wakati muwekezaji yupo.

Kwa hivyo, tunaweza kuwasaidia kwa kuzingatia yale maelekezo ambayo tunataka kuifanyia sheria marekebisho. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe hao wawekezaji waje, ili tuweze kusaidiana nao na tutakapofikia pahala, basi sheria yetu tutairekebisha ili iweze kutoa msukumo zaidi katika kuwekeza kwenye Sekta ya Viwanda ambavyo vitasaidia kutoa ajira pamoja na kuinua uchumi wetu.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Zanzibar tumekubali sisi wenyewe wawekezaji kuja kuwekeza na kuna baadhi ya wawekezaji sasa wamekuwa wajeuri mno. Kwa mfano, unapokwenda kuangalia kama ni Mjumbe wa Kamati basi hizo jeuri wanazozitoa na kufikia hadi kutoa kashfa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri analijua suala hili?

(b) Ikiwa analijua au halijui basi ni utaratibu upi ambao umewekwa na wizara husika, ili kuhakikisha kwamba nidhamu katika nchi inachukuliwa?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba suala hili mimi silijui. Lakini kupitia kwa Mhe. Mjumbe nimemsikia akiniuliza na sina sababu ya *doubt* suala lake, nataka nimhakikishie tu kwamba nitazungumza na wawekezaji na Wizara yangu itaweka utaratibu ili wawekezaji waweze kuheshimu sheria na kanuni na taratibu za nchi yetu.

Nam. 137

Nyongeza ya Mshahara kwa Watumishi wa Umma

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk - Aliuliza:

Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu viwango vidogo vya nyongeza za mishahara vya kila mwaka kwa Watumishi wa Umma hapa Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri ni viwango gani vya nyongeza za mishahara vinavyolipwa kwa Watumishi hao hivi sasa.

(b) Je, ni lini viwango hivyo vimefanyiwa mapitio kwa mara ya mwisho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora –Alijibu:

Naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake namba 137 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika. napenda kumuarifu Mheshimiwa Mwakilishi kuwa naomba kukubaliana na suala la kuwepo kwa malalamiko ya viwango vidogo vya nyongeza za mishahara vya kila mwaka kwa watumishi wa umma na kimsingi marekebisho ya mshahara yanayokusudiwa kufanyiwa mapitio, yamezingatia suala hilo ili kuwashajihisha wafanyakazi kukamilisha malengo ya kazi watakazopangiwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu swali lake Na 137 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika kwa hivi sasa Serikali imesita kutoa nyongeza hizo wakati wa marekebisho ya mshahara yaliyofanywa katika mwaka 2007/2008 na Serikali kwa wakati huo ilipanga kuandaa utaratibu wa kutoa nyongeza hizo baada ya mfanyakazi kupimwa uwezo na utendaji wake wa kazi.

Hata hivyo katika mwaka wa fedha ujao wa 2011/2012 Serikali inakusudia kurejesha utaratibu wa kuwapatia nyongeza za mshahara wafanyakazi wake wote kwa kila mwaka. Hata hivyo naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kiwango kinacholipwa kwa hivi sasa cha mshahara ni kima cha chini ni Shs. 100,000/= .

b) Mhe.Spika kwa mara ya mwisho Serikali ilifanya mapitio ya nyongeza mwaka 2007/2008

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Waziri anajua kwamba kuna wafanyakazi wa serikali ambao wameongeza viwango vyao vya elimu na huu ni mwaka sasa hawajarekebishiwa mishahara yao. Je, hilo Mhe. Waziri analijua.

Na kama analijua anafanya juhudi gani kuhakikisha kuwa watu hawa wanarekebishiwa mishahara yao lakini pia wanalipwa *area* zao za mwaka?.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nalijua suala la wafanyakazi ambao wameongeza viwango vyao vya elimu na ambao bado hawajarekebishiwa mishahara yao, nalijua kwa sababu malalamiko yamekuja katika Wizara yangu na baada ya kulifuatilia tumeona ni kasoro tu za kiutawala ndizo zilizosababisha mapungufu hayo.

Hata hivyo napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba katika marekebisho ya mshahara ambayo yameshafanywa na serikali yamezingatia maoni au suala ambalo ameniuliza, namuomba Mhe. Mwakilishi awe mstahamilivu nitakaposoma bajeti yangu nitaweza kueleza utaratibu mzima ambao utatumika katika kuondosha kasoro hizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Juzi tu baada ya serikali kuwasilisha bajeti yake hapa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar wametoa malalamiko wakisema kwamba wamekuwa hawashirikishwi katika kufikiria au kupanga viwango vya mishahara kama ndio sheria ya kazi inataka kufanyika.

Je, Mhe. Waziri anayajua malalamiko hayo na ana kauli gani kuhusu malalamiko hayo ya Vyama vya Wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Nasikia kwamba Shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi linasema kwamba hawashirikishwi katika kupanga viwango vya mishahara serikalini. Lakini naomba nimhakikishie kwamba Shirikisho la Vyama huru vya Wafanyakazi linayo Wizara ambayo inasimia sekta na sheria iliyowaweka na sheria ile inawataka kwanza wafanye mazungumzo katika kutafuta huo utata, wafanye

mazungumzo ya kuona kwanza *private sector* wanaweka viwango vya mishahara ambayo ina maslahi kwa watumishi wao, baada ya vikao hivyo pia wanatakiwa waowanishe kati ya viwango vile na viwango vya watumishi wa Umma.

Hata hivyo napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Shirikisho la Wafanyakazi Zanzibar *(ZATU)* walifika Ofisini kwangu na nilifanya mazungumza nao kati yangu na wao. Moja kati ya masharti niliyowapa ni kwamba wao ni wajumbe wa kamati za uongozi za Wizara katika sekta husika na viwango vya mishara vinapangwa na Wizara wakati wanapopanga bajeti vinaanzia huko, sasa tulikubaliana kwamba wao wanapata taarifa gani kutoka kwenye sekta husika katika masuala haya ya ushirikishwaji.

Lakini tukiendelea tu kujenga zana kwamba *(ZATU) ni Makao* Makuu na sio kwenye Taasisi husika nafikiri tutakuwa hatufanyi jambo zuri, lakini vyema katika masuala haya kuzingatia huo utata ni kwanza tushiriki kwenye wafanyakazi wenyewe jambo ambalo linaonyesha kasoro kubwa kwamba mikutano hiyo katika sekta husika wafanyakazi hawashirikishwi kikamilifu, sasa unaposema kwamba wewe ushirikishwe kwa jinsi gani wewe unawashirikisha hao wafanyakazi wenyewe.

Lakini nataka nimhakikishie kwamba watapozingatia masharti hayo serikali iko tayari kushirikiana nayo katika kutekeleza sheria ambazo wamezitunga.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi kuuliza suala moja la nyongeza ambalo ni fupi sana.

Mhe. Spika, kwa ufupi serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia pesa nyingi sana kuwasomesha vijana wetu mpaka elimu ya juu kabisa, lakini wengi wao huacha kazi Zanzibar au kutokuripoti kabisa baada ya masomo kwa sababu ya mshahara mdogo wanaoupata.

Je, katika marekebisho haya ya viwango vya mshahara serikali imetilia maanani suala hilo ili wale watu wetu wabakie katika nchi hii na kuleta matunda ya elimu yanayoipata.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwanza nataka nikubaliane nae kwamba baadhi ya wahitimu wengi au Serikali inatumia fedha nyingi kwa kuwasomesha wataalam wake na baadhi yao sio wote huamua kuondoka nchini kwa kuowanisha hivyo viwango vidogo vya mishahara, sitaki niende kwengine namalizia hapo.

Lakini nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba katika marekebisho ambayo yamefanywa na nitayawasilisha kwenye bajeti yangu yamezingatia viwango vya elimu ili kuweza kuwalipa wataalam wetu mishahara ambayo itakidhi kwa kiasi fulani kuwapa moja ya wakuweza kufanya kazi, sio hilo tu bali tumezingatia pia kwa mfano wewe umepata *master degree* yako mwaka 1983 basi kiwango chako kitatofautiana kabisa na yule ambae amepata kiwango cha elimu hiyo katika mwaka 2010.

Nam. 96

Chama cha Wanasheria Kuistaki Serikali

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, kutokana na suala langu la zamani na kupoteza uhalisia wake sasa kwa heshima na taadhima naomba kuliondoa.

Mhe. Spika: Suala hili limeondolewa.

Nam. 15

Ujenzi wa Barabara za Vikunguni Chake-Chake

Mhe. Salma Mohammed Ali (Nafasi za Wanawake) - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dr. Amani Abeid Karume katika Sherehe za kuwakabidhi zawadi wanafunzi wa Skuli ya Vikunguni waliofanya vyema mitihani yao miaka mitatu iliyopita, aliahidi kuitengeneza barabara ya Vikunguni- Wawi katika kiwango cha lami. Lakini hadi leo barabara hiyo haijatengenezwa na inabaki kuwa ni tatizo kwa wakaazi wa Vikunguni.

(a) Je, ni lini Serikali itaitekeleza ahadi hiyo.

(b) Je, Mhe. Waziri, huoni kuwa kitendo cha kutotekelezwa kwa ahadi hiyo iliyotolewa na Mhe. Rais Mstaafu, kunawadhalilisha viongozi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 15 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa, Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dr. Aman A. Karume aliahidi kutengeneza barabara ya Wawi – Vikunguni katika kiwango

cha lami katika sherehe za kukakidhi zawadi wanafunzi wa skuli ya Vikunguni. Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kuwa ahadi zinazotolewa na viongozi wetu wa juu ni nyingi na zinahitaji fedha nyingi katika utekelezaji wake. Katika utekelezaji wa agizo hilo la ujenzi wa barabara hiyo, Wizara yangu imeanza kufanya matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja na kupiga greda, kuweka kifusi na muda huu makalbi yanatengenezwa kwa ajili ya kuweka makalvat kwa maeneo husika. Utaratibu huu umeanzia Wawi – Vikunguni hadi Mzambarau Mboko. Malengo ya kuweka lami yatafikiwa pale hali itakaporuhusu.

(b) Wizara yangu inapenda kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba bado ahadi hiyo ya Mhe. Rais Mstaafu wa awamu ya Sita, Dr. Amani Karume imepokelewa na inafanyiwa kazi, kama nilivyoeleza katika jibu (a) hapo awali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifutavyo:

Kwa kuwa barabara ya Vikunguni hadi Wawi ni barabara muhimu sana kwa ajili ya usafiri na usafirishaji wa bidhaa, kwa kuwa serikali yetu imetilia mkazo sana wananchi kujiajiri ili kujiongezea kipato, kwa kuwa barabara ile inaponyesha mvua hata kipindi hiki cha miezi mitatu ya nyuma iliyopita inakuwa haipitiki na mazao mengi hushindwa kusafirishwa kutoka Vikunguni hadi kufikia soko kuu la Chake Chake.

Je, kuendelea kuicheleweshe kuitekeleza ahadi ya Mhe. Rais wetu sio kuendelea kuwanyima haki yao ya msingi wale wananchi wa Vikunguni kwa kuweza kujipatia kipato.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Katika maelezo yangu ya awali tumeeleza kwamba barabara hii tumeiboresha kwa kuweka kifusi na kujenga ma-*calvat* katika maeneo ambayo yalikuwa yanawazuia wananchi katika kupata huduma ya usafiri, malengo ya kuweka lami na kuwapa fursa wananchi hao kwa ajili ya kusafirisha mazao yatafikiwa pale hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa ahadi ya Rais ni ahadi ya serikali na kwa kuwa zipo ahadi tokeza Dk. Salmin Amour, Mhe. Amani Karuma na hadi leo Mhe. Ali Mohamed Shein anaweza kuendelea kuweka ahadi na kwa kuwa hazitekelezwi kwa kisingizio cha fedha.

Je, Wizara yako kwa sababu ni sehemu ya Baraza la Mapinduzi ameshauri viongizoi wetu wakuu hawa, kwamba wanapoweka ahadi waangalie hali ya fedha kwa sababu inaonekana kwamba inadhalilisha pale hali ahadi isipotekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, nadhani ahadi wanazotoa viongozi vinatokana na mahitaji maalum viongozi hawa wanatambua uwezo wa serikali yetu fedha zilizopo na mahitaji hayo ya wananchi, ahadi zao wanazitoa pale ambapo wanahisi kuna haja maalum ya kufanya hivyo. Hivyo basi nadhani itakuwa sio busara kuwazuia viongozi watu wa juu wasitoe ahadi kwa maeneo na haja maalum pale inapobidi. Jambo la msingi ni kuona namna gani serikali yetu inaongeza fedha na upatikanaji wa fedha hizo ili kuweza kukamilisha mahitaji na ahadi hizi za viongozi wetu.

Nam. 89

Uhaba wa Walimu wa Sayansi

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:

Kwa muda mrefu, Wizara ya Elimu inalalamikia kuendelea kuwepo upungufu wa waalimu wa masomo ya sayansi. Ni ukweli unaoendelea kuwepo kwamba wizara iliwajengea mazingira mabaya ambayo yaliwafanya washindwe kuendelea na shughuli zao za ufundishaji. Miongoni mwa walimu hao ni walimu wa masomo ya sayansi ambao bado wapo na wengine wanaendelea kuwasaidia wanafunzi wa skuli zetu bila ya malipo yeyote.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni haja ya kuwatafuta walimu hao na kuwashauri warudi kufundisha katika skuli zetu.

(b) Je, Wizara itakuwa tayari kupatiwa majina ya walimu kama hao na kufanya mazungumzo nao na wakiridhika na majadiliano nao iweze kuwarejesha kufundisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Eilimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali namba 89 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa skuli zetu zinakabiliwa na upungufu wa walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya sayansi. Upungufu huo unatokana na ongezeka la wanafunzi wanaojiunga na skuli zetu kulingana na idadi ndogo ya walimu wanaomaliza mafunzo ya ualimu katika fani Sayansi na Hesabati. Dhana ya

kuwa Wizara imewajengea mazingira mabaya ya kazi walimu wa fani za sayansi sio sahihi kwa vile mazingira ya skuli zetu zote yanafanana na hakuna ubaguzi wa walimu kwa mujibu wa fani zao. Katika kukabilina na upungufu wa walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya Sayansi Hesabati. Wizara imeandaa mafunzo mbali mbali kwa walimu wa sayansi kwa nia ya kuongeza ujuzi wao. Miongoni mwa mafunzo hayo ni mafunzo ya walimu wa Sayansi na Hesabati yaliyoandaliwa kupita mpango wa "*Teachers" Advancement Programme*" *(TAP)* ambapo walimu baada ya kukamilisha mafunzo ya muda wa mwaka mmoja walikabidhiwa vyeti vya kufaulu mafunzo hayo.

Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:

a) Wizara haina taarifa ya kuwepo kwa walimu wa sayansi ambao hivi sasa hawana ajira. Iwapo kuna walimu kama hao ambao hawana ajira, Wizara inawaomba wafuate taratibu zilizowekwa ili waweze kuajiriwa rasmi.

b) Wizara iko tayari kupokea majina ya walimu kama hao na pindipo itathibitika kuwa wana sifa za kufundisha masomo ya sayansi, taratibu za kuwaajiri zitafuatwa kwa mujibu wa sheria za utumishi.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Waziri Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri hao walimu wa sayansi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Serikali ina mpango wa kuajiri walimu wa sayansi, ukweli tuna matatizo ya walimu hao na katika bajeti hii kama wajumbe wa baraza lako tukufu watatupitishia basi tumeomba kuajiri walimu mia nane (800) kati ya hao walimu mia tano (500) ni walimu wa masomo ya sayansi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Moja kati ya mambo yanayosababisha walimu wa sayansi kuondoka na kukimbilia katika skuli za binafsi ni maslahi duni kwa wafanyakazi hao. Je. Wizara katika kuwabakisha walimu hawa ina mpango gani wa kuwaandalia mazingira bora walimu hawa ili waendelee kubaki, kwa sababu kuajiri tu sio tatizo unaweza kuajiri halafu wakakimbia, lakini ili kuwabakisha na waendelee Wizara imewaandalia mpango gani mahususi walimu wa sayansi ili waweze kubakia katika maskuli yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe Spika, ni kweli tofauti ambayo tunayo ya walimu wa sayansi na art ni tofauti ndogo sana, kwa mfano kama walimu ambao wana diploma ya sayansi wanapishana na walimu wa art kwa shilingi elfu tatu tu si zaidi ya hapo. Kwa kiwango hiki kidogo ni kweli hakiwezi kumvutia hata yule anayeanza sasa kusoma kuchukua masomo ya sayansi ambayo anahisi ni magumu.

Lakini kama nilivyoeleza kuwa bajeti yetu imezingatia hilo ni utayari wa wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kuikubali na baada ya hapo tutarajie walimu wengi watapenda kusomesha masomo ya sayansi.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa vile walimu wa sayansi hapa nchini kwetu wapo wengi wameshastaafu kwa nini Mhe. Waziri hatoi wito wa kuweza kukaa nao na akafunga nao mkataba kabla hatujawapata hao wengine watakaokuja.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kama nilivyojibu kwenye jibu langu mama ikiwa walimu hao wapo wa sayansi basi tunawakaribisha waje Wizarani na utaratibu wa kuajiri utafuatwa kwa mujibu wa sheria.

Nam. 50

Urejeshwaji wa Ardhi Walizoporwa Wananchi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:

Napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar kwa umakini wa kuwachagua wasaidizi wake ikiwa ni pamoja na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad (Makamo wa Kwanza wa Rais) na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi (Makamo wa Pili wa Rais), unaoanza kuonekana matunda yake. Aidha, nampongeza Makamo wa Pili wa Rais kwa tamko lake la kuwataka watendaji na Viongozi waliohusika na upotevu wa ardhi za Serikali na wananchi, wazirejeshe ardhi hizo na wawajibishwe kisheria.

(a) Kwa kuwa Serikali imegundua kuna baadhi ya watendaji wake hawakuwa waaminifu katika masuala ya ardhi, Je, Serikali iko tayari sasa kufanya uchambuzi wa kina ili kugundua mali zilizopotea ili zirejeshwe.

(b) Kwa nini Serikali haiweki Sheria inayohusu, pamoja na mambo mengine, kushughulikia maadili ya Watumishi na Viongozi wa Umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 50 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu kama sehemu ya Serikali inaendelea hatua tafauti kuhakikisha malalamiko yote yanayohusu ardhi yanashughulikiwa ipasavyo, kama itavyokuwa nje ya uwezo wa Wizara yangu, wahusika watashauriwa kuhakikisha wanapeleka malalamiko yao kwenye vyombo vya Sheria. Kwa upande wa ardhi za Serikali, Wizara inafuatilia na itapobainika, ardhi yake inahodhiwa isivyo halali, itachukua hatua muwafaka kuirejesha ardhi hiyo.

(b) Swala la Sheria ya maadili liko nje ya Mamlaka ya Wizara yangu, siwezi kulisemea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala maja la nyongeza lenye vifungu a, b na c kama ifutavyo.

a) Zipo taarifa za kuaminika kwamba eneo la kilimo na Mifugo la Mboghoja Kachunge Mwambe, limepimwa na kuchukuliwa na wageni na baadhi ya Maafisa wa serikali kwa njia ya siri bila ya hata kuwashirikisha wazalendo. Je, Wizara yako hilo inalijua.

b) Kama eneo hilo halikutolewa kisheria

(b) Kama eneo hilo halikutolewa kisheria na kwa vile walihusika Maafisa wa serikali kuligawa eneo hilo. Lini Wizara yako itachukua hatua ya kuwafukuza kazi wale ambao wamehusika.

(c) Kwa kuwa mtindo huu wa kuyatoa maeneo kiholela yanakera sana serikali hii, pia Mhe. Balozi Makamo wa Rais amelikemea na pia Mhe. Rais wa Zanzibar amelikemia. Nini kauli ya serikali kupitia kwako na kwa kuwa hasa kilimo na mifugo ni kwa ajili ya bajeti hii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza naomba alirejee lile swali la mwanzo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rejea swali la kwanza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Swali la kwanza lilifuatiwa na maelezo kwamba kuna eneo linaitwa Mhoja Kashinde Mwambe ni eneo la kilimo na mifugo. Limepimwa kupitia Idara ya Ardhi na Upimaji na wamepewa baadhi ya wageni na maafisa wa serikali kwa njia ya siri.

Swali langu ni kwamba wizara yako ilihalalisha vipi na hata wazalendo wasipewe eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nasema wizara yangu haina taarifa ya eneo hilo kutolewa.

Mhe. Spika, ni kweli kuna watu wengi ambao wanahodhi ardhi za serikali kinyume na utaratibu. Wizara yangu kwa kulifanyia kazi suala hili, itahakikisha wale wote ambao wanaovamia na kuhodhi ardhi za serikali, itafanya uchunguzi na ikishakuwabaini, tutawachukulia hatua zinazofaa kisheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika,

(a) Atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kuwa migogoro ya ardhi wizara yako inachangia kwa kiasi kikubwa.

(b) Suala ulilozungumza kuwa wahusika waende kwenye vyombo vya sheria, huoni kuwa serikali itapata hasara kubwa kutokana na kutowajibika kwa wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nimesema kwamba wizara yangu italishughulikia tatizo hili na kuwafuatilia mmoja baada ya mmoja yule ambaye anahodhi ardhi za serikali. Pale ambapo tatizo litakuwa halipo katika wizara yangu au wizara yangu haina uwezo wa kulishughulikia suala lile, basi nitalipeleka katika vyombo vya sheria.
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, kwa kuwa wizara hii ina waziri mpya, ina naibu mpya, Mhe. Waziri umejipanga vipi katika kuliondoa tatizo hili kwa kuwa lina muda mrefu na sasa hivi imekuwa ni kero kwa watu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapenda wananchi wake wapate makaazi bora na salama kwa kutoa ardhi za serikali.

Mhe. Spika, nitahakikisha wizara yangu italishughulikia suala hili ipasavyo. Inajua wananchi wa Zanzibar wengi wamedhulumiwa ardhi zao kupitia wajanja wanaoshirikiana na baadhi ya watendaji wa serikali ambao hushirikiana na wajanja hawa wakawanyang'anya watu ardhi zao baadaye wakasingizia ardhi hizi zimechukuliwa na serikali.

Kwa kuliangalia hili wizara yangu itajitahidi na italisimamia kikamilifu na kuhakikisha tatizo hili linawekwa sawa katika kipindi kifupi.

Nam. 39

Umalizwaji Kituo Cha Afya Kibokoni

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Kibokoni katika Jimbo la Wawi tayari wameanzisha Ujenzi wa Kituo cha Afya kwa ajili ya kupunguza usumbufu kwa wananchi kufuata huduma ya afya ikiwemo ile ya afya ya mama na mtoto katika masafa ya mbali, na kwa kuwa kituo hicho tayari kimejengwa imebakia hatua ya usafi na kumalizia.

Je, ni lini serikali itaunga mkono juhudi hizo za wananchi kwa kumaliza sehemu iliyobaki ya ujenzi huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwanza naomba niombe msamaha kuwa sauti yangu haipo vizuri.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwamba naomba kutoa maelezo mafupi juu ya ujenzi wa vituo vya afya, kwa muda mrefu sasa limekuwa ni jambo la kawaida kwa wananchi kujenga vituo vya afya katika sehemu mbali mbali. Mara nyingi ujenzi huu hauzingatii sera, mipango na miongozo ya Wizara. Sera ya Afya (Serikali) imeweka bayana taratibu za mpangilio wa vituo vya afya katika nchi.

Mtandao wa vituo vya afya unatakiwa uwe ndani ya kilomita tano (5) ili kila mwananchi aweze kuzifikia huduma hizo. Kwa upande wa Zanzibar, hatua hii

imefikiwa vizuri sana kwani zaidi ya asilimia 95 ya wananchi wanaishi ndani ya km 5. Kwa upande wa Pemba wananchi walio wengi wanaishi karibu na kituo cha afya chini ya kilomita 5. Kazi kubwa kwa sasa ni kuimarisha vituo vya afya ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za wafanyakazi karibu na vituo.

Kijiji cha Kibokoni kipo karibu sana na hospitali ya Vitongoji, *Ali Khamis Camp*, vyote hivyo ni chini ya kilomita 5. Suala hilo liliwahi kupelekwa katika uongozi wa afya wa Wilaya ya Chake-Chake *(DHMT)* na ilikubaliwa kwamba ujenzi huo usiendelee na badala yake watumie vituo vilivyo karibu nao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba niuulize swali moja dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa kituo hiki kilijengwa kwa bidii kubwa ya wananchi pamoja na misaada mbali mbali kutoka kwa viongozi wetu wakuu wa serikali akiwemo aliyekuwa Makamo wa Rais ya Jamhuri ya Muungano ambaye kwa sasa ni Rais wetu mtukufu Mhe. Ali Mohammed Sheni. Vile vile mama Shadia Karume alifika kusaidia na kutoa msaada mkubwa katika kituo hiki.

Kwa kuwa ilani za vyama vyote viwili kikiwemo Chama cha Mapinduzi ambacho Mhe. Naibu Waziri kimemuingiza katika Baraza hili, zimetilia mkazo ilani hizi juu ya kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Kwa kuwa wanawake wa Kibokoni wanatoka karibu kilomita moja na nusu au kilomita mbili hadi kufika Hospitali ya Changuo. Je, kuendelea kukiacha kituo kile kibomoke au kuvunjika, hii si kudharau bidii za wananchi wetu pamoja na kudhalilisha jitihada za viongozi wetu.

Kwa kuwa yeye ni mwanamke na kwa kuwa wanawake wanapata shida sana kutoka Kibokoni hadi Vichanguo kufuata huduma ya mama na mtoto. Je, kuendelea kukiacha kituo kile kuvunjika si kuwadhalilisha wanawake wenzake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nimezungumza katika jibu la msingi kwamba vituo vya afya vinatakiwa viwe si chini ya kilomita 5, na vituo vya Vitongoji, *Ali Khamis Camp* vipo karibu sana na Mgogoni. Kwa hivyo hatuwezi kuwa na vituo vitatu katika *area* moja ambayo ni ya kilomita 5.

Tunapozungumza suala la kwamba tunataka kuimarisha vituo vya afya tunakusudia tuwe na wafanyakazi, ambalo sasa hivi ni tatizo hilo. Tunatakiwa tuwe na vifaa vya kutosha ambalo sasa hivi pia ni tatizo. Tunatakiwa tuwe na madawa ya kutosha ambalo sasa hivi ni tatizo. Sasa kama hizo zilizokuwepo ni tatizo kuyatimiza hayo, tukijenga kingine kipya tutakifanyaje.

Hilo halimaanishi kwamba nawadhalilisha waliochangia na waliopendekeza. Isipokuwa nafuata sera na mipango ya serikali. Kufuata sera na mipango ya serikali haimaanishi kwamba unawadhalilisha wale waliochangia.

Ninachosema kwamba wananchi hawafuati taratibu wala muongozo wanapojenga vituo vya afya. Maana kama kingelikuwa kilomita 5 tungekibariki na tungekifanya kinavyotakiwa kufanywa.

Sasa naomba kusema kwamba ile nyumba haitabomolewa kwa sababu katika moja ya mambo ambayo tunataka tuyafanye ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu tunaowapeleka wanapata nyumba za kukaa. Naiimarishwe ili iwe nyumba ya kukaa wafanyakazi. Keshokutwa Vitongoji itakuwa hospitali kubwa na tunahitaji pa kuwaweka madaktari, patakuwa hapatoshi. Nakusihini mkaimalize ile nyumba muifanye iwe nyumba ya kukaa.

Mimi nimeiona hiyo nyumba ya Kibokoni kwanza haikujengwa kama hospitali, imejengwa zaidi kama nyumba ya kukaa kuliko hospitali. Haikuzingatia kabisa utaratibu wa hospitali, ikirekebishwa itafaa zaidi. Lakini kilomita tano (5) zilizopo pale wanapokaa wanawake wa Kibokoni na Vitongoji hazifiki kilomita 5 ni chini ya hapo.

Population iliyokuwepo katika sehemu ile kuwa na hospitali mbili tena halafu tukaweka na nyengine kwa kweli itakuwa ni vigumu kwa serikali.

Mimi kama mwanamke ningependa wanawake wote wapate huduma. Nina imani hospitali ya Vitongoji na *Ali Khamis Camp* wakienda watapata huduma. Sio kwamba kila nyumba iwe hospitali, hiyo haiwezekani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa nampongeza sana, lakini kuna msemo wa Kiswahili unasema "*mtoto akihomokeza huwa amuomolea mzee wake" na "mtoto anapoliharibu bega hili hubebwa kwa bega jengine"* huwezi ukamtupa mtoto. Serikali ni mama kwa wananchi wake, ili kujali wananchi wake na nguvu zake wananchi tayari wamejenga jengo lile kwa ajili ya hospitali, lakini kwa sababu hospitali zipo karibu na wao wameshapoteza nguvu zao nyingi kwa ajili ya kujenga.

Mhe. Naibu Waziri kasema kwamba lile jengo sasa litumike kwa ajili ya nyumba ya madaktari. Je, serikali kupitia Wizara ya Afya iko tayari kulinunua jengo lile ili kuwafidia wananchi zile nguvu zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nia ya wananchi kujenga ni kuisaidia serikali iwe kituo cha afya, iwe nyumba. Iweje leo hii Serikali inunue nyumba eti kwa sababu inatakiwa.

Hilo la kwanza la pili jamani! Tuulizeni maswali ambayo yana haki, hii sio haki. Nilichoomba mimi ilikuwa imejengwa iwe hospitali, badili ya kuwa hospitali kwa vile tunayo hospitali nyengine sasa ile nyumba iwe kwa ajili ya wafanyakazi wa hospitali. Hizo pesa zenyewe tunazopewa Wizara ya Afya hazitutoshi, tena tukanunue na nyumba?

Nam. 42

Mahoteli Katika Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Inaonekana kuna wimbi kubwa la Uwekezaji wa Mahoteli na Mabaa katika Mji Mkongwe kiasi ambacho inakuwa kero kubwa kwa wakaazi wa eneo hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uwekezaji wa mahoteli katika eneo la Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 42 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii inashajiisha uwekezaji katika miradi ya kitalii. Hata hivyo mradi wowote wa kitalii hauwezi kuanzishwa na kukubaliwa na Kamisheni ya Utalii bila ya kushirikiana na taaisi husika zenye mamlaka ya eneo linaloekezwa mradi huo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mji Mkongwe, miradi inayoanzishwa hupata ridhaa ya uanzishwaji wake kutoka katika Mamlaka ya Mji Mkongwe ambayo imepewa dhamana ya kuuendeleza mji huo. Hivyo, Kamisheni haina uwezo wa kuanzisha mradi wowote iwapo wenye mamlaka hawataki kulingana na miongozo na Sheria zilizopo katika maeneo hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali langu halijajibiwa. Nilichouliza mimi kero za wananchi wa Mji Mkongwe. Sikuuliza namna ya kibali cha kupata kutoka Mji Mkongwe kutoka Uwekezaji. Swali langu halijajibiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, jibu lako limejibiwa kiusahihi na watendaji wangu, kama hulikubali jibu hili njoo ofisini ili nimfahamishe vizuri jibu alilouliza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, naamini Mawaziri wetu wajirekebisha watujibu hapa ili wananchi wapate kusikia majibu yanayotolewa na serikali yao badala ya kutujibu maofisini.

Mhe. Spika, swali langu la nyongeza kama lilivyoulizwa katika swali hili la msingi.

Kumekuwa na wimbi kubwa la uongezekaji wa mahoteli na mabaa kiasi cha kufanya *Stone Town* sasa kuwa *Hotel Town*. Suala hili linaweza likaathiri dhana nzima ya kuutangaza Mji Mkongwe kuwa ni urithi wa Kimataifa ambao hauhusu majengo tu lakini ni pamoja na jinsi ya watu walivyo na utamaduni wetu na mambo mengine yote.

Je, serikali haioni sasa wakati umefika wa kutoa tamko la kuzuia uendelezaji au ujengaji wa mahoteli au kufanya majumba ya Mji Mkongwe kufanywa Mahoteli. Badala yake uekezaji wa namna hii uelekee katika maeneo mengine ambayo pengine yanahitaji zaidi kuliko Mji Mkongwe ambao tayari umefurika kwa Mahoteli. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mimi ningependa kuchukua fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu labda wakati mwengine huwa wanachanganya.

Kwa kweli sisi hatu-*deal* na *physical investment,* sisi tuna *deal* zaidi na *operation* mambo ya uwekezaji, mambo ya ujenzi, yote yanakwenda katika kasma hiyo, wao ndio wanatoa idhini, ndio wanatoa fursa. *Once* umekubalika kule sisi tuna-*deal* na *operation.* Unapotaka kuanza kufanya *operation* ndio sisi tunaanza kukupa ile leseni kama umekidhi yale mahitaji.

Vile vile pamoja na kwamba linatugusa basi tutakaa na wenzetu wanaohusika ili kuweza kurekebisha hii hali. Lakini muelewe kwamba *investment* zote inahusika taasisi ya ZIPA sio Kamisheni ya Utalii au Wizara ya Utalii kwa ujumla. Sisi tuna-*deal* na *operation* hatu-*deal* na *physical establishment* . Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza kwa suala alilouliza Mhe. Jussa kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza tufahamu kwamba kama alivyoeleza Waziri nchi yetu bado inakaribisha wawekezaji, hasa kwenye maeneo ya utalii yaliyojengwa mahoteli. Mji wetu wa Zanzibar umekua kivutio kikubwa kabisa. Nafikiri Mhe. Jussa atakumbuka kwa sababu yeye, samahani nitatumia neno si zuri lakini namaanisha kwamba mtoto wa mjini, mtoto wa Mji Mkongwe, kakulia Mji Mkongwe. Nakumbuka Mji Mkongwe ulivyokuwa hapa kati, majumba yalikuwa yanaporomoka, yanaanguka, hayana maandalizi, hayashughulikiwi hata kidogo. Lakini limekuja wimbi jipya, *alhamdulillahi* majumba yale sasa yametengenezwa, yamekuwa mahoteli, imekuwa kivutio kikubwa.

Kama alivyoeleza Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwamba muhimu kwamba Mamlaka ya Mji Mkongwe wanasisitiza kwamba ile miundo au ujenzi ufuate urithi wa miji ya kale. Kwa hivyo bado hayo mahoteli yanayojengwa ni kivutio kikubwa, mfano mzuri Hoteli za Chavda, hoteli za Karafuu na mahoteli mengineyo.

Mimi ningemuomba sana Mhe. Jussa tuwashajihishe wawekezaji waje kuwekeza katika Mji Mkongwe. Kila mmoja ukitamka Zanzibar basi anaona raha lile jina kulitamka tu. Umekwenda Zanzibar eeh! Kuna nini? Mji Mkongwe tu ndio kitu kinachovutia. Mhe. Spika, naomba nigusie suala la Mhe. Hija la mwanzo la Mabaa katika Mji Mkongwe.

Mheshimiwa mabaa yale yanatolewa leseni na Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Wakuu wa maeneo yaani Masheha. Maombi yanapokuja sisi tunawataka wakaazi wenyewe wa maeneo yale wao waseme je, ni kero au si kero katika maeneo yao. *Alhamdulillahi* kama ni kero basi hatuwapi leseni, kama wanafanya kwa ubabe basi hilo ni suala jengine na tunachukua hatua zifaazo. Kwa hivyo kama kuna kero zozote za mabaa katika maeneo ya Mji Mkongwe nawaomba sana Waheshimiwa waje, tutazuia leseni na mabaa hayo tutayafunga.

Nam. 119

Watuhumiwa wa Makosa ya Udhalilishaji
Kukimbia Nje ya Z'bar

Mhe. Salma Moh'd Ali - Aliuliza:

Imebainika kuwa mara nyingi Watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji wa watoto hukimbia nje ya Zanzibar, jambo ambalo hupelekea wazazi wa watoto waliodhalilishwa kushindwa kuwapata watuhumiwa hao kwa kuwa hawana uwezo wa kuwafuatilia huko walikokimbilia. Je, wizara yako ina mkakati gani wa kuwasaidia wazazi hao ili haki itendeke.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji wa watoto hukimbia nje ya Zanzibar, jambo ambalo hupelekea wazazi wa watoto waliodhalilishwa kushindwa kuwapata.

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la Mhe. Mwakilishi, naomba kuelezea maelezo yafutayo kuhusu aina ya makundi ya watuhumiwa wanaokimbia Zanzibar.

(1) Kuna watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji wanaokimbia Zanzibar mara tu baada ya kufanya kosa la kitendo cha udhalilishaji kabla ya makosa yake kuripotiwa Polisi na kukamatwa.

(2) Kuna watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji wanaokimbia Zanzibar baada ya kufikishwa Polisi na kukamatwa.

(3) Kuna watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji wanaokimbia Zanzibar baada ya kufikishwa Mahakamani kupewa dhamana na Mahakama.

Mhe. Spika, makundi yote hayo matatu ya watuhumiwa wanapaswa kufikishwa mbele ya Sheria na Sheria kuchukua mkondo wake.

Mhe. Spika, sasa naomba kumuarifu Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kwamba endapo mtuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji amekimbia akiwa katika mikono ya Jeshi la Polisi au Mahakama ni jukumu na ni wajibu wa taasisi hizo mbili la kumtafuta, kumkamata na kumfikisha Mahakamani mbele ya sheria.

Mhe. Spika, Wizara yangu mara zote huwa na mawasiliano ya karibu na familia au mzazi wa mtoto aliyefanyiwa kitendo cha udhalilishaji ili kupata taarifa zitakazosaidia kufuatiliwa na kukamatwa kwa mtuhumiwa popote pale alipo chini ya msaada wa Jeshi la Polisi. Hii Mhe. Spika, imeshafanyika na baadhi ya wahalifu kukamatwa.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, tunayo mashirikiano ya kutosha baina ya Wizara yangu, Jeshi la Polisi na Mahakama katika kulishughulikia tatizo hili. Hivyo tunaomba ushirikiano wenu zaidi kutoka kwa jamii vile vile ili tuweze kuwafichua, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wote wa vitendo vya udhalilishaji ili tulikomeshe kabisa tatizo hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kutokana na jibu lako ulojibu kwamba umekubaliana kwamba kweli wahalifu wapo na wa aina mbali mbali na wanakimbia.

Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba wizara yako ifanye marekebisho ya utoaji wa dhamana ili wahalifu kama hao wasiweze kukimbia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna haja ya kutizama utaratibu mzima wa utoaji dhamana juu ya makosa haya. Lakini tujue tu kwamba kwa hivi sasa sheria zipo na Mahakama ndio yenye jukumu la kutoa dhamana katika kesi hizi, hivyo tutashauriana na Wizara ya Katiba na Sheria ili tuweze kuliangalia suala hili kwa ujumla na baadae tutizame namna gani tunaweza tukarekebisha sheria hii.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake ni jambo ambalo sikuhizi limeshika kasi kubwa sana. Kwa bahati mbaya watuhumiwa hupelekana polisi, lakini pamoja na kuwa kuna ushahidi wa kutosha basi hufanywa maridhiano kwa wale watu wawili waoane.

a) Hii ni hukumu safi kutokana na kitendo chenyewe kilivyo. Mhe. Spika, pia mimi nina ushahidi kwamba kuna mtoto mmoja amezalilishwa vibaya sana, lakini kwa sababu wenye kudhalilisha alikuwa mgumu wa kuoa, hivi sasa wamekubaliana kwamba atamuoa baada ya kuzaa na hili nalo ni sawa.

b) Mhe. Spika, hivi wizara husika inachukua hatua gani kuona kuwa udhalilishaji unapungua na kuwa hukumu ambayo si halali mwenye kuhukumu anachukuliwa hatua.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, hapa naomba kwanza tutofautishe unapokuwa na kesi ukaipeleka polisi na baadae wazee wa mtoto wakakubaliana na polisi kwamba wayasawazishe kwa watoto kuoana hilo ni suala jengine na ni suala ambalo madhali wameshakubaliana wao wenyewe nafikiri serikali haiwezi kuingilia sana katika utaratibu huo. Lakini pale ambapo alodhalilisha amekamatwa na halafu ikawa vyombo vyovyote vile vyengine havichukui hatua za kutosha za kumchukulia hatua yule aliyedhalilisha hilo ni tatizo ambalo wizara yangu inajitahidi kulipigia vita suala hilo.

Mhe. Spika, utakumbuka kwamba hivi karibuni tulifanya mkutano na vyombo vyote vya polisi, Wakuu wa Polisi wa Mikoa yote, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili kujaribu kuwahakikishia kwamba suala hili ni zito na kuwaomba kwamba wao ni lazima washirikiane na wizara yangu ili matokeo kama haya tuweze kuyadhibiti kwa hali ya juu kabisa. Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba vyombo hivi pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wazee tutashirikiana kwa pamoja ili wahalifu wa aina hii tuweze kuwakamata na tuweze kuwachukulia hatua ipasavyo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali karibu sana kumalizika kuna dakika kama mbili tu, kwa hiyo haraka haraka nimuombe Mheshimiwa tuendelee na suala lilobaki ili tutaongeza muda mchache sana ili kulimalizia suala hili tuendelee na bajeti yetu ya serikali.

Nam. 8

Wafanyakazi wa Shirika La *ZSTC*

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:

Kwa kuwa shughuli nyingi zilizokuwa zikifanywa na Shirika la *ZSTC* hapo zamani kwa sasa hazipo tena. Shirika limebaki na ununuzi wa karafuu tu, ambao pia unaathiriwa kutokana na biashara ya magendo.

Na kwa kuwa pamoja na kuondolewa shughuli zake bado Shirika limebakiwa na wafanyakazi 265 na wengi wao hufika Afisini na kukaa bure bila ya kuwa na majukumu ya kufanya kazi lakini bado wanalipwa mishahara.

(a) Kwa kuwa Shirika lipo katika hali mbaya kwanini lisiwezeshwe kifedha hata kama kwa mkopo ili liagize bidhaa kama vile mchele, unga, sukari na kadhalika.

(b) Kwa kuwa wafanyakazi wengi wa Shirika hawana shughuli za kufanya kwanini Wizara isiwahamishie wafanyakazi hao katika Taasisi na Idara nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatayo:-

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar miongoni mwa mikakati yake iliyojiwekea ni kuyaongezea ufanisi mashirika

yake kwa kuyafanyia marekebisho ili yajiendeshe kibiashara na kuleta tija kwa serikali pamoja na wafanyakazi na nchi kwa jumla, kuhusiana na suala la kuipa ZSTC jukumu la kuagizia bidhaa. Jengine Mhe. Spika, suala hili linafanyiwa uchambuzi wa kina ili kuepuka makosa ya kiutendaji kama ambavyo yaliweza kutokea wakati linafanyiwa marekebisho Shirika lile la Bizanje.

b) Mhe. Spika, tatizo la wingi wa wafanyakazi ni miongoni mwa masuala ambayo yanatafutiwa ufumbuzi ndani ya Shirika la *ZSTC*. Hata hivyo, labda niseme tu kwa ujumla kuwa Shirika la *ZSTC* limo katika mchakato wa kufanyiwa marekebisho (*Re-structuring*) ili liweze kumudu kufanya kazi zake ipasavyo na kuleta tija kwa taifa. Hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Mhe. Spika, watusaidie katika kuelimisha wananchi juu ya suala hili wakati Serikali ikiendelea na hatua ilizozianza ili hatimae mafanikio tunayoyategemea yaweze kupatikana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa serikali haijakuwa makini kujua inafanya nini katika zao hili kupandisha bei au zao hili kulibinafsisha. Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kama ndio sababu ya kusafirishwa kimagendo zao hili na wananchi kufuatia kipato zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ningeomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba suala la msingi linahusiana na ZSTC na sio bidhaa ya karafuu. Ningeomba nijibu kwa utaratibu unaotakiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mwakilishi hebu uliza tena swali lako.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, suala la karafuu nadhani hapa lipo na mimi ndio suala nilouliza na suala la kusafirisha kimagendo pia lipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kama alivyoahidi Mhe. Rais katika ziara yake ya Pemba hivi karibuni siku ya majumuisho ya Mkoa wa Kusini, Mhe. Rais aliahidi kwamba zao la karafuu bei yake itaongezwa na mimi kama ni waziri wa wizara hiyo nina jukumu kubwa la kuona kwamba ile kauli ya Mhe. Rais inatekelezwa kwa vitendo. Kwa hivyo, naomba kuwahakikishia wananchi kwamba zao la karafuu bei yake itaongezwa kama Mhe. Rais alivyoagiza na tunaamini kwamba kwa mchakato tutakaofanya tutawapatia wananchi bei nzuri kabisa kutokana na bei ya soko la dunia

inavyokwenda. Mhe. Spika, kwa hali hiyo basi tuna imani kwamba tutashirikiana sote kwa pamoja suala la magendo litaondoka kabisa.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba siku ya Jumatano wiki iliyopita Bajeti hii iliwasilishwa mbele yetu wakati wa jioni na ilikwisha ungwa mkono na Waheshimiwa Wajumbe karibu wote kwa kusimama kuashirikia kwamba sasa majadiliano yanaweza yakaanza, na kwa maana hiyo kama Katibu alivyoainisha kwamba sasa majadiliano yaanze. Nataka nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti ambaye atatoa maoni ya kamati yake na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwa utaratibu kabisa baada ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kumaliza tuweze kujadili kama alivyoomba Mhe. Waziri mwenyewe Bajeti hii ya Serikali kwa uwazi, utulivu na tupange mada na points zetu vizuri ili kumsaidia Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla katika suala hili la Bajeti yetu ya Serikali. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kutoa maoni ya kamati.

(Mhe. Hamza Hassan Juma) (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti) Mhe Spika, kwanza hatunabudi kumshukuru MwenyeziMungu kwa kutuwezesha siku ya leo kufika hapa tukiwa wazima wenye afya njema kuweza kuwatumikia wananchi wetu wapendwa wa Zanzibar.

Mhe Spika, pili. tunakupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuendelea kutuongoza kwa busara na uadilifu mkubwa kwenye Baraza letu hili la Wawakilshi la Zanzibar bila chuki, au upendeleo wowote na hili hakuna mtu miongoni mwetu atakaebisha.

Mhe Spika, tatu tunampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwake kuwaongoza wananchi wa Zanzibar, tunaamini atatuongoza kwa uadilifu mkubwa bila ya chuki au upendeleo wowote kama anavyotueleza kila siku kwenye hotuba zake. Hivyo, tunamuomba Mwenyeenzi Mungu ampe hikma , busara na mafanikio makubwa katika uongozi wake ili nchi yetu ipate mafanikio makubwa katika maende;eo na kuuondoa umaskini hapa Zanzibar.

Mhe Spika, nne tunampongeza sana Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar aliyevuliwa hivi karibuni ambaye tulikuwa naye hapa Barazani Mhe. Jaji Omar Othman Makungu, naye tunamuombea mafanikio katika kazi yake hiyo mpya na tunaamini anao uwezo mkubwa kwani ni jaji mzoefu na ameshakuwa na uzoefu katika shughuli mbali mbali za kuwatumikia wanachi katika kusimamia haki zao, pia ni mcha Mungu mkubwa naye tunamuombea Mwenyezi Mungu ampe wepesi katika kazi zake mpya na Mwenyezi Mungu atamsaidia Inshaallah.

Mhe Spika, tano tunampongeza sana Mhe Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutusomea hotuba ya hii ya Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba ambayo ameisoma kwa muda masaa mawili bila ya kuchoka. Lakini ameisoma kwa ufundi na umahiri mkubwa.

Mhe Spika, pia tunawapongeza Mawaziri wote walioteuliwa kumsaidia Mhe. Rais katika kazi zake. Pamoja na Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, na watendaji wote walioteuliwa kumsaidia Rais isipokuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwani wao bado hawajateuliwa kuitumikia Serikali hii ya awamu ya saba.

Mhe Spika, bila ya kuwasahau pongezi kwa Waheshimiwa wenzangu wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa na wananchi wetu kuja kuwawakilisha hapa Barazani tunakutakieni kila la kheri katika kuwatumikia wananchi wetu kwani hii ndio kazi tuliowaomba na wakatuamini kuwa tutawatumikia.

Mhe Spika, mwisho kabisa kwa heshima zote nawashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwamtipura kwa kunichagua na kunileta hapa kuja kuwatumikia, nnawaahidi kwamba nitajitahidi kuwatumikia kwa juhudi, uzoefu na uwezo wangu wote ili kukidhi matarajio yao kwenye jimbo letu na nchi kwa jumla.

Mhe Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba niendelee moja kwa moja kuanza kuchangia hotuba ya bajet hii iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar.

Mhe Spika, katika suala amani na utulivu uliopo hivi sasa hapa Zanzibar kwanza ni lazima tumshukuru na kumpa pongezi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete pale alipolihutubia Bunge la mwanzo la Bajeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale alipotamka kwamba atahakikisha ndani ya kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ya uongozi wake kwamba mpasuko wa kisiasa

uliopo Zanzibar atupatia ufumbuzi. Baada ya hapo aliunda kamati ya Makatibu Wakuu wa CCM na CUF na matunda yake ndio haya tunayojivunia hivi sasa. Kwa hiyo, katika vitabu vya kumbukumbu Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete anaingia bila ya ubishi kwa amani na umoja uliopo hapa Zanzibar, tunamshukuru na Mwenyezi Mungu atamlipa kwa hili.

Mhe Spika, pia katika kuitikia wito wa Mhe. Rais Kikwete wa kuondoa mpasuko na kuleta amani Zanzibar pia tunampongeza Mhe. Mwakilishi Mstaafu Mhe. Abass Muhunzi pale alipoondoa ukimya na akazungumza ndani ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi kwamba wanasiasa tuache usanii wa kutoitambua serikali wakati tunashirikiana kwa kila kitu. Mhe Spika, ingawa baadhi ya Waheshimiwa walichukia, lakini leo wao ndio wanaopata matunda ya mafanikio hayo pamoja ya kwamba yeye Mhe. Muhunzi yuko nje ya uwanja. Tunamtakia kila la kheri katika maisha yake mapya ya uraiani.

Mhe Spika, kwa maridhiano yaliyofikiwa na vyama vyetu CCM na CUF pongezi maalum ziende kwa Rais mstaafu wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuamua kumaliza mzozo wa kisiasa uliodumu kwa muda mrefu hapa Zanzibar, kwa kukubaliana kuunda Serikali yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa baada ya uchaguzi mkuu wa 2010, na hivi sasa ndio tuliyonayo, na tunafanya kazi kwa pamoja bila ya chuki wala bughudha, na hivi sasa nchi yetu imo katika hali ya amani na utulivu mkubwa, ambayo ndio sera ya CCM. Kwa hiyo, natoa wito kwa Wazanzibari kuitumia fursa hii kujituma kwa juhudi na maarifa ili kujikwamua na hali ya umasikini ili tuishi vizuri na familia zetu kwa jumla.

Mhe Spika, hii amani na utulivu iliyopo ni matunda ya sera nzuri ya CCM inayoweza kutekelezeka na hata vyama vya upinzani, kwa hili tunampongeza sana Mwenyekiti wa CCM taifa kwa busara na hekima zake katika kusimamia amani na utulivu hapa nchini Tanzania.

Mhe Spika, hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka huu 2011/2012 ni nzuri na inalenga kumkomboa mwananchi pamoja kasoro ndogo ndogo zilizopo tunaamini Waheshimiwa wataichangia na kutoa ushauri unaofaa ili kuiboresha na kushauri mwakani tufanye nini ili iwe nzuri zaidi.

Mhe Spika, tukitaka tusitake muundo wa Serikali yetu uko kimaridhiano zaidi kuliko umoja wa kitaifa, kwani serikali ni kubwa sana kuanzia mawizara mengi, mawaziri ni wengi, makatibu wakuu na pia wakurugenzi ni wengi sana. Kwa hiyo, ukiangalia ni fedha nyingi sana za

umma zinatumika kwenye utawala kwani kuwahudumia watendaji hao ni mzigo mkubwa kwa wananchi wetu ambapo tulifikiria serikali ingelikuwa ni ndogo sana ambayo ingelikuwa na uwajibikaji mkubwa na fedha nyingi zingelikwenda kuwahudumia wananchi kwenye huduma za kijamii na maendeleo. Tunaamini pengine hiyo nyongeza ya mishahara inayotegemea kuongezwa kwa kipindi hiki na Serikali wafanyakazi ingelikuwa kubwa zaidi kuliko itakavyokuwa hivi sasa.

Mhe Spika, hili naamini wengine litawaudhi lakini ni vyema sisi Wawakilishi wa wananchi tukaeleza yaliyomo ndani ya hisia za wananchi wetu kuliko kuyanyamazia kwani tunaamini hii ni serikali ya watu na inapaswa kuwasikiliza hisia za wananchi wake.

Mhe Spika, kunamwanafalsafa mmoja Bw. Martin Lutherking alisema kwamba "ukimya wa rafiki yako unaumiza sana kuliko kelele za adui yako".

Mhe Spika, hotuba ya Bajeti imejaribu kutoa taaswira ya hali halisi ya mwenendo wa uchumi wetu tangu mwaka 2009-2010, na matarajio ya mwaka 2011-2012. kwa hiyo, hali ya uchumi wetu huwa inabadilika kila mwaka hasa kuzingatia bei za mafuta kupanda duniani na kushuka mara kwa mara pamoja na mfumko wa bei ulotokea duniani.

Mhe Spika, kitu ambacho tunaipongeza serikali kupitia Bajeti hii ukiangalia *program* karibu asilimia 70 za maendeleo ni muendelezo wa *program* zilizopita katika serikali ya awamu ya sita ambayo ilipiga hatua kubwa tu za maendeleo kiuchumi na zilizobaki 30% ni mpya. Hii inatupa faraja kwani ni vyema yale mema yote yalioachwa tukayaendeleza kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe Spika, katika hotuba yake UK – 4, Mhe. Waziri ameelezea ni namna gani serikali imejipanga kutekeleza ahadi ilizoahidi wakati wa kampeni ya uchaguzi wa mwaka 2010, hili linatupa faraja na tunaona ni kiasi gani Rais wetu alivyokuwa mkweli katika yale yote aliyoyaahidi najua Waheshimiwa wengi pamoja na mimi katika majimbo yetu kuna ahadi nyingi alizozitoa Mhe. Rais basi ni wajibu wetu sisi kukumbushia kupitia katika wizara husika, kwani wengine hawakuwepo wakati zilipotolewa.

Mhe Spika, **B**ajeti ya Serikali imelenga mambo matatu makuu, kutekeleza malengo ya *vision 2020* imejikita zaidi katika kuutekeleza MKUZA ambapo vipaumbele ni 1) Kuinua Uchumi na Kuondoa Umasikini, 2). kuimarisha utawala bora na 3) Kuboresha Huduma za jamii, na Katika kuutekeleza utawala bora basi tunaiomba serikali iandae mazingira

mazuri kwa Baraza letu la Wawakilishi kuwa na fungu lake maalum kwani kwa mfumo tulionao hivi sasa inaonekana serikali ina nguvu kubwa na hata wakati mwengine kuingilia kati majukumu ya Baraza la Wawakilishi wakati sio sahihi, tunaamini serikali yetu ni sikivu hili litatekelezwa haraka na tunaamini itaondoa sitofahamu kati Serikali na chombo hiki cha kutunga sheria. Pia tunaiomba serikali kuuangalia muhimili wa tatu wa dola (Mahkama) kwani wao hawapati fursa kama sisi kuzungumzia mambo yao.

Mhe Spika, klasta ya pili ya MKUZA ni kuuimarish utawala bora hii ni kazi ngumu sana kwani utawala bora unahitaji uwazi (*TRANSPARENCY*) ambapo wananchi wanapaswa kujua kila kitu wanapohitaji maelezo kutoka serikalini, namna rasilimali za nchi zinavyotumika basi musiwe wakali na kutoa kauli kali, busara zitumike katika kuwaelimisha wanachi rasilimali zao zinavyotumika, kwani katiba ya Zanzibar kifungu cha 23 (2,na 3) kinafafanua vizuri ,kwamba kila mtu anpaswa kulinda mali na rasilimali za nchi na kupiga vita aina zote za ubadhirifu na uharibifu wa rasilimali na Wazanzibari wenyewe (wananchi) ndio wenye maamuzi ya hatma ya nchi yao. Pamoja na hayo ili kuutekeleza utawala bora kwa vitendo basi ni vyema sisi Waheshimiwa tuwe mfano kwa kutangaza mali zetu pamoja na watendaji wakuu wa serikali ili kuonyesha ni namna gani tulivyopata mali hizo, kwa hiyo tunaitaka serikali kuleta mswaada wa sheria ya kutaka kuziorodhesha mali zetu kwani hili ni miongoni mwa utawala bora tunajua hili ni gumu lakini hayo ndio matakwa ya utawala bora.

Mhe Spika, uhuru wa vyombo vya habari ni sehemu ya utawala bora kwa hiyo tunawataka mawaziri na watendaji wakuu wa serikali kutoa mashirikiano na waandishi wa habari pale wanapohitaji taarifa hata kama zinawagusa nyinyi binafsi, kwani waandishi wa habari wanchangia kwa kiasi kikubwa kuibua maovu na ufisadi katika jamii na tunashuhudia mambo mengi tunayapata kupitia vyombo vya habari, lakini inaonyesha bado kuna baadhi ya watendaji serikalini wanawahisi waandishi kama ni maadui kwao wakati kumbe kama watakuwa waadilifu basi waandishi ndio wawafanye wenzao kwani hata ukifanya mazuri ya aina gani kama hayakutangazwa basi yanakuwa ni bure tu. Hili hata Mhe. Rais mwenyewe amelisisitiza kwenye ziara zake kwa watendaji kuwaelezea wananchi yale serikali inayoyafanya ili wananchi wajue serikali yao nini inafanya. Je, bila ya vyombo vya habari wananchi watapashwa habari na nani?. Kupitia kikao hichi tunawapongeza sana vyombo vya habari kwa kazi yao kubwa ya kuelimisha umma. Na wala wasiwe na hofu wakti wanapofanya kazi zao.

Mhe. Spika, pia katika klasta ya tatu kuboresha huduma za jamii na huduma za elimu Zanzibar tumebahatika serikali kwa kushirikiana na wananchi tumejenga maskuli mengi mijini na vijijini na hivi sasa tumevuka lengo la Milenia kwani hakuna mtoto aliyetimiza umri wa kwenda shule akakosa nafasi, lakini bado tunaiomba sana serikali yetu kusomesha walimu wengi zaidi ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu katika maskuli yetu.

Pia tatizo jengine ni madarasa yetu kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi huwafanya waalimu kutoweza kuwakaribu nao kufuatilia maendeleo yao. Tunaiomba serikali kuzipatia vifaa vya maabara zile skuli zinazosomesha masomo ya sayansi, pia kusaidia wanachi kumalizia majengo ya shule yaliokwama kutokana na ukosefu wa fedha, pamoja na maboresho ya mishahara ya walimu yaangaliwe kwa umuhimu wa aina yake kwani huwezi kupata mafanikio ya kimaisha bila ya kufundishwa na mwalimu. Lakini walimu wanageuka ngazi tu kwani wanafunzi wao baadae huwa na maisha mazuri lakini wao wanabaki pale pale ndio maana baadhi yao huacha kazi hiyo na kujiunga na siasa kama baadhi yao wamo humu ndani ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe Spika, tumeona jitihada za serikali baada ya Baraza lako tukufu kupitisha sheria ya kuanzisha Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu tayari kwa muda mfupi tu karibu wanafunzi 1,271 wameshapata mikopo hiyo na 1,058 wanasoma vyuo vya ndani na 213 vyuo vya nje. Tunaipongeza sana serikali pia tunafarijika na taarifa ya ya kukamilika kwa shule 15 za Sekondari vijini mwishoni mwa mwaka huu hizi pia zitasaidia kuongeza wasomi hapa Zanzibar. Lakini pia tunaiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu kuwasaidia Kikosi cha JKU kuwatafutia wahisani kujenga shule yao ya Sekondari ambayo itakuwa kisasa kwani wanalo eneo kubwa sana na wameshajitahidi sana kutafuta misaada lakini bado hawajafanikiwa.

Mhe Spika, huduma za maji safi na salama ingawa serikali imeahidi kuchimba visima vingine 52 kwa Unguja na Pemba, lakini hapa tunatoa angalizo inaonyesha watendaji wa Mamlaka ya Maji uwezo wao wa kazi ni mdogo au wanafanya makusudi kuwakosesha wananchi huduma hiyo ya lazima. Mhe Spika, tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais suala hili alifanyie kazi ya ziada, kwani hata hiyo nyongeza ya mshahara mtakayoitoa basi itaishia kununulia mageloni ya maji tu Kwa hiyo, hapo ndipo panapochangia kwa kiasi kikubwa huo umasikini ambao upo hapa Zanzibar.

Mhe Spika, tunatoa mwaka mmoja kwa Mamlaka ya Maji kutatua tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi, vinginevyo tutaitaka serikali kuikabidhi Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuifanya kazi hiyo, kwani tunaamini wanao wataalam na mafundi mahiri na wataweza kutatua tatizo hilo. Pili tunaishauri Mamlaka ya Maji kuugawa mji kwa ma-*block* ili kutatua *block* moja moja kuliko ilivyo hivi sasa kwani ni Mji Mkongwe tu peke yake ndio wanaopata maji kwa uhakika, sijui hapa kuna siri gani.

Mhe Spika, tunapongeza jitihada za serikali katika kuyalinda makundi maalum, ikiwemo walemavu, wanawake, watoto, pamoja na wazee. Tunapongeza serikali kwa kusema kuwa katika bajeti kuu ya serikali kuwa wazee wataongezewa posho ya kujikimu na kushughulikia nyumba za wazee. Tunaishauri serikali pamoja na makampuni, mashirika na wafanyabiashara wakubwa kutenga fungu maalum kila mwaka kuwasaidia wazee hao, kwani haya mafanikio tunayoyapata hivi sasa kuna mchango mkubwa na wao waliutoa kwa njia tofauti wakati wa ujana wao, pia serikali kuwajengea sehemu ya kufanyia mazoezi ili kuzidi kujenga afya zao.

Tunampongeza sana Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto jinsi anavyoshughulikia wazee hivi sasa. Na hii ni kutekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi wa CCM. Lakini pia tuipongeza serikali kuanzisha *ONE STOP CENTRE* hapo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kushughulikia kesi za udhalilishwaji wa watoto, kwani vitendo hivi vimeshamiri hivi sasa hapa kwetu na wananchi walishindwa cha kufanya pale walipofikwa na majanga kama haya ya udhalilishwaji, lakini tunaiomba serikali kuchukua hatua kali sana kwa wale wote watakao husika na vitendo hivyo.

Mhe Spika, Klasta ya kwanza ya utekelezaji wa programu ya kuondoa umaskini **(**MKUZA**)** ni **u**wezeshaji kiuchumi kwa wananchi wetu. Mhe Spika, pamoja na nia nzuri ya serikali, eneo hili linahitaji uangalizi maalum kwani hivi sasa pesa nyingi za serikali zimeshatoka kwa kukopesha wananchi kupitia Mfuko wa A.K na J.K, lakini ni asilimia 50 tu ndio zilizorejeshwa, hii inatokana na kutokuwa na maandalizi mapema kwa wanaopewa mikopo hiyo. Serikali nadhani ingelikiimarisha zaidi kikosi chetu cha J.K.U kwa kuwapatia zana za kisasa ili kuwafunza vijana wetu taaluma ya ufundi mara tu baada ya kumaliza shule na baadae kuwapatia elimu ya biashara na mtaji wakaanze maisha mapya ya kujitegemea bila ya kutegemea ajira serikalini.

Mhe Spika, hivi sasa taasisi tofauti za serikali zinatoa mikopo kwa vijana, swali hapa kwa nini shughuli hizi za utoaji wa mikopo zisitolewe na wizara moja tu? Kwani ndio kutakapokuwepo na usimamizi mzuri pia kujua changamoto zinazowakabili wananchi wetu na kuweza kuzishughulikia.

Pia tunatoa ushauri kwamba mikopo itakapoanza kutolewa basi kipaumbele wapewe *SACCOS* kwani zitasaidia kuwafuatilia wale wanachama wao wote kwa karibu popote pale walipo na hata sisi majimboni itasaidia kuwa karibu nao na kutoa ushauri kila mara na kuhamasisha kufanya marejesho ili waweze kupata na wengine, lakini kwa utaratibu wa kumpa mtu mmoja mmoja hakuna mheshimiwa atakaeweza kujuwa walipo na kufuatilia maendeleo yao.

Hapa pia tunaomba ufanyike utafiti wa kutosha hasa katika miradi ya wananchi ikiwemo ya *TASAF*, *PADEP* kwani ni pesa nyingi zimeshatoka zimewafikia walengwa, lakini unapoitembelea miradi hiyo bado utakuta haijawaondolea umaskini wananchi hao, kwani malengo yetu wale wanaopatiwa misaada hii basi wajitegemee kimaisha kupitia miradi ile wakati miradi hii ni misaada na sio mikopo, lakini bado inasuasua. Je, kama wangelipewa mikopo nadhani *TASAF* na *PADEP* wangelikuwa wameshawapeleka mahakamani wananchi wengi. Hapa ni lazima serikali ifanye tathmini ya kutosha ili kuwa na miradi ambayo itawaondolea wanchi wetu umasikini.

Mhe Spika, hapa pia naomba kuunganisha na sekta ya fedha ambapo pamoja na jitihada za serikali kuhamasisha kuanzisha mabenki na kufungua matawi yao hapa Zanzibar lakini bado mabenki haya hayajasaidia sana kuinua wananchi wetu, kwanza masharti yao ni magumu kupata mikopo, lakini hata hao wanaopata mikopo hiyo riba ni kubwa sana, kwani kiwango kinachotolewa na benki cha riba ni asilimia 19 hadi 22, hiki ni kikubwa sana na zaidi kinazinufaisha benki sio wananchi, kwani kama mwananchi anaweka pesa katika mabenki hayo hupata riba isiozidi asilimia sita. Mhe. Spika, hii ni tofauti kubwa sana kwa hiyo, tunaiomba serikali kuongea na *B.O.T* ili kuangalia tofauti ya viwango kwani *B.O.T* ndio inayosimamia viwango vya riba za mabenki hapa Tanzania.

Mhe Spika, hapa pia tunaitaka serikali kuyabana mabenki kupunguza riba kwa wafanyakazi wa serikali waliokopa, kwa kuwa serikali ndio iliyobeba dhamana hiyo na kuna uhakika wa asilimia 99 ya kulipwa pesa hizo kupitia mishahara yao, ambapo moja ya sababu ya madai ya mabenki yetu kudai riba kubwa ni kusema kwamba kutokuwa na uhakika wa malipo ya mikopo hiyo. Kwa hiyo, kikwazo hicho kwa watumishi wa serikali hakipo na hii ndio kuitekeleza kwa vitendo programu ya kuuondoa umaskini.

Mhe Spika, katika mkakati wa serikali wa kufanya mapinduzi ya kilimo hapa Zanzibar, bado naona tunayo safari ndefu kwani bila ya kuwa na Benki ya Kilimo ambayo itatoa mikopo nafuu kwa wakulima basi suala hili litakuwa ni gumu utekelezaji wake, kwani wakulima wapo wengi lakini uwezo wao wa

kifedha ni mdogo. Kwa hiyo, kazi kubwa ya utekelezaji wa mpango huo utakuwa ni wa serikali peke yao, kwani wao ndio wenye fedha na wananchi watakuwa ni watazamaji tu na hilo lengo la serikali halitofanikiwa. Mfano hai uliopo Mhe. Spika, kwani kuna miradi mingi inyofadhiliwa na wahisani ya kilimo hutekelezeka vizuri tu pale wanapokuwepo wahisani kwa sababu wana fedha, lakini tumeshuhudia wakiondoka tu basi miradi inakufa kwani wananchi wanaokabidhiwa miradi hiyo huwa hawana fedha za kuendeleza miradi hiyo.

Mhe Spika, serikali inasema ina mkakati wa kuimarisha kilimo lakini hali inaonyesha ni kwa maneno zaidi kwani tulitegemea waziri angelisema hivi sasa tayari wameshaleta matrekta alau kumi mapya, lakini inaonyesha kipaumbele ni kuimarisha wakubwa kwani tumeona kabla ya kusomwa bajeti kuu ya serikali tayari kipaumbele cha mwanzo cha serikali hii ni kununua magari mapya ya wakubwa, sijui magari haya yana uwezo wa kulima ekari ngapi za mpunga kwa siku, labda Mhe. Waziri atakuja kutueleza atapokuja kusimama hapa.

Mhe Spika, bado kilimo ndio uti wa mgongo wa wananchi wetu na taifa letu tunaiomba serikali kuleta matrekta kwa wingi ili kuwaondoa wakulima wetu katika kilimo cha kizamani kilichopitwa na wakati cha kulima kwa jembe la mkono, hivi sasa bado kuna mabonde mengi ya mpunga hayalimwi kwa muda mrefu ambapo wanachi hupelekea kuyavamia na kujenga nyumba za makaazi na kuishi,

Mamlaka ya Maji tunaiagiza kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili kuchimba visima vya maji kwenye mabonde ya mpunga ili kuwezesha wakulima kulima kwa kumwagilia maji kitu kitakacho wafanya waweze kulima mara mbili hadi tatu kwa mwaka, ambapo itasaidia kuongezeka kwa chakula hapa nchini. Pia itasaidia kupunguza uagiziaji wa chakula na kupunguza nakisi ya uagiziaji wa chakula hapa nchini. Mhe Spika, Mwenyezi Mungu ametujaalia tuna ardhi nzuri na maji ya kutosha lakini bado mipango yetu hatujaiweka sawa kuitumia ardhi yetu vizuri.

Mhe Spika, kama tutayatumia vizuri mabonde ya mpunga tulionayo basi suala la kujitosheleza kwa chakula hapa Zanzibar litawezekana. Mhe Spika, tunatoa ushauri serikali kuiimarisha JKU ili kuwapa fedha za kutosha ili kuwachukua vijana wote wanaomaliza skuli na kuacha kukaa vigogoni tu bila ya kazi ili kwenda kujenga taifa, kuwapatia ujuzi wa ufundi na kuwashirikisha katika kilimo mbali mbali ikiwemo mboga mboga ambapo kilimo hicho ni muhimu sana hasa kutegemea soko kubwa la utalii liliopo hapa Zanzibar, kwani mboga mboga nyingi tunaagiza kutoka nje ya Zanzibar.

Hiyo ni ajira kubwa sana na ina pesa nyingi inaweza kuwalipa posho la sabuni kila mwezi vijana hao na naamini vijana wengi watavutiwa kujinga na JKU wataacha kuzurura mitaani na kukimbilia Darajani kuuza kufuli pamoja na madawa ya kulevya. Serikali isione tabu kutumia pesa kwani tunataka kujenga taifa la vijana wenye moyo wa kujitegemea ndio maana tukashauri serikali iwe ndogo ili pesa nyingi ziende kwenye kazi na sio kununulia magari ya wakubwa.

Mhe Spika**,** utalii kwa sasa ndio lango letu kuu la uchumi la kutuingizia mapato kwa nchi yetu. Mhe. Spika, kamati yangu haijaridhika na maamuzi ya serikali yetu kuuweka utalii katika Wizara ya Habari, nadhani ili kuweza kuushughulikia na kudhibiti mapato yatokanayo na utalii basi ni vyema ukapelekwa Wizara ya Biashara na Uekezaji ili kukusanya masuala ya uchumi kwenye wizara moja, kwani hata huko nyuma ilikuwa hivi, lakini kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na umuhimu wa utalii kwa mapato ya nchi basi serikali iliufanya utalii kubeba jina hata la wizara, tunaelewa utalii unatakiwa uendane na utamaduni lakini kwa sasa umekwenda mbele zaidi kiuchumi.

Mhe Spika, sekta ya utalii ni sekta mtambuka kwani inatoa mapato ya moja kwa moja yanayotokana na watalii wenyewe. Lakini pia inatoa ajira nyingi sana kwa vijana na wananchi wetu. Mfano, ajira hizo zinazotoka sio moja kwa moja katika njia ya watalii, ni kwa wenye magari ya kubebea watalii na *Taxi*, wakulima wanaolima mazao ya matunda, mboga mboga na samaki, nyama, kuku, wauza mafuta ya petroli na dizeli, mafundi wa magari, mama ntilie wanaowahudumia wafanyakazi wa mahoteli, wauza vinyago na vitu vya asili, wakodishaji wa nyumba za kuishi pamoja na *Guest Houses*, skuli na taasisi za lugha za kigeni, makontrakta na wajenzi pamoja na vibarua, wauzaji wa vifaa vya ujenzi wa mahoteli na wafanyakazi wanaojenga kupitia mishahara yao inayotokana na mahoteli na biashara nyingine inayohusiana na utalii, wakodishaji wa boti na mashua kwa wageni, wakodishaji vipando vya moto, wauzaji wa maji, huduma ya umeme, watembeza watalii, wanaosuka, kupaka hina. wanaokanda watalii **(***Massage***),** wazoaji taka, wakulima wa mazao mbali mbali na kadhalika. Kwa

Hii Mhe. Spika, ni mifano tunaonyesha utalii jinsi gani unavyotoa ajira kwa wananchi wengi zaidi basi ni lazima serikali yetu iliangalie kwa umuhimu unaostahili kwa uchumi wa nchi yetu. Mhe Spika, cha kushanagaza sana sijui serikali yetu imefikiria nini kukuza utalii hapa Zanzibar, kwani kwa bajeti ya mwaka huu sijaona fungu la kuutangaza utalii nchi za nje ambapo ndio njia moja kubwa inayosaidia kuwaita watalii wengi kutoka nchi mbali mbali, hii inaonesha tumewaachia wenye mahoteli wenyewe kuutangaza utalii wetu. Hapa ni lazima tuwe makini sana, kwani sekta hii ikiporomoka basi Wazanzibari wengi wataathirika. Pia ukiangalia hiyo sekta ya mahoteli ya

kitalii kuna haja ya serikali kuwasaida waekezaji wazalendo ili kuweza kumudu ushindani wa kibiashara na wageni ambao wana uzoefu mkubwa katika biashara hiyo ya utalii.

Mhe Spika, kwa kuwa utalii ndio uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu, basi ni vyema serikali kujenga chuo kikubwa cha utalii hapa Zanzibar kwani tunakosa kuwa na mameneja wazalendo kwenye mahoteli yetu na matokeo yake ajira hiyo huchukuliwa na wageni.

Mhe Spika, sekta hii ina umuhimu mkubwa kwa taifa letu kwa hiyo, tunatoa wito kwa serikali kuimarisha ulinzi kwenye ukanda wa mahoteli ya kitalii, ingawa hivi sasa nchi yetu iko katika hali ya amani na utulivu lakini bado kuna watu wachache wanaotishia amani ya usalama kwa wanachi pamoja na wageni wetu. Mhe Spika, tunaionba serikali kuangalia kwa karibu mapato ya utalii kwani kuna baadhi ya nchi ndogo kama yetu ya Afrika kama vile nchi ya Botswana inapokea watalii kidogo sana lakini inaingiza mapato kwa wingi.

Mhe Spika, kamati yangu ya wenyeviti inamuomba Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuipeleka Kamati ya Wenyeviti kule Botswana ili ikaone na kujifunza ni siri au uchawi gani nchi ile inatumia na kuweza kukusanya mapato kwa wingi ili ije kuishauri serikali ni namna gani ya kuinua mapato ya utalii. Mhe Spika, nadhani Mhe. Waziri ni msikivu na hili nadhani atalitekeleza.

Mhe. Spika, wajumbe wako tunahitaji sana kutoka nje ya nchi ili kuona hatua walizopiga wenzetu na sisi tuje kuiga yale yalio mazuri. Pamoja na mapato yanayotokana na utalii bado utalii wetu unachangia uharibifu mkubwa wa mazingira katika nchi yrtu, basi ni vyema kutilia mkazo kodi ya uhifadhi wa mazingira ili kusaidia kurejesha hali ya mazingira pale yanapoharibiwa.

Mhe Spika, suala la nishati ni suala muhimu sana katika taifa letu kwani bila nishati hakuna maendeleo. Tunaishukuru serikali yetu kwa kuendelea kuukamilisha mradi unaoendelea wa kuleta umeme mkubwa wa *Kilowatt 100*, unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la (*MCC*)**.** Pia tunapongeza sana jitihada zinazoendelea kwa kushirikiana na sekta binafsi kuwekeza katika umeme wa upepo na jua, lakini bado kamati yangu haijaridhishwa na jitihada za serikali hii ya Awamu ya Saba namna ya kutatua tatizo la nishati ya kudumu na ya uhakika hapa Zanzibar, kwani masuala ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi hapa Zanzibar serikali imeamua kwa makusudi kulifumbia macho kwa kukaa kimya wakati serikali ya Awamu ya Sita ililivalia njuga suala hili ili kulipatia ufumbuzi suala hilo, ililishirikisha Baraza la Wawakilishi kikamilifu katika mashirikiano katika kila hatua.

Lakini sasa hivi Mhe Spika Baraza lako limewekwa kizani hatujui kinchoendelea na ndio maana waziri aligusa kidogo kwani hakuna hatua yeyote inayochukuliwa kwa sasa, wakati ambapo kama jitihada za uchimbaji wa mafuta zikianza tunaamini gesi itapatikana na kupatikana kwa gesi hapa Zanzibar tungeweza kuitumia kwa kuzalisha nishati ya umeme na kupikia, hapa tungeliweza kuokoa uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa kuepuka ukataji wa miti ovyo, lakini pia tungeliweza kuzalisha umeme wa kutosha kwa kutumia gesi na pengine kutokana na matumizi yetu ya umeme hapa Zanzibar kuwa madogo basi tungeweza kuuza hata nchi jirani ikiwemo jirani zetu Tanzania Bara, kitu ambacho kingesaidia hata kuongeza mapato ya Zanzibar. Kwani kuna nchi kubwa duniani kama Urusi sehemu kubwa ya uchumi wake unategemea usafirishaji wa gesi, basi hata hapa Zanzibar inaweza kuwa ni mingoni mwa muuzaji mkubwa wa gesi katika nchi za Afrika Mashariki na duniani kwa jumla.

Mhe. Spika, usafirishaji. Tunaipongeza sana serikali kwa kuendeleza programu ya ujenzi wa barabara Unguja na Pemba, lakini tunaona ile kasi iliyokuwepo mwanzoni hivi sasa imepungua sijui tatizo nini, kwani barabara zinachangia sana kuimarisha uwekezaji na kuinua uchumi wa nchi. Kwa upande wa viwanja vya ndege tunapongeza sana jitihada zinazoendelea za ujenzi wa *Terminal Building* tunaamini baada ya kukamilika kwa mradi ule ndege nyingi zitakuja na wageni wengi watakuja na kupita kama *transit* na mapato ya *landing charge* yataongezeka.

Mhe Spika, tunapongeza jitihada zinazochukuliwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, mpendwa wetu Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi binafsi anazozichukua kutafuta wafadhili na wabia kwa ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri, kwani kuna taarifa nzuri kutoka kwake naamini atakuja kutueleza wakati wa hotuba yake ya kuahirisha Baraza hili la bajet. Kwa hivyo, tunaamini biashara na uekekezaji hapa kwetu itaongezeka mara mbili zaidi na Zanzibar itarejea na ile hadhi yake ya kuwa ni kituo kikubwa cha biahara kwa nchi za Afrika Mashariki. Tunamtakia kila la kheri na mafanikio kwa jitihada zake kwa mafanikio ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, suala la biashara. Katika kuinua uchumi wa Zanzibar na kutokana na mazingira yetu ya kijografia kuwa ni visiwa, basi katika mfumo wa mashirikiano ya kikanda hasa kupitia katika Shirikisho la Jumuia ya Afrika ya Mashariki basi ni lazima Zanzibar itangazwe kuwa ni (*Special Economic Zone)* ili kuwavutia wawekezaji kuja kuekeza hasa viwanda ili na sisi kuweza kuuza katika soko kubwa la Jumuia ya Afrika Mashariki, kama alivyosema waziri kwenye kitabu chake kwamba utafiti uliofanywa na serikali kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Shirika la Fedha la Kimataifa kwamba Zanzibar inamazingira mazuri zaidi ya kibiashara, basi serikali iharakishe kukamilisha

vigezo vya kisheria ili kurahisisha kuondoa urasimu kwa wawekezaji ili waweze kuja kuekeza hyapa Zanzibar.

Sekta ya Afya. Mhe. Spika pamoja ya kuwa Zanzibar tumepiga hatua katika kuwafikishia karibu wananchi huduma za afya, kwani mtu hatembei zaidi ya kilomita tano bila ya kukuta kituo cha afya, lakini bado serikali yetu ina changamoto kubwa katika upatikanaji wa madaktari na wauguzi, upungufu wa madawa hospitalini haya yanahitaji pesa, lakini kuna baadhi ya uzembe wa makusudi ambao hufanywa na baadhi ya wauguzi na madaktari kuwasumbua wananchi. Kwa mfano, wakati mwengine wagonjwa hukaa foleni zaidi ya saa nzima kumsubiri daktari hajafika kazini, pia baadhi ya wauguzi huwatolea lugha chafu wagonjwa hasa kwenye Wodi ya Wazazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo malalamiko mengi tunayapata. Hapa Mhe. Spika, inashangaza sana kwani wengi wa wauguzi hao ni wanawake wenzao ambapo mambo haya hayahitaji pesa za kigeni bali ni uwajibikaji na uzalendo ambapo kwa hapa kwetu suala la uwajibikaji ndio mtihani kwetu.

Mhe Spika, tunashukuru jitihada zinazochukuliwa na serikali kuendeleza miradi ya upigaji dawa majumbani ili kutokomeza kabisa mradi wa Malaria hapa Zanzibar ambapo kwa sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa na hivi sasa dunia nzima inatusifu kwa kufanikiwa kupiga vita ugonjwa wa malaria. Mhe Spika, tunampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kulitekeleza hili.

Mhe. Spika, Mfuko wa Maafa bado tunaiomba serikali kukamilisha taratibu za kuanzisha mfuko wa maafa kwani hali ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani, ambayo husababisha maafa mengi duniani ikwemo mafuriko, joto kali, baridi kali, upepo na dhoruba kali, matetemeko ya ardhi, maradhi ya miripuko, majanga ya moto na kadhalika. Haya ni baadhi ya maafa yanayoweza kutokea wakati wowote, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe mbali kwa hilo. Kwa hiyo, ni lazima serikali ianzishe mfuko huo ili kuweza kusaidia wananchi wetu wakati wowote yatokeapo maafa, kwani hili jambo halipendezi kwamba leo tunapitisha Bajeti ya Serikali tunashindwa kutenga fungu la kusaidia kupunguza makali ya maafa pale yanapotokezea.

Mhe Spika, **s**uala la mapato ya nchi kwa sasa ni mazuri kwa kiasi chetu, lakini bado jitihada zinahitajika katika kukusanya na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato, lakini iko haja ya kuibua vianzio vipya vya mapato ingawa mapato yetu ya ndani yanaendelea kuimarika. Katika huba ya Mhe. Waziri mwaka 2005/2006 tuliweza kukusanya karibu shilingi 62.4 bilioni na kufikia 149.5 bilioni katika mwaka 2009/2010 ambapo ni sawasawa na 139.6%. Kwa kipindi cha miezi 9 mwaka 2010/2011, karibu shilingi 132.96 bilioni ambayo ni sawasawa na 1009% mapato yamekua kwa asilimia 16.7.

Kwa makadirio ya kipindi kilichopita mapato ya wizara ni madogo ya shilingi 6.88 bilioni. Hii Mhe. Spika, ni pamoja na waziri kusema yanatokana na viwango vidogo vya kutozea ada na sheria zetu kuruhusu baadhi ya taasisi kutoa misamaha lakini pia kuna kodi nyingine zimo ndani ya sheria pia hazikusanywi ambapo baadhi ya taasisi huwa hawataki kulipa hasa kwa miradi ya wahisani, pamoja na waziri kusema mapato yetu yameongezeka.

Mhe Spika, serikali yetu bado haijakuwa makini katika kukusanya baadhi ya mapato yake kwani kuna mapato yamo ndani Katiba ya Jamhuri ya Mungano na kama yangelisimamiwa vizuri basi uwezekano wa kukusanya mara mbili ya hayo yaliyokusanywa yangeliweza kupatikana. Mhe. Spika, serikali yetu ingelipaswa kukusanya na ingeliweza kuongeza mapato yetu ya nchi na yangaliweza kutusaidia kupunguza utegemezi wa misaada ya bajet kutoka nje. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya sura ya saba ya kifungu cha 133 kinasema hivi nanukuu:-

> "Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa AKAUNTI YA FEDHA YA PAMOJA ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano ambayo itaweka fedha yote itakayochangwa na serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na tume ya pamoja ya kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa madhumuni ya matumizi ya shughuli za Jamhuri ya Muungano na mambo ya Muungano".

Fedha ambayo baada ya matumizi yake Mhe. Spika, fedha inayobaki inatakiwa igawanywe kwa serikali mbili ambapo Zanzibar ingelistahiki kupata mgao wake, ambao ungesaidia kuongeza mapato yake. Kwa mfano, mapato yaliyomo katika mambo ya Muungano ni suala la bandari, mapato ya anga, mapato ya mafuta na gesi, mapato yote ya *TRA*, mapato ya uhamiaji, faida ya mapato ya *B.O.T* na kadhalika.

Mhe Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo mapato hayo yanatosheleza kabisa matumizi ya shughuli za Muungano na fedha nyingi sana zinabaki ambazo zingeliweza kusaidia kuongeza mapato yetu ya Zanzibar. Je, Mhe Spika, namuuliza Mhe Waziri hilo linafanyika? Kama halifanyiki je, hatuoni kama linaikosesha serikali yetu mapato halali ambayo yangeliweza kusaidia uchumi wetu na kutupunguzia utegemezi wa bajeti yetu kwa wafadhili? Naamini mapato haya yangeliweza kusaidia sana mapato yetu.

Mhe Spika**,** kama waziri alivyosema katika masuala la Mafuta na Gesi, linashughulikiwa na serikali zetu mbili, lakini kwa kuwa wenzetu upande wa pili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaendelea na jitihada za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia, basi ni vyema na sisi Zanzibar tuanze

kutafuta wahisani kuanza utafutaji wa utafutaji wa mafuta na gesi hadi suala hili litakapopatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, suala hili kama litaendelea kuwa la Muungano basi tutapigiana mahesabu nani amlipe mwenziwe, kwani kila tukichelewa gharama za utafiti zinaongezeka lakini pia kutokana na misukosuko wa kiuchumi duniani nchi zinazotoa mafuta kwa wingi uwezekano wa kupanda bei ya mafuta upo mkubwa sana. Lakini je, nasi tukiwa na mafuta yetu hatutoagiza tena mafuta kutoka nje na mengine tutauza nje. Tutapunguza nakisi ya uagiziaji wa bidhaa na tutaongeza usafirishaji wa bidhaa kwenda nje, lakini pia tutapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji na bei ya bidhaa itapungua na wananchi wetu watapata unafuu wa maisha. Hiyo isitoshe, lakini pia meli za nje zitakuja kupakia mafuta na hata ajira itaongezeka.

Mhe Spika, hali ya chakula nchini kwa sasa sio nzuri sana, kwamba chakula bei imekuwa ni kubwa mno, wananchi wetu wanaumia na bei ya chakula, kwani kila kukicha bei inaongezeka kwani mwaka 2005 bei ya mchele ilikuwa shilingi 450/=, mwaka 2010 ilikuwa shilingi 900/= na hivi sasa 2011 ni 1,200/= **.** Mhe. Spika, kwa kweli hii ni hatari kubwa, hali hii kama hatukuidhibiti basi wananchi wetu wanaweza wakapata tabu, kama hali itaendelea hivyo, ikifika mwaka 2015 bei ya mchele kwa kilo itafika 1,500/=**.** Hapa tunaishauri serikali kupitia Shirika lake la Biashara (*ZSTC*) kuagiza mchele na kuingiza kwenye soko ili kupunguza bei na pia kuhamasisha wakulima kulima mpunga kwa wingi na kuununua na kuuhifadhi maghalani baadae kuuingiza kwenye soko ili kupunguza bei zilizopo.

Kutokana na taarifa ya Benki ya Dunia kwamba kuna mategemeo makubwa ya kuongezeka kwa mfumko wa bei kwa aslimia **2** na matarajio ya kuongezeka kwa bei ya mafuta duniani upo mkubwa sana. Hii itapelekea kuongezeka kwa bei ya chakula duniani, wakati mwezi Oktoba mwaka 2010 pipa moja la mafuta lilikuwa ni dola 79 kwa pipa lakini hadi itakapofika mwaka 2012 linatarajiwa kufikia dola 100. Ndio maana tukaitaka serikali kuanza mara moja kushughulikia suala la uchimbaji wa mafuta na gesi kwani yakiongezeka bei wakati tukiwa nayo na sisi tutaongeza mapato ya nchi.

Mhe Spika, tunapongeza sana jitihada zinazooneshwa na Mhe. Waziri wa Fedha kwa umakini na umahiri wake wa kuona mbali na kuongeza mapato ya Serikali kwa kupunguza misamaha isiyokuwa ya lazima ya kodi kutoka bilioni 21 hadi bilioni 14. Huu ni ujasiri mkubwa sana pia tunaipongeza sana Serikali kwa kujitahidi kuzuia mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali, hii itasaidia kuongeza mapato yetu. Pamoja na jitihada hizo tunaishauri Serikali ili kuzuia kabisa uvujaji wa mapato basi ni vyema kuachana na utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa fedha taslim na baadae kuanzisha utaratibu wa malipo ya fedha kupitia benki. Hii ndio njia pekee itakayoweza kuzuia uvujaji huo.

Mhe. Spika, serikali yetu inakosa mapato mengi kupitia kodi ya ardhi ambapo kuna baadhi ya watu pamoja na wawekezaji wamehodhi ardhi kubwa sana hasa katika maeneo ya uwekezaji bila ya kuyaendeleza na wengine wameyazungushia ukuta kwa miaka mingi wakati wengine wanaotaka kuekeza wanakosa nafasi hiyo. Kwa hiyo, serikali ifanye tathmini ya maeneo hayo ya ardhi na aliyeshindwa kuyaendeleza basi ni vyema ikarejeshwa serikalini na kupewa watu wengine ambao wana uwezo wa kuendeleza.

Mhe Spika, pia suala la zao la karafuu serikali iko haja ya kurejesha upandaji wa mikarafuu na kusimamia wakulima kwani kuna baadhi ya wakulima wameanza kulalamika kati ya mikarafuu kumi waliyopanda basi si zaidi ya mitatu tu ndio inayopona. Hapa ndipo kwenye uchumi wa nchi yetu kwa hiyo ni vyema serikali ikaliangalia kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, katika suala la kupanda kwa bei ya vyakula vikuu hapa Zanzibar. Tunaishukuru serikali kuwa haikuongeza kodi yoyote kwa wafanyabiashara lakini imeshusha kodi ya vyakula vinavyoingizwa nchini. Lakini pamoja na jitihada hizo za serikali ili kuwapunguzia makali ya maisha wananchi, lakini bado bei ya vyakula ipo juu. Tunaiomba serikali ingeliwafuatilia wafanyabiashara na wao wakapunguza bei ya vyakula, vyenginevyo nia ya serikali ya kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wetu haitofanikiwa lakini itawaneemesha zaidi wafanyabiashara wachache tu.

Mhe Spika, Serikali imesema kwa mwaka ujao inatarajia kukusanya shs 631.08 bilioni kutoka shs 444.64 sawa na asilimia 38 ambapo ni ziada ya shs 186.44 bilioni ukilinganisha na makusanyo ya mwaka uliopita. Hii inaonesha kuimarika kwa mapato ya ndani na nje ambapo mchango wa washirika wa maendeleo ni 340.96 bilioni sawa na asilimia 90 na SMZ ni 37.95 sawa na asilimia 10. Kwa hesabu za haraka haraka utaona bajeti yetu ni tegemezi sana wakati kumbe karibu ya asilimia 70 ya pesa ni zetu wenyewe, kwani kati ya hizo pesa za wahisani ni 378.90 bilioni ambapo kati ya hizo ni 124.95 bilioni tu ndio ruzuku lakini 216 bilioni ni mikopo ambapo Serikali italipa hapo baadae.

Kwa hiyo, ukijumlisha mchango wa Serikali wa 37.95 + 216 bilioni Serikali itakuwa imechangia karibu 254 bilioni. Hili Mhe Spika, sio aibu hata kidogo kwani Serikali kukopa kwa ajili ya kuekeza kwenye miradi ya maendeleo na kuimarisha huduma za jamii, pia huu ni utaratibu wa kawaida duniani kwani hata mataifa makubwa mfano Marekani na Japan nao pia wanakopa kwenye vyombo vya fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao. Sio hayo tu lakini pia mapato ya ndani yanakadiriwa kukua hadi kufikia 221.24 bilioni.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tunaiomba serikali rasimu ya bajeti ya mwaka ujao Mhe. Waziri atuletee mapema kwenye kikao cha Januari au Machi ili tupate kutia maoni yetu mapema ili iwe ni bajeti ya wananchi kweli kweli kwani kuna baadhi ya mambo yanapokosekana kupangiwa matumizi inakuwa ni mzigo mkubwa hapo baadae. Mhe. Spika, baada ya hayo, mimi pamoja na wajumbe wangu wa kamati na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunampongeza sana Mhe. Waziri na tunaipongeza hotuba hii ya bajeti kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti. Kuna mambo mawili nataka niyaseme ili tupate kwenda vizuri. Waheshimiwa Wajumbe kuna karatasi imesambazwa inaonesha ni ukurasa wa 74. Hiyo karatasi inafanya marekebisho katika ukurasa wa 74 wa kitabu cha Mhe. Waziri. Hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe usahihi umo kwenye karatasi hii iliyosambazwa na kwa wale ambao wanataka kufanya rejea yale mahesabu yaliyozungumzwa mle basi rejea yao iende kwenye karatasi hii na sio ile iliyoko kwenye kitabu kwa sababu ndio iliyorekebishwa. Hilo la kwanza.

La pili Waheshimiwa Wajumbe katika kuchangia tujitahidi kuokoa muda. Mhe. Mwenyekiti ametumia muda wa karibu dakika 50. Kanuni inanambia nimpe dakika 30 kama naona inafaa nimuongezee 10 nikafanya hivyo, lakini zaidi amechukua dakika 10 nyengine. Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe tujitahidi kwenda kwa mujibu wa kanuni kuchangia si zaidi ya muda wa dakika 30 ambao kwa kweli kwa hapa ni muda mkubwa sana.

Bungeni pale wale waliokuwa wabunge wanajua kwamba kuna dakika 15 tu sasa hapa dakika 30. Kwa hiyo, tupange pointi zetu vizuri ili tuhakikishe kwamba tunaokoa muda na kupata wajumbe wengi zaidi kuchangia bajeti hii ya serikali. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya mwanzo kwa asubuhi ya leo baada ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Wenyeviti.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake safi na nzuri ambayo imetupa moyo katika suala zima la kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu nitamke kwamba mimi mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Dole tunaipongeza hotuba hii na tunaikubali kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nina sababu ya kuipongeza na kuikubali hotuba hii. Katika hotuba hii kuna mambo mengi yamejitokeza ambayo yanasaidia sana katika uchumi wa nchi yetu. Moja, ni suala zima la mgawanyo wa mapato kati ya mapato yatakayotumika kwenye matumizi ya kawaida na mapato yatakayotumika katika matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, ukiangalia katika bajeti zetu za nyuma kwa bahati mbaya sijapata zile bajeti nyengine. Lakini ukiangalia kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011 ilikuwa mapato jumla ni milioni mia tatu mia mbili na arubaini na moja. Mapato hayo yaligawika kwa kazi za maendeleo ni milioni moja na mia tano na kazi za kawaida ni milioni moja mia saba na arubaini na moja.

Mhe. Spika, lakini ukija ukiangalia bajeti ya safari hii kwa kweli katika mapato yetu yamegawika vizuri sana, imelenga sana katika shughuli za maendeleo. Hili ni suala zuri kabisa kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, maendeleo ndio yanayompunguzia umasikini mwananchi, maendeleo yatakwenda katika huduma ya maji, kwa hivyo maji yakipatikana tayari mwananchi umempunguzia umaskini. Maendeleo yatakwenda katika utengenezaji wa barabara, ukenda kupeleka katika sehemu ya barabara tayari mwananchi wetu umempunguzia umaskini. Maendeleo yatakwenda katika mambo ya kilimo na mambo mengine ambayo tunahisi ya maendeleo. Moja kwa moja hapa Mhe. Spika, tayari mwananchi wetu umempunguzia umaskini.

Kwa maana hiyo, mwaka huu shughuli za maendeleo zimetengewa shilingi bilioni 378.90, shughuli za kawaida bilioni 234.18. Kwa hivyo, kwa kweli tunahisi tunapiga hatua na tunaomba sana Mhe. Waziri hii kasi aliyoianza isiwe ni mwisho hapa tukaenda halafu baadae tukarudi nyuma. Tunaomba tuendelee kwa hili kwa sababu wananchi wetu wako katika hali ya umasikini.

La pili Mhe. Spika, sababu hasa mimi ya kuipongeza bajeti hii ni katika suala zima la vipaumbele vya serikali iliyojiwekea. Suala la vipaumbele Mhe. Spika, ni zuri kwa sababu limeangalia katika zile nyanja hasa zinazowagusa wananchi wetu na hasa katika suala la kuwaondoshea umasikini. Ukisema suala la afya Mhe. Spika, ni muhimu sana, maeneo yote binadamu unaweza usiyaguse. Kwa mfano ukiacha maji, lakini mambo ya elimu, kilimo na masuala mengine, suala la afya ni muhimu sana.

Kwa hivyo, mimi napongeza sana kwa kuwa hichi ni kipaumbele cha mwanzo katika mpango wetu huu wa bajeti ya safari hii kuona kwamba Wizara ya Afya ndio ya mwanzo katika suala zima la kulipatia maendeleo au fedha za kutosha kuweza kutekeleza matatizo yake.

Lakini Mhe. Spika, katika suala la afya hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro kuna mapungufu kidogo. Nimesoma humu katika bajeti mambo ya kipaumbele tele yametiwa katika Wizara ya Afya lakini suala la vifo vya mama na mtoto hamna. Japo ukiangalia katika kitabu cha mwelekeo wa hali ya uchumi mpango wa maendeleo wa mwaka 2011/2012 utakuta kule katika MKUZA lakini ndani ya bajeti yenyewe hamna suala hili. Kwa hivyo, suala la afya kupunguza vifo vya mama na mtoto ni sehemu kubwa bado linatutatiza kinamama, watoto wanafariki, kinamama wanafariki. Mhe. Spika, naomba na hili nalo lichukuliwe kipaumbele kama lilivyo kuweza kutiliwa fedha wakaweza kukidhi shughuli zao.

Mhe. Spika, pia nimevutiwa na vipaumbele hivi katika suala la elimu. Mhe. Mwenyekiti, suala la elimu kwa kweli tunaona jitihada zipo japo mapungufu yapo lakini serikali inajitahidi. Hata mimi nimefaidika katika jimbo langu nashukuru nimepatiwa skuli ya sekondari. Kwa hivyo, nashukuru sana kwa hili naamini nia hii ya kuipatia sekondari haitoishia hapo tutasaidiwa pia kupatiwa na wale walimu wanaokwenda sambamba na sekondari ile.

Mhe. Spika, katika suala zima la vipaumbele pia kuna suala la maji. Kwa kweli hili Mhe. Spika, watu wanasema halitaki tochi, tatizo la maji bado lipo na wao wenyewe wamekiri hili jambo. Tunachoomba kwamba wajitahidi sana kwa kweli haya matatizo mbali yaliyotajwa yale ya kuwa visima vinachimbwa lakini mitandao ya maji yale mabomba na mambo mengine yanakuwa tatizo. Lakini mimi naomba pia jambo jengine serikali iliangalie isiwaachie wizara peke yake, serikali iliangalie katika suala zima la kuwa na visima vingi. Ukiacha mitandao ile ya mabomba kuharibika lakini suala jengine ni pampu kuharibika mara kwa mara linalosababishwa na uingiaji na utokaji wa umeme.

Mhe. Spika, hili tunaambiwa kwamba kuna chombo maalum wenyewe wanaita *stabilizer* ya kuweza kudhibiti ule umeme unapoingia na kutoka ili usiweze kuathiri kile chombo. Kwa hivyo, tungeomba wizara kupitia serikali kuu wasaidiwe kupatikana hivi vyombo vyenginevyo Mhe. Spika, mwezi mmoja unaweza ukatia pampu hata tatu.

Mhe. Spika, katika jimbo langu pia mfano huo upo, tumepewa pampu baada ya siku tatu pampu ile imeungua tena. Kwa hivyo, mimi ningeomba hii hasara na shida wanazozipata wananchi wetu, lakini serikali pamoja na kuipa kipaumbele pia waangalie na yale masuala ya kina na mazito zaidi. Mengine yanayohusu maji nitakuja kuzungumza wakati wa wizara yenyewe itakapofika.

Mhe. Spika, kipaumbele chengine ambacho mimi kimenikosha ndani ya moyo wangu ni suala la kilimo kwa kuwa serikali sasa hivi itajikita katika kusaidia wakulima. Kwa kweli kwa muda mrefu kulikuwa kuna mpango wa maelezo na

hapo hapo kwa kuwa tumepewa maelezo lakini dalili za vitendo zimeshaanza kuonesha. Kuna mbegu sijui za nerika, sijui kuna matrekta yameshaanza kuja, *power tiller* na vitu vyengine.

Mhe. Spika, tungeomba sana huu mgao wa hivi vifaa utakapofika basi uende vizuri na nia ile iweze kukamilika na bajeti itakayokuja mwakani tutataka kujua hatua gani ambayo tumefika kwa hii ahadi tuliyopewa ya kuinua kilimo kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, ningeomba tu kuwa serikali ishirikiane sana na hawa watu wa Shirika la Umeme katika kusukuma suala zima la miundo mbinu katika maeneo yetu hasa suala la umeme na mimi limenigusa katika jimbo langu katika bonde la Bumbwisudi. Kwa hivyo, ningeomba sana wale wanaohusika suala hili livaliwe njuga kwa sababu kule watu wana hamu, watu wanategemea, watu sasa hivi wanahisi kama wameokolewa kiasi gani katika maisha yao baada ya kupelekewa miundo mbinu hii ya maji katika umwagiliaji wa mpunga.

Mhe. Spika, la tatu katika lililonifurahisha na kuona kwamba hii kweli ni bajeti ya wananchi wote imewagusa ni suala la kuwapandisha mishahara watu wetu. Kweli sasa hivi katika nchi yetu hali imekuwa ngumu kimaisha kila siku vitu vinapanda. Haki ya Mungu Mhe. Spika, sasa hivi wewe ukatie mafuta sheli ukizunguka ukirudi mafuta yameshapanda asilimia 5 mpaka 6. Kwa kweli hili ni tatizo na mimi nadhani serikali ifike pahala haya masuala ya mafuta basi watafute mbinu ya kuona yanafikia pahala yanadhibitiwa bei ziwe za aina moja.

Halafu Mhe. Spika, kuna mtindo mbaya kabisa unaofanyika. Hawa wenye kumiliki mafuta wanapotaka kupandisha bei kwanza wanayaficha, watu wateseke wahangaike wakatiliwe mafuta mabovu wakanunue vichochoroni huko magari yaharibike, halafu baadae hapo tena ukifumba na kufumbua bei imepanda. Ikishapanda bei sasa hapo nisikilizie Mhe. Spika, vyakula vinapanda, huduma nyengine zote zinapanda, wanaojaaliwa kujenga wakigusa mchanga haushikiki, wakigusa mawe hayakamatiki. Sisi tusiokwisha kujenga maskuli na vituo vya afya kila siku matatizo.

Kwa hivyo, mimi nadhani hili suala serikali nalo ilitazame kwa kina. Hili suala kweli ni tatizo la huko tu wanakotoa hao wenzetu au kuna jambo jengine zaidi hapo linafanywa. Mhe. Spika, mimi napongeza sana kwa haya masuala kwa sababu wenzetu wanaofanya kazi kwa kweli wana maisha magumu, matatizo, pesa wanazozipata hazikimu, mtu ana watoto, watoto mara homa, matatizo mengi tu skuli wanatakiwa ada, mambo mengi.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba katika suala zima hili la mishahara basi mjitahidi kadri ya uwezo wenu itakapokuja bajeti nyengine au kama tulivyoambiwa hapa waziri yule anayehusiana na mambo ya utumishi atakuja kutwambia ni kiasi gani ambacho wametiliwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, isipokuwa nina ombi maalum naliombea vikosi vya SMZ kwa kweli hali nayo pia iko chini mno ya fedha wanazopatiwa. Serikali mtaangalia wenyewe vikosi vya ulinzi katika nchi yetu usalama, amani, utulivu tunategemea vikosi vyetu. Kwa hivyo, tuangalie sana tuwasaidie tuone wanaweza kuishi kwa raha na kumudu maisha yao ili ule ulinzi watufanyie wa uhakika.

Mhe. Spika, katika suala la kilimo pamoja na hii hali ambayo imejionesha kwenye bajeti ya kupatiwa matrekta, pembejeo pamoja na mbegu lakini mimi ningeomba sana wakulima tuwatafutie utaratibu maalum. Kwa wenzetu Tanzania Bara sijui inatoa benki gani lakini naona zimeanza kuanzishwa hizi benki za wakulima na wao hapa nchini kwetu ziweze kuja waweze kutusaidia wakulima. Wapo wakulima wengi wanataka kujiendeleza hasa katika suala la mboga mboga.

Hivi sasa Mhe. Spika, kuna watu wanajitahidi sana kulima mboga mboga ili kupunguza huu utaratibu wa kuagiza makabeji, tungule, karoti na vitu vyengine Tanzania Bara. Hapa vitu vyote hivyo vinaota, kama unakwenda Mfenesini meli nane unapandisha kilima mkono wa kushoto pale walikuwa wanalima makabeji yanatoka mazuri kweli kweli, lakini wanachokosa utaalam wakati mwengine na jinsi ya kujiendeleza.

Kwa sababu kama unalima kabeji inahitaji utaratibu wake, iwekwe dawa, sijui utie mbolea kiasi gani, pamoja na wataalam wenyewe wa kilimo nao wamekuwa wanasomeshwa wengi lakini hawaonekani. Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili tutakuja kuambizana kwa hili. Lakini Mhe. Spika, wasaidiwe nao hawa wenzetu wa kilimo katika suala zima la kuweza kujikwamua kimaisha na kupunguza umaskini wa kipato.

Mhe. Spika, katika bajeti yetu pia kuna mapungufu kama nilivyosema hasa katika suala la maendeleo yetu. Pamoja na kuwa tumeelekezwa washiriki wetu hawa wa maendeleo wanapotusaidia si kama ile dhana yetu ambayo tuliyokuwa nayo sisi kwa kuwa ni ruzuku peke yake tunayoitegemea, inaonekana pia hii misaada huwa inatusaidia zaidi. Kwa hivyo, ningeomba kwamba hii misaada tunayoipata tuitumie vizuri lakini na hizi ruzuku pia tunazozipata tuzitumie vizuri. Lakini hata hivyo Mhe. Spika, bado kuna haja tujitahidi kupunguza kutegemea hawa washiriki wa maendeleo.

Mhe. Spika, sasa hivi dunia inabadilika mambo mengi, atakayekusaidia anakusaidia kwake ana faraja nzuri, kesho au kesho kutwa hali imekuwa mbaya kwa upande wake hakupi wewe atajihangaikia mwenyewe kwanza nafsi yake. Tunasikia hali huko mara vita, mara kumeripuka hichi, mara hawamtaki huyu.

Mhe. Spika, mimi ningeliomba sana kwamba tujitahidi japokuwa bajeti yetu imepunguza kidogo utegemezi kutoka asilimia 26 imekwenda kwenye 24. Tunapongeza kwa hilo tunajipunguzia kidogo kidogo utegemezi lakini kuna haja bado katika shughuli zetu za maendeleo tujitegemee sana na hasa katika masuala pia yanayohusu Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, nitaitaja sana Wizara ya Afya kwa sababu mimi ni mdau wa kudumu kule. Kwa hivyo, tusaidiane na hili tusitegemee wafadhili watusaidie mara dawa, mara vifaa, wakija wakisema hoo, nimekwama hapo sasa tutaanza kutafutana. Kwa hivyo, kama hujajiandaa vizuri huenda hali ikawa ngumu, tunaomba sana jamani tujitahidi katika masuala haya.

Mhe. Spika, kujitahidi kwetu ni katika suala zima la utaratibu wa ukusanyaji wa mapato yetu ya ndani. Mhe. Spika, ukusanyaji wetu bado sio mzuri, mapato bado yanavuja vuja huko kwa nguvu, watu wanapenda kujaza mifukoni zaidi kuliko kujali uzalendo. Haipendezi Mhe. Spika, tujitahidi kadri tunavyoweza kuangalia taasisi zetu hizi zinazotuchangia mashirika yetu na vitengo vyetu mbali mbali kudhibiti.

Mhe. Spika, hata katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na wafanyabiashara nayo si mazuri kwa sababu wafanyabiashara wanapenda sana kukwepa katika masuala mazima haya ya kulipa kodi. Kila akiipata nafuu pamoja na kwamba utasikia tuwasaidie wafanyabiashara, bidhaa wakileta tuwapunguzie ushuru, lakini wao ukikaa ukifumba ukifumbua utawakuta katika hali ile ile ndio kwanza wanapandisha bei. Wakipandisha bei hizo basi, mwambie akakupe risiti ya chochote kile anachokuuzia hakupi.

Kwa hivyo, utaratibu huu wa wenzetu hawa wanaokwepa kodi za biashara hasa wakati wa kuleta bidhaa zao bandarini ujanja upo unafanyika pale taarifa tunazipata. Lakini siwezi kusema lini na jambo gani limetokea kwa sababu ni taarifa tu sina uthibitisho nisije nikashikwa kwa hapo. Haya masuala yapo na ni vizuri serikali ikipata taarifa ichukue na ilifanyie kazi. Haiwezekani watu wakatoa taarifa za ovyo ovyo inategemea wakati mwengine, lakini kitu kama hichi cha maslahi ya wananchi wetu basi kiangaliwe vizuri.

Mhe. Spika, jengine katika suala zima la kukusanya mapato yetu ya ndani ni katika suala zima la mahoteli yetu na watalii wanaokuja. Mhe. Spika, utaratibu uliopo sasa hivi sio mzuri, sasa hivi mtalii analipa kila kitu huko, analipia

chumba, analipia gari, analipia mpaka maji yale ya kunywa, chakula vyote analipa kwao. Pia akifika hapa yule mtalii basi mwenye hoteli ameshakodi gari wewe ukawachukue wale watalii upeleke. Nisikilizie Mhe. Spika, kasheshe inayotokea hapo na sisi utalii huu tumeutaka hapa ili wanufaike wananchi wetu, vijana wetu wapate ajira lakini na wafanya biashara wetu nao waweze kupata mapato kuweza kujikomoa kiumaskini. Lakini kinachotokea hapo mwenye gari atakwenda kuwachukua watalii wale awapeleke hoteli, malipo miezi mitatu au minne hajapewa. Mfanyabiashara atapeleka kama samaki, nyama au bidhaa yoyote ile zikiwemo mayai, kuku na vitu vyengine, matokeo yake mtu anasafa miezi mitatu, minne mpaka mitano halipwi. Niulize kwa nini Mhe. Spika.

Kwa sababu unaambiwa fedha hazijaletwa kutoka huko walikolipia. Sasa utalii huu mimi nashangaa Mhe. Spika, kweli wanatusaidia kwa hakika. Kwa hivyo, tunaomba wajitahidi sana wenzetu katika suala hili, wazingatie wana ili kuona mapato yetu ya ndani tunayadhibiti kutokana na ule utaratibu tuliokubaliana, sio kila mmoja awe anafanya vyake anavyovitaka yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti hapa alichangia mambo mengi mno. Kwa hivyo, ninachoomba mimi Mhe. Spika, ni kuwa yale ambayo tumekubaliana katika bajeti yetu hii basi tujitahidi kadiri ya uwezo wetu tuweze kufanikiwa.

Samahani Mhe. Spika, kuna jambo moja nimelisahau kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, humu wamezungumza gharama za elimu mpaka kufikia elimu ya juu. Lakini Mhe. Spika, pamoja na idadi iliyoelezwa katika kitabu hiki inayohusiana na masuala ya wangapi wamepata kufaidika, lakini bado ni tatizo watusaidie wenzetu. Huko majimboni ni tabu kweli kweli, mtu anakuja na gia ya mwanzo, anasema ili pale nianze tu kuingia halafu mambo mengine yatafuata na mfuko ndio unasubiriwa subiriwa basi upatiwe laki nne, laki tano au milioni moja na zaidi ndio gia ya mwanzo hiyo.

Mhe. Spika, mimi nikihesabu kwa haraka haraka nina vijana kama saba hivi ambao hawajapata mfuko huo, najitahidi kuwaandikia vimemo nendeni huko kunakohusika, lakini bado hali ni ngumu. Kwa hivyo, huu mfuko wa elimu ya juu kweli kama unatakiwa usaidie vijana wetu basi suala hili tusaidiwe sana na huo mfuko utunishwe, vijana wetu wengi sasa hivi wanahitaji elimu na sisi wajumbe kila kitu Mhe. Spika, wewe unajua hali iliopo huko majimboni, kuwa kila kitu ni sisi wajumbe. Kwa hivyo, na hili la elimu madhali mfuko upo basi watusaidie.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa na hayo tu ndio nikaona sio vizuri bajeti hii ipite tu bila kuichangia japo kidogo na mimi kuna mambo yamenigusa gusa na nipo hapa kwa ajili ya wananchi wangu wa Jimbo la Dole.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa bajeti yake hii, nampongeza tena kwa bajeti nzuri, ambayo inamuelekeo, imeleta imani kwa wananchi wetu. Kwa sababu Mhe. Spika, nchi hii ni nchi ya wakulima na wafanyakazi na kwenye bajeti imewagusa wakulima na imewagusa wafanyakazi. Kwa hivyo, tunaamini kwa kuwa bajeti hii ikitekelezeka vizuri yale mapinduzi ya masuala ya maisha yetu yawe ya kupunguza umaskini katika nchi yetu, nadhani yatafikia hatua nzuri. Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa nafasi hii uliyonipa na wewe nakutakia kila la kheri kutokana na maelezo niliyokuambia mwanzo kuwa tutakuwa tuna shughuli nyengine. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo, nawatakia wote kheri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana*(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Bismillah Rahman Rahim. Mhe. Spika, hii ni moja katika ishara ya kupiga makofi kuwa hii bajeti ni nzuri ndio maana yake. Mhe. Spika, ingekuwa bajeti sio nzuri basi wasingepiga makofi wajumbe.

Kwanza mimi nikusifu wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwa umahiri wako mzuri wa kutuongoza na kutukosoa kwa kuweza kuhimili kiti chako hapo kwa muda mrefu kuweza kukaa tofauti na wajumbe wengine katika *backbencher* huko, mara wanatoka mara wamekaa, lakini wewe unastahamili mpaka dakika ya mwisho. Kwa hilo nakupa pongezi kubwa sana Mhe. Spika, kwa afya yako ilivyokuwa madhubuti. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimshukuru sana au nimsifu sana Mhe. Waziri shemeji kwa bajeti yake nzuri sana. Mhe. Spika, ukweli niuseme, tangu nianze Baraza hili sijaona bajeti iliyokuwa haina tegemezi kwa asilimia kubwa kwa wafadhili kuliko hii. *(Makofi).*

Mhe. Rais wetu hakutia mkono kizani, amemchagua kijana kwa kumuamini na ndio maana imefika pahala leo tunafuraha nayo bajeti yake hii aliyoitoa juzi, japo alikuwa akikohoa kwa hapa na pale ndio usomaji ulivyo, lakini namshukuru sana kwa bajeti nzuri sana.

Mhe. Spika, nisiendelee kumsifu sana hatimaye akaja akaharibu, lakini Mwenyezi Mungu atakubariki, atakupa kila lenye kheri na wewe na haya yaliyokuwemo humu uweze kuyatekeleza kwa ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nina mambo mengi sana katika bajeti yake Mhe. Waziri na yamenipa taaluma nzuri sana, pamoja na muda mfupi tu tuliopewa wa kuchangia, lakini nimeridhika nao ndio nikaona huo huo muda mfupi na mimi nitatoa maoni yangu au ushauri wangu, kama ndani yake kutakuwepo na swali basi litatokea humo humo katika kuchangia.

Mhe. Spika, wananchi wetu kwenye majimbo wengi hawafahamu nini maana ya ukuaji wa uchumi. Wanasikia tu uchumi umekuwa kwa asilimia Fulani, uchumi umekua lakini hawajui. Labda wengine wana hisia kuwa kukuwa kwa uchumi waziri kupata gari mpya, labda wanaona hivyo wengine, lakini si hivyo.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri kwamba bajeti inayokuja aanzie kwa wananchi, bajeti yake akaitengeneze kwa wananchi walafu ndio uje juu. Kwa sababu mimi nitajua asilimia ya kukua kwa uchumi, nitaelewa ni jinsi gani ambavyo unafanya kwa ukuaji wa uchumi. Lakini mwananchi kwenye jimbo hafahamu hilo. Namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi bajeti inayokuja akayaanzie kule chini kwa wananchi wa jimboni, ili bajeti yake mara nyengine itakapokuja iwe nzuri zaidi kuliko ya leo hii.

Mhe. Spika, katika ukuaji huo wa uchumi, kuna mambo mengine Mhe. Waziri amejitahidi sana kuyabana na ndio maana leo anakwenda kifua mbele. Lakini pamoja na kuyabana na sisi ni lazima tumshauri Mhe. Waziri na tumuoneshe njia nzuri ya ukuaji wetu kuweza kuendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti wangu hapa Saitoti ameeleza ni moja katika njia nzuri kabisa. Mhe. Waziri hii uikubali kwa makusudi tu, sasa hivi walipaji kodi wageuke bwana, sio waende wakalipe pale kwenye wizara yenyewe, waende wakalipe banki moja kwa moja. Mhe. Spika, hili litatusaidia kwa dhana ambayo tunasema labda wanakula pesa na litatusaidia kuonesha jinsi gani, hata yule mtu ambaye analipa kodi yake akaiona inavyozunguka. Sasa hili Mhe. Spika, naomba ulione kwa makusudi kuwa walipa kodi waende kulipa kule benki ili kuondoa miaya hiyo tunayoisema kila siku watu wanakula, pengine hawali lakini isipokuwa ndio unajua tena Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kweli ningemuomba Mhe. Waziri katika utekelezaji wake kwenye hayo maeneo ambayo, kwa mfano tuna afya, kilimo na tuna maji katika wizara hii husika. Mhe. Spika, katika miradi hii, mimi nafikiri tungekuwa tuna *special plan*. Kwa mfano bajeti hii tungechagua moja tu.

Nakumbuka wakati ule Marehem Abeid Aman Karume, alisema tutakunywa uji wa mapande, lakini lengo lake alikuwa anataka kujenga majumba na kweli, leo tizameni yale majumba ya Michenzani tumenufaika sote. Kwa hivyo, na sisi tungeamua kwa makusudi, Mhe. Waziri ungesema mimi sasa naelekeza kwenye kilimo, huna masihara nako kabisa. Lakini tunasema tu kilimo tutakinyanyua, maji, sijui umeme. Sio kweli Mhe. Waziri miradi yote hiyo, huna fedha hizo tusijidanganye. Fedha hizo Mhe. Waziri huna.

Sasa kwa kukusaidia tu tujaribu katika kupanga *special plan* ya kuchagua eneo moja la kuweza kulisaidia, nafikiria tukifanya hivyo Mhe. Waziri *Wallah* hupati tabu mwakani kabisa, tutakwenda vizuri tu. Lakini ukisema uyachukuwe haya mambo yote tutajidanganya.

Sasa mimi Mhe. Spika, niingie kwenye suala la kilimo. Mhe. Spika, kilimo kwa kweli hatujataka kukisaidia, hili tuseme kweli. Mimi nitakupa mfano, katika ukurasa huu wa 23, sehemu ya Jimbo la Kitope kuna maeneo makubwa sana ya ulimaji, lakini utakuta ardhi ile kuna sehemu nyengine hazilimwi, kwa sababu gani hazilimwi. Wakati wa kupata vile vianzio vya kufanyia ukulima basi wanakosa, wanaona aah! Sasa hii tena haina maana.

Kwa hivyo, mheshimiwa hebu tulitizame hili kilimo sio kitu cha masihara, kilimo kitaondoa matatizo yote tunayopiga kelele, kupanda kwa bei au mfumuko wa vyakula, sijui mishahara. Mhe. Spika, suala hili tukiliweza basi hakuna haja hiyo ya kupiga mtu kelele. Tutampa kazi Mhe. Mansour bure, tutakuja kumsema hapa na tumpige mabuti bure, kumbe hatujampa nyenzo. Mhe. Spika, tumpe nyenzo kijana huyu, mahiri sana na yuko *strong* kabisa katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, nakuhakikishia bajeti yake itakapokuja utaona vitu gani anavyovifanya, hivi sasa hivi bado tunatizama zile rasha rasha za mvua, kama alivyosema Mhe. Bukheti hapa tayari tunaanza kunyeeshewa nyeeshewa, ameshaona sehemu nyengine umwagiliaji kule umeshaanza kufanya kazi. Sasa je, ukimmalizia yote, fungu lakini la pesa. Sasa Mhe. Spika, tuangalie vizuri, sio lazima tukanunuwe matrekta yenye bei kubwa. Kuna hivi vitrekta vidogo vya kisasa, kila siku mimi huangalia Bara kule, vitoroli sijui vinaitwaje vitrekta vile.

Mhe. Fulani: Vibajaji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Vidogo, sio Bajaji bwana. Vidogo vile vya kuchimbulia. Vile bei yake ni kama shilingi milioni tano tu.

Mhe. Spika: *Power teller*.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *Power teller*. Zile *power teller* Mhe. Spika, kama tutasema kuwa tuwanunulie wananchi wetu au tuwakopeshe wananchi wetu, basi wanaweza wakamiliki na wanaweza wakakurudishia mkopo kwa wakati. Sasa tuangalie na maeneo hayo ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nije kwenye maeneo ya umeme na maji. Kwa kweli tutamlaumu bure Mhe. Ali Juma Shamuhuna na tutampigia buti ya bure tu, lakini hamuujui undani wake ukoje. Mhe. Shamuhuna juzi kaondoka hapa na karudi katuambiaje, atatuchimbia visima 68 kama sikosei, lakini ameshaeleza jinsi gani *plan* yake atakavyoifanya na akasema kuna majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, na ndio ilivyo. Lakini je, tuangalie fungu lake zuri la fedha. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Spika, kama hamukumtilia fedha za kukimu haja, basi tusidanganyane bwana, tutampigia mabuti mpaka mtachoka, lakini hana fedha.

Mhe. Spika, ndio maana nikasema kuwa hebu tuangalie mradi gani wa kuweza kuusaidia katika bajeti hii, kwa kusema kuwa miradi yote, Mhe. Spika, tutajidanganya bwana. Lakini hata hivyo sasa hivi tukiangalia wamejitahidi vya kutosha, sehemu nyengine tayari maji yanatoka, sehemu nyengine tayari visima vinachimbwa kwa nguvu zaidi. Kwa hivyo, iliyobakia ni *plan* ya *fitting* tu.

Mimi nasema ni *fitting* ambayo ndio iliyokuwa sasa hivi ni ngumu zaidi kuliko yale maji yenyewe kutafuta. Kwa sababu kuna matatizo nyingi tu ya *fitting*, kuna sehemu nyengine kumeshaziba, masuala ya kuingia *calcium* kufanya jiwe na kuna sehemu nyengine mizizi imeshapenya pale, imeziba kwa hivyo sio kitu cha leo na kesho kusema kuwa ni rahisi jambo hilo kuweza kulifanya, hili suala tuliangalie jamani. Taaluma hiyo na ndio inayojitokeza sasa hivi sio kama maji hatuna, maji tunayo, lakini zile njia zimeshapitwa na wakati, sasa wao wamo katika kuziboresha zile. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nafikiria hili suala tulione na tuweze kumsaidia Mhe. Waziri wetu ili kuweza kupata fedha kwa kutekeleza.

Mhe. Spika, nije kwenye afya. Mhe Spika, juzi nilikuwa hospitali, kwa bahati nzuri mwenyewe hayupo mtampa salamu zake Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili. Juzi alinikuta hospitali kule kama fumanizi tu, tulikuwa tunawasaidia wananchi wetu ambao walipata matatizo kule kwenye nyumba yangu. Mhe. Spika, kwa kweli bado hospitali yetu hatujaipatia lile jina la kusema hospitali ya rufaa, tusijidanganye, mimi nasema tusijidanganye Mhe. Spika. Nina sababu zangu kuu, kwanza unapokuwa unataka rufaa ile uwe nayo, basi uwe na vitendea vya kazi vilivyokamilika.

Naanza kwenye chumba cha upasuaji. Chumba cha upasuaji jamani hata zile nguo za kijani ni mbovu, hospitali ya rufaa hiyo, yaani yale maguo ya upasuaji ni mabovu nyang'anyang'a. Sasa unawatibu *bacteria* au unawagandisha mule. Halafu hata zile *tools*. Wanapokuwa hawa *specialist* wanaokuja kwa muda wa siku mbili au tatu wa mradi ndio tunanufaika, wanaita "mgeni njoo mwenyeji apone". Wakija wale ndio angalau tunabakia na baadhi ya vitu, wakiondoka wale hata zile nyuzi ya kushonea hatuna. Mhe. Waziri hebu tuliangalie hili suala hospitali sio kitu cha masihara jamani, roho za watu ziko pale.

Mhe. Spika, hebu tupige hesabu tuna madaktari wangapi wamebakia sasa hivi hapo hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini tukikaa tunafanya masihara, hamtembei nyinyi hospitali ndio maana, tungekuwa tunatembea hospitali Mhe. Spika, basi *Wallah* tungesema hata maposho yetu yote tuyaelekeze kule hospitali, lakini hatutembei, hali ni ngumu. Babu Juma Duni atafanya nini na Naibu Waziri watafanya nini, mtawasema kila siku pale lakini hawana kimoja watakacho kifanya, hawana kitu hawa.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi hata ile miradi midogo mdogo ile wanayokusanya wanaambiwa wapeleke hazina, hee! Jamani, hata hiyo mwachieni Mhe. Waziri, kwa sababu ile inaficha siri kama mnataka nikupeni mimi sasa. Kuna vitu vikipungua basi wananyofoa mule wanakwenda kununua vitu. Sasa wewe leo unangojea mpaka umtengee fungu basi umeshauwa, waachieni hilo fungu Mhe. Waziri ili waweze kuwasaidia wagonjwa wa dharura angalau fungu hilo liwepo.

Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa *lift* nzuri. Mhe. Spika, tuna *lift* nzuri sasa hivi *Alhamdulillah*, tumepiga kelele, lakini *lift* hiyo kuna mlango mmoja haufunguki, *minus zero*, bado kabisa pamoja na kuna naisifu kwa sababu kile kitu kipo, lakini kufanya kazi kwake haifanyi, kwa sababu mlango mmoja haufunguki sasa si sawa sawa na hakuna. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi ile ni roho bwana, madaktari waongezwe fedha, tusifikie sawa na watu wa Muhimbili, lakini wapate ili wajisikie na wao.

Mhe. Spika, watu wale wanaowalaza watu usingizi, tumebakiwa na wachache tu. Ninaowajua mimi ni wanne tu katika hospitali nzima kama nitakosea Mhe. Naibu Waziri samahani utanisahihisha, lakini nakutetea wewe hilo, usije ukanirudi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri bajeti yako naomba itaje pahala ambapo unajua safari hii utaokoa. Hilo ni suala ambalo Mhe. Waziri nakuomba kwa makusudi lifanye.

Mhe. Spika, tunakuja kwenye suala la JKU ambalo tulififu sana hapa. Mhe. Spika, juzi mimi nilisikitika sana, nilipigiwa simu Mhe. Spika, kuwa kuna ajira kule ndani ya JKU, ajira, ajira gani. Mimi nakwenda kule naambiwa kuwa ajira ya ndani ya JKT, aah! Mimi nikajiuliza hii dhana ya kuwa na JKU zamani tulikuwa tuna madhumuni gani. Mimi naomba kama ikiwa namna yenyewe ni hivi basi na hiyo JKU basi tuifute, kwa sababu Mhe. Spika, JKU na JKT dhana yake ni ile ile moja ya kuwaweka vijana pamoja, kuwaondoa hisia za mitaani na kuwaweka pale na kuwafundisha taaluma. Kwa sababu JKU ina kila sehemu ya sekta ya kujitolea mtu, ukenda kilimo ipo, ufundi wanao, uchongaji wa vitu vyote wanao, gwaride na kujifundisha mambo ya silaha wanazo na JKT halikadhalika, kwa nini tunawapeleka kule watoto wetu.

Mhe. Waziri watafutie fungu. Tatizo letu sisi hatutaki kuwapa lile posho, kule wenzetu wanalipwa sijui shilingi 50,000/-. Juzi nilipo kwenda pale nilioneshwa orodha kubwa, nikaambiwa waziri fulani ana watoto wake watatu, waziri fulani ana watoto wake wanne na waziri fulani ana watoto watano, mimi Makame Mshimba ninaye. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri hili suala tuliangalie ili tuiimarishe ile JKU, tukiwapeleka kule wanarudi, hawarudi. Idadi yetu ile tunajidanganya. Tukisema sasa hivi tuna idadi ya watu kiasi fulani, inapungua imeshaondoka hiyo.

Mhe. Spika, tizama Bambi kule unasema hapa una mbegu ile rika sijui, unataka kuwapelekea kwenye shamba lao, sasa leo wote unawapeleka JKT utampa nani alime kule, vijana wote unawaondoa unawapeleka JKT sasa kule utampa nani alime. Mhe. Waziri tafuta fungu ili uwapelekee wale vijana, angalau Shs. 30,000/= tu kwani ni nyingi hizo. Vijana wetu wazuri wamesoma kabisa, lakini hatimaye leo tunawaondoa na kuwapeleka JKT. JKT kule wanakwenda kunufaika, wanawalimisha na kuwachongesha vitu. Utakuta vitu vyao vizuri tu, unafikiria nani ni hao hao vijana wako unaowapeleka kule. Sasa mimi nakuomba Mhe. Waziri hilo ulione kwa makusudi kabisa ili uwatafutie fungu JKU iinuke kabisa Mhe. Waziri. Hatua hii iliyofika sasa hivi ndio iwe mwanzo na mwisho, tuwazuwie sasa vijana wetu tusiwapeleke kule.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuwa mimi nina maeneo maalum, sasa niingie kwenye utalii. Utalii bado sio kitu cha kukipa kipaumbele, kuna vitu ambavyo Mhe. Waziri kama utavipa kipaumbele basi mimi nafikiria nchi yetu haitokuwa masikini kamwe. Mhe Spika, wawekezaji wetu wa ndani namba tuwape nguvu zaidi. Kweli tunataka utalii. Mhe. Spika, nitatoa mfano hai, naomba unikubalie, lakini limo kwenye kanuni.

Mhe. Spika, huko nyuma ulikuwa unataka utuwekee Kiwanda cha Saruji, tulikataa. Lakini katika kukataa kwetu hatukukataa kitaaluma, kwa sababu wenye taaluma walisema *ok*, inafaa. Lakini sisi kwa utashi wetu tu tukasema hatutaki. Halafu kuna kitu kimoja mimi sipendi tusimsingizie Mhe. Rais, tuna tabia wajumbe neno sio neno Rais, au Rais anamchukia mtu fulani, jamani Rais umemsikia wapi, mimi nawashangaa kweli.

Mhe. Rais anakuwa na watu wake wawili au watatu tu, wewe wanne unalisikia wapi suala la Rais kama sio uongo ni nini, si kamba tu hizo. Mhe. Spika, tusiwasingizie viongozi wetu wa juu kwa kuwapaka tope, hutaki sema hutaki wewe tu, kwa sababu siku zote Mhe. Rais anachosema analinda ilani yake, yale aliyoyataka anataka yawe kwa watendaji wake, halafu wewe unakwenda kusema aah! Rais mradi huu alikuwa hautaki, mimi sikubaliani nalo suala hili, sisi watendaji ndio wabaya.

Mhe. Waziri na hili uliangalie vizuri. Watendaji hawa Wakurugenzi na wengine msiwakubali tu, akakujia mtu na *paper* yake akakuambia mheshimiwa hili zuri saini, Mhe. Waziri usikubaliane na suala hilo. Nenda *deep* waite wawekezaji, waite wataalamu ridhika na meza yako pale, halafu baadae toa ruhusa, lakini vyengine vyovyote tutakosa vitu vilivyokuwa muhimu. Leo Kiwanda cha Saruji wanalipa kodi kule kwa wenzetu. Wenzetu wana akili sana kwetu tukubaliane nao, wanakutizameni nyinyi vitu mnavyovikataa, wao wanavichukua na kwenda kuvipeleka kule kodi inakuwa kubwa wanalipa kule, tumekosa kodi ya saruji.

Tulikuwa na *Zanzibar Packing* ya mambo ya vyakula vile, iko wapi, jumba lile pale sijui kama halijaingia mabuibui ndio wanaokaa mule ndani. Mpaka leo hatujapata sababu yoyote ya kukataliwa mradi ule

Mhe. Spika: Unadakika tano bado.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Kuna mradi Mhe. Spika, wa kutengenezea *dryadic* huko sehemu za Manga Pwani. Mhe. Spika, hapa kwa kumalizia ile safari yangu ambayo nilikuwa nikizunguka. Sasa ndio nakuja hapa.

Mhe. Spika, maradi ule utatusaidia kutia dola, sio TShs. Utatia dola na utapata ajira ya vijana wetu wengi tu, sio chini ya 250 vijana wa Kizanzibari mwekezaji wa mradi ni Mzanzibari. Mhe. Spika, naomba chonde chonde huo mradi tuukubali, kwa sababu wale wahusika yule Mkurugenzi wa Mazingira anasema hakuna matatizo ya kuharibu mazingira. Mhe. Spika, ndio maana sisi tunaposema tukaonekana wabaya *backbencher*, kwa sababu sisi kazi zetu ni kuishindikiza serikali, tusionekane vingine Mhe. Spika, tuna uchungu wa maendeleo ya nchi yetu, hatusemi kwa kumchukia mtu, tunachukia lile jambo la mradi kukataliwa bila kuangalia taaluma.

Mhe. Spika, naomba mradi Mhe. Waziri awaite wawekezaji hawa, akae nao na wataalamu wake, halafu aridhike kwenye meza pamoja na wataalamu, asiridhike kwenye *paper*. Watakuweka kona hao wakurugenzi wako na watendaji wako, siku zote tunasema hiki kitu. Mradi mzuri, halafu anakuambia hatari, hatari yake nini. Kuna mradi pale uliokubalika wa *petrol* na ni wa mwekezaji wetu hapa mzalendo, kwa Afrika ya Mashariki nzima anaweka ma-*tank* pale. Ni nzuri, lakini je ipi ni hatari *dryadic* na *petrol*, ipi itakayoharibu mazingira. Hatuangalii hapa. Kwa hivyo, jibu hulipati hapo. Mhe. Waziri nakuomba kijana wangu liangalie kwa kina kabisa. *Dryadic* Zanzibar hatuna. Wanakwenda kule Mombasa vijana wetu, lakini hata *material* yao sio mazuri sana. Tunapeleka fedha zetu za dola kule bure tu, je tukiwa nazo sisi.

Mhe. Spika, hilo namuomba Mhe. Waziri ili uweze kusaidia na Inshaallah Mwenyezi Mungu atakuba uwezo huo ili ulifanikishe. Utakapokuja kufanya majumuisho, nakujua mimi utajibu majibu mazuri na mradi huo utautekeleza.

Mhe. Spika, pamoja na haya naomba niunge mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa asilimia 120, hiyo ni ya aina yake kwa ile furaha yangu. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii adhmu angalau kusema machache juu ya Bajeti hii Kuu ya Serikali. Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nataka niseme kwamba namtakia dua njema swahiba yangu, ndugu yangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa kweli ametuonesha dira na ametupa matumaini kwamba bajeti ya mwaka huu kwa zile tulizoshuhudia zilizopita basi tunayo tamaa. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme Mhe. Spika, kazi nzuri na nia njema aliyonayo mwenzetu haitoleta matunda kama hatutompa nguvu za ziada. Kwa hivyo, sote Wajumbe wa Baraza lako tukufu na serikali yenyewe kama Mhe. Rais alivyomteua aliona anafaa na sisi tunakubaliana naye. Kutokana na hali tuliyonayo ya uchumi wetu wa Zanzibar naomba sana tumuamini lakini tumpe kila uwezo pamoja na msaada wa yale ambayo yanahitaji nguvu za ziada. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namsifu pamoja na kumpongeza si kwamba tu nataka nisikilikane au asifiwe, isipokuwa nampongeza kwa sababu ni mkweli. Kwa kweli ndani ya kitabu hiki amekiri kwamba bado hali ya uchumi wetu wa Zanzibar ni finyu pamoja na ustawi wa jamii. Kwa hivyo, anamaanisha kuwa ipo kazi ya kufika huko tunako kuhitaji. Utamaduni wa visiwa vingi duniani uchumi wake ni biashara. Biashara za Zanzibar si jambo geni, yaani ni utamaduni wa visiwa hivi na ndio historia yetu, lakini bahati mbaya hapa katikati wimbi limetukokota na tumefika pahala pabaya na pagumu mno. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hali ya biashara Zanzibar kwa wafanyabiashara wazalendo inasikitisha kwamba sasa hatunao tena, yaani uzalendo umewashinda na si kwa sababu hawaipendi nchi yao, isipokuwa vituko vimezidi ndani ya sekta hii.

Mhe. Spika, kwa kuyaacha maeneo ambayo yangesaidia sana uchumi wetu tumekamata wafanyabiashara hao ndio waimarishe uchumi huu, tuondoe umasikini kutoka kwao pamoja na kufanya shughuli za maendeleo kutoka kwao na serikali inahitaji asilimia 90 kutoka kwa mfanyabiashara. Kwa mfano, kodi, yaani utitiri wa kodi umekuwa mkubwa mno kiasi ambacho hawawezi kuhimili na hili limekuwa gumu mno.

Kwa hesabu za haraka mzigo X ameuleta hapa Zanzibar, mfanyabiashara huyu amelipishwa shilingi 262 elfu na mzigo kama huu X ameushusha bandarini Dar-es-Salaam amelipishwa shilingi 254 elfu. Kutokana na hali hiyo, ule wa Zanzibar huchelewa kununuliwa au kumalizika basi huona ni vyema kuupeleka Dar-es-Salaam na kufika Dar-es-Salaam anatakiwa kuulipia kodi mpya.

Mhe. Spika, kuna suala la *harmonization*, lakini hili linatumika vibaya na huu ni ujanja mtupu. Kwa kweli huu ni ujanja kwa sababu umetoa kima cha juu , yaani *maximum* na hiki cha chini, kutokana na hali zetu Zanzibar tukasema tutatumia hiki cha chini, lakini hii ni *loophole* kwa wenzetu ile bakaa utakapoingia nao tena Dar-es-Salaam au Bara utailipa ile, kwa sababu kisheria haifungi kukutoza ile kodi, ndipo niliposema ni ujanja mtupu.

Mhe. Spika, maeneo haya yanadhoofisha kwa kasi kubwa hali za wafanyabiashara wetu, Wazanzibari wote kwa ujumla wake pamoja na nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ni habari njema ambazo zimenipa matumaini kwamba suluhisho, ili tuweze kurudi huko tulikotoka na ile sifa ya Zanzibar kuwa ni *Centre of Trade*. Serikali sasa ikubali kwa nia safi kabisa tuondoke hapa tulipo na umasikini usiokuwa na sababu kuitangaza Zanzibar *Free Port* na hili ndilo suluhisho na hii ni nchi yetu wenyewe. *(Makofi)*

Kwa kweli si kusema Fumba au Micheweni lugha hii haitusaidii tena hivi nani atakuja Micheweni kwa hali ilioko kule au nani aende Fumba kwa hali ile ilioko. Kwa hivyo, tunaitaka Zanzibar itangaze *Free Port* na tuone, Mhe. Spika, kutokana na hali hii tutaachwa nyuma sana. Mhe. Spika, Zanzibar ni ya Wazanzibari kuna lipi jengine tunatafuna maneno kwa nini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limetupa moyo na matumaini na siri ya uongozi wa wizara hii ni suala zima kwamba serikali hivi sasa iko mbioni katika jitihada kuona mafuta tunayachimba pamoja na gesi asilia. *(Makofi)*

Suala hili Mhe. Spika, Baraza lako tukufu wewe ni shahidi kwa sababu tumelifanyia kazi nzuri na tumefika mahala dunia sasa ikasema Wazanzibari wanakwenda kunakostahiki.

Mhe. Spika, sitaki nirudi nyuma sana hata kidogo, lakini rasilimali ya mafuta na gesi asilia waliiheshimu hata wakoloni waliotutawala hapa na leo tutakaaje sisi wenyewe tushindwe tena kuitumia rasilimali hii. Kwa kweli hatutaeleweka isipokuwa tutaendelea kutegemea misaada na washirika wa maendeleo na Mhe. Shawana Bukheti Hassan amesema hapa kwamba kuna siku watachoka mabadiliko yanavyoingia ya tabia za nchi yanawakumba wale wenzetu

tunaowategemea misaada yao, hivi kweli wataacha watu wao waje watusaidie sisi. Kwa hivyo, nadhani haya ni maswali kwa pamoja tujiulize na tujue kwamba kuna mahala tutafika tutashindwa kupata misaada hii. Kwa maana hiyo, tutumie rasilimali na Mwenyezi Mungu ametupa ni zetu, mali yetu na jambo la msingi ni kutumia vichwa vyetu kwa ajili ya kufaidika.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu ni kuhusu kilimo. Kwa kweli jitihada za serikali zinazoendelea mimi nazipongeza, isipokuwa nataka nitanabahishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kilimo kina changamoto kubwa kwa Wazanzibari. Zanzibar ni kisiwa kama nilivyotangulia kusema kina kasi kubwa ya wanaozaliwa, yaani Mwenyezi Mungu ametulaaji tunazaa vizuri na atupe watoto wa kheri *Inshaallah*.

Kwa hivyo, watoto hawa wanahitaji kulelewa tena kwenye maadili mema, lakini maadili ya leo ya kiuchumi na wala hatuwezi kuwa kisiwa na utandawazi, isipokuwa tutakuwa kisiwa kijiografia, lakini kwa masuala ya kileo Mhe. Spika, hatuna jinsi lazima tukubali kwamba tutakwenda na hali ilivyo weather we like or not na huo ndio ukweli utakavyobaki.

Kama hivyo, ndivyo kilimo chetu hiki kwa ardhi tuliyonayo kwa maoni yangu tutakuwa na maeneo machache mno ya kujivunia katika kilimo. Kwa kweli kilimo chetu suluhisho lake ni umwagiliaji na umwagiliaji ambao kwetu ni mgumu kifedha.

Mhe. Spika, kwa hesabu za haraka tunazo hekta elfu nane na kidogo, hadi leo tunazo hekta mia sita na kidogo kutoka hekta elfu nane na nukta tano na kidogo tumemudu mia sita na kidogo. Nadhani tuitizame safari ilivyo ngumu, hivi lini tutafika angalau nusu na hapa tunazungumza kilimo cha kuweza kupata chakula, lakini kilimo ambacho kitamkomboa Mzanzibari kimapato aweze kusafirisha ziada.

Mhe. Spika, katika kusafirisha sio vile bidhaa ilivyo lazima zisarifiwe, yaani *products* hizi tuweze kuzisarifu na kusafirisha kwa ajili ya kupata *foreign money* na hapo ndipo tutakuwa tunazungumza kilimo. Kwa kweli kilimo kwa upana wake ni pamoja na mifugo na uvuvi ambayo ni Wizara ya Mhe. Said Ali Mbarouk.

Lakini sehemu zote hizo zinahitaji *foreign* ili kuwekeza kwenye hizi sekta na ziwe *productive* kwetu na kwa nchi hii, vyenginevyo Mhe. Spika, hiyo productive itatoka vipi ni kwa kuwekeza peke yake na wala hatuna mnmna, kwa sababu fedha ya moja kwa moja hatuna.

Kwa hivyo, tunahitaji mazingira mazuri yaweze kujengwa ambayo yatakayowavutia wenzetu waje kuwekeza kwenye sekta hizi na hapa tutakuwa tunayo nia kweli ya kutumia rasilimali bahari, lakini na rasilimali ya chini ya bahari Mhe. Waziri ameitaja kwamba sasa ndio mwelekeo.

Mhe. Spika, kilimo hiki lazima tuchanganye kwenye mifugo na uvuvi kama kinavyosema kwa upana wake na hapa ndipo tutakuwa na *Agricultural Industrial Relationship*, yaani tutumie mazao ya kilimo, mifugo pamoja na ya baharini kwa ajili ya kupata Viwanda vya Kati na Vidogo, kwa upande wa Viwanda Vikubwa vya kidunia sisi hatuna nafasi hiyo kutokana na lile nililolisema kwamba jiografia yetu hairuhusu.

Vile vile *challenge* nyengine ambayo nimeisema kwenye kilimo ni ardhi. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwa sababu ardhi tunaichezea kama kwamba hatujui thamani yake. Kwa kweli uwezo wangu ni mzogo, lakini mimi ningetoa adhabu mbaya sana, kwa sababu ardhi ndio ya kujivunia lakini tunahitaji ardhi hii kwa watoto na wajukuu waje waitumie ardhi hii, matatizo yanayoikumba dunia kuhusu mabadilio ya tabia ya nchi kwamba ardhi yetu inaliwa kwani ni kisiwa, yaani kila siku tunapoteza eneo.

Kwa mfano, hivi tunavyokwenda maeneo ambayo ni productive kwa kilimo ndiyo tunayoyaharibu kwa kujenga nyumba, kwa sababu anao uwezo wa kujenga, maeneo ambayo yangestahiki huko kujengwe kiwanda yeye tayari ameshauza kwa tamaa ya kupata mabilioni ya mahoteli.

Kutokana na hali hii lazima serikali sasa ikubali kwamba kujenga utaratibu wa kuiheshimu ardhi hii kama ni rasilimali ya leo na kesho, vyenginevyo Mhe. Spika, tutaendelea kuimba uchumi kumbe wenyewe ni maadui wakubwa wa uchumi huo.

Mhe. Spika, napenda sana kuheshimu muda wako niseme ili tufike kwenye ile nia ya kujitegemea kwa chakula na lishe. Kwa kweli ardhi hii tukijipanga vizuri pamoja na umwagiliaji huo mdogo tutakaomudu, basi utaweza kusaidia chakula, matunda na mboga mboga ndicho kilimo tutakachoweza kujivunia.

Kwa hivyo, kilimo kama kilimo hatuna nafasi ya kujilabu, kwa sababu tumezungukwa na vikwazo kadhaa, *population* yetu inakua haraka sana na *geography* yetu haituruhusu na mengi mengineyo, uchumi bado haujakaa mahala pake. Kwa maana hiyo, haya hayatufanyi sisi kilimo tukitaje kwamba ndio mkombozi haidhuru ndicho kilichobeba idadi kubwa ya watu wetu, lakini kwa upana ule ule wa uvuvi na kilimo hiki cha juu.

Mhe. Spika, wataalamu wa kilimo wamefanya kazi nzuri na mbegu zipo. Lakini bila ya kusahau zao mama ambalo bahati mbaya sana tulilipa mgogongo ni karafuu. Mhe. Spika, karafuu imetajwa kwamba imevamiwa na watu wa magendo na ndio maana tumepoteza kwa kiasi kikubwa usafirishaji wa nje.

Kwa hivyo, mimi najiuliza miaka ya 1960 mpaka 1970 kutoka tani 65 elfu na zaidi, leo tunasafirisha tani elfu 2000 na kidogo ndio zimeibiwa na watu wa magendo.

Lakini mbona hatutaki tukubali ni karafuu au mashamba ya karafuu tumeyapa mgogongo na Mhe. Spika, mkarafuu miongoni mwa miti inayojipenda ni mmoja wapo na kuna ile kauli nayosema "Mpende Akupendaye", tena mpende yule ambaye naye atakuthamini na sisi mikarafuu hatukuithamini itabaki itusubiri sisi, kwa kweli imekufa kwa kiasi kikubwa mno. Kwa mfano, Mhe. Spika ukitembea Donge pamoja na Mkoani uione mikarafuu utapata jibu.

Mhe. Spika, leo serikali inasema itapandisha miche, itatoa taaluma kwa wakulima wa mikarafuu wenye *experience* nzuri tena kubwa ya kuendesha mashamba yao kwa ajili ya kuzalisha na kwenye asilimia 100 basi inaweza kubaki angalau 60 ama 70.

Lakini taaluma hii leo tunaizungumza Mwenyekiti wa Wenyeviti amesema imebaki mitatu na kasoro yetu iko wapi. Kwa hivyo, suluhisho karafuu zao libinafsishwe na wakulima waachiwe wafanyakazi yao wenyewe na serikali kama serikali nyengine duniani ni *Tax* tu na kuling'ang'ania zao hili tunaliua.

Mwisho si kwa umuhimu Mhe. Spika, umefika wakati sasa mafuta yatafutwe yalipo na kuchimbwa, ili tuweze kufaidika na tuondokane na hali hii ya umasikini wa kujitakia na watoto wetu wanayo matatizo ya kielimu, watu wetu wana maradhi balaa. Kwa upande wa Wajumbe wako wote humu taabani kutokana na kazi nyingi, yaani wanafanyishwa kazi ambazo haziwahusu majimboni ni kutokana na umasikini na mimi nasema wa kujitakia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni vyema kuamua kama tulivyoamua Zanzibar ni nchi ina heshima, mamlaka na kauli yake na wala hakuna sababu tulitakalo lenye faida na maslahi ya nchi yetu, sasa tunaanza tena kutafuta ushauri na tunamshauri nani na hii ni nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana na Mwenyezi Mungu atubariki. Mungu Ibariki Zanzibar, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima pamoja na kupata nafasi ya kuchangia dakika hizi.

Suala ambalo napenda kulisema mwanzo ni kumhakikishia Mhe. Shadiya Moh'd Suleiman kuwa aje jioni. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kusema nashukuru sana kwa kuingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa kweli nikiwatizama Viongozi wa Kitaifa kuanzia Mhe. Rais wa Zanzibar, Makamo wake wawili, Mhe. Waziri wetu wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na mawaziri wote wanapozungumza na wakati wanapojibu maswali naona yanatoka ndani ya nyoyo zao. Hili ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, siku moja nilipata fursa ya kukaa na mtaalamu mmoja ikiwa wananchi wanatoa maoni yao, lakini hawakumuona na karatasi walka kalamu kuandika. Mwananchi mmoja akauliza sisi tunafanyakazi ya bure hapa kukueleza haya maelezo yetu mbona wewe huandiki chochote. Kwa kweli jibu alilowajibu ni kwamba mimi nakutizama wewe usoni haya maneno unayoyasema ni ya kweli au si ya kweli, yaani anakujua kwamba unayoyasema unayaunda au ya kweli. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika nashukuru sana tukiwatizama viongozi wetu namna wanavyojieleza, yaani wanajieleza ndani ya nyoyo zao. Hii ni dalili njema inaonesha kwamba kuna nia njema ya kuwatumikia wananchi. Katika nchi ambazo masikini na zinataka kujikwamua na umasikini, basi wataalamu wanasema lazima ipatikane dhamira ya kweli ya kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Kwanza yapatikane maadili ya kufanyakazi, viongozi wawe waaminifu wenye kuwajibika, wanaheshimu sheria na wenye bidii katika kufanyakazi zao. Vile vile waweko tayari kufanya mambo makubwa na sio mambo madogo madogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri anasita nini na suala la uchimbaji wa mafuta. Tukiiangalia bajeti Mhe. Spika, tokea mapato ya ndani mpaka ya nje kuna nakisi kwa vitabu vyote viwili kile cha Bajeti na cha pili cha Mwelekeo wa Bajeti, mapato ya ndani ni shilingi bilioni 221.24 na Matumizi ya Kawaida ya Serikali ni shilingi bilioni 234.18 nakisi ya bilioni 13.

Mapato mwengine kutokana na mikopo ya serikali na hati fungate ni shilingi bilioni 16.6, lakini mchango wa SMZ katika matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 37.95 nakisi ya shilingi bilioni 21.35. Mhe. Spika, sijui Mhe. Waziri

anao mwelekeo gani wa kuzitoa kama hakuanza mchakato wa kuchimba mafuta kwa ajili ya kukopeshwa. *(Makofi)*

Mapato ya ndani ya kodi ni mbili kumi elfu nukta mbili mbili, asilimia 15 ndio tunalipa kwa ajili ya kodi. Mapato yasiyokuwa ya kodi 11.2 asilimia 5 inaonesha hatuna uzalishaji. Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi namuonea huruma sana Mhe. Waziri kupewa jukumu kama hili katika kipindi hiki ambacho wananchi wanayo matumaini makubwa. Nadhani ni vyema atafute njia sisi Baraza la Wawakilishi tulipitisha hapa kwamba mafuta na gesi vilivyoko Zanzibar ni vya Wazanzibari wenyewe.

Lakini kama yangekuwa hayo yaliyotajwa kwenye Katiba ni ya Muungano, kwa nini SMZ haijatuopa taarifa hata siku moja ya kushirikishwa katika uchimbwaji wa gesi pamoja na utafutaji wa gesi Tanzania Bara, mbona kuna kitendawili hapa, kwa sababu hivi sasa visima viko vingi ambavyo vinatoa gesi na huu ni mwaka wa tatu au zaidi na wala sisi hatushirikishwi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi hatuchimbi mafuta yetu kwa sababu tunasubiri yatolewe na yatatolewa na nani kama si sisi wenyewe. Mhe. Spika, sidhani kama atakuja mtu kuyatoa kama hatukuyatoa sisi wenyewe, kama Wazanzibari wameshasema mafuta yao basi kwenye Muungano na iwe basi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kidogo nina wasiwasi kwamba hizi shilingi bilioni 4 zilizoletwa mbele kwenye bajeti ya mwaka huu 2011/2012 kutoka 2010 wakati wanangu wana sehemu ya kukaa skuli, wengine hawajapata kama alivyosema Mhe. Mjumbe mmoja hapa kwamba hospitali hazijapata magodoro wala mashuka zinaletwa mbele ni kwa sababu gani. Mhe. Waziri ni vyema angetueleza hizi shilingi bilioni 4 zilizokuwa *broad forward* katika mwaka uliopita na kuja mwaka huu.

Mhe. Spika, suala muhimu la bajeti ni kulielezea jinsi gani inavyoweza kuchangia katika kuleta au kuzalisha ajira kwa wananchi wake. Kwa kweli pamoja na maelezo mazuri yaliomo kwenye kitabu cha Bajeti cha Kuimarisha Uchumi, lakini Mhe. Waziri bado hajatuchanganulia namna gani bajeti hii inavyoweza kuongeza ajira za watu wetu.

Suala jengine Mhe. Spika, suala la mafuta nililitaja kwa sababu nilitaka kuliunganisha kabisa na Mhe. Asaa Othman Hamad. Lakini Mhe. Spika, kuna kero nyingi na wengine hawaiti kero kwa sababu kero ni jambo ambalo ukeshalipita halikukeri tena, lakini ikiwa hata ukilala bado linakurera basi hilo ni tatizo. Kwa kweli yapo matatizo mengi ya Muungano na hasa kwenye maendeleo ya uchumi.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atueleze kinaga ubaga ni matatizo gani ambayo yanaathiri Zanzibar kiuchumi ndani ya Muungano ambayo yanatafutiwa dawa yake, ili na sisi tukajitayarisha kuyauliza, kuyatetea pamoja na kuyalinda. Kwa mfano, Mhe. Spika uchumi wetu unategemea misaada sana, lakini kuna Afisi za Mabalozi nyingi za Nchi za Nje za Tanzania.

Tunakubali kweli Mabalozi wanatoka sehemu zote mbili, lakini kwa nini Zanzibar haijakuwa na *economic attaché* katika kila Balozi wa Nchi za Nje mpaka hivi leo na hili ni suala rahisi, kwa sababu kila nchi ina-*manage* uchumi wake. Kwa maana hiyo, kwa nini haipewi fursa Zanzibar ikaweka mtaalamu wake wa kiuchumi ambaye ataambatanishwa na Balozi zile kwa ajili ya kuitafutia maslahi Zanzibar na sio Tanzania, jambo hili limeshindikana wapi. Kwa hivyo, tuangalie kwa sababu isijekuwa watu wananufaika kupitia migongo yetu.

Vile vile kuna suala la Wazanzibari walioko nje, kinadharia na ukweli hasa wanachangia sana kwenye mapato ya watu wetu, yaani mmoja mmoja katika nchi yetu. Je, wizara imeliweka wapi hili na wanalipangia mkakati gani wa kuona hasa serikali pamoja na nchi kwa jumla inafaidika na Wazanzibari walioko nje, ambao kwa kiwango kikubwa wanaingiza mapato yao katika kuwasaidia jamaa zao na wengine ambao wanataka kuisaidia nchi.

Mhe. Spika, hii ni sehemu moja ya kukuza uchumi, kwa kweli kuna nchi nyingi duniani ambazo moja kwa moja zinazo bajeti hasa za wale ambazo tunaita siku hizi Diaspora. Kwa mfano, Misri, Bangladesh, India, yaani nchi hizi zote kuna watu wako nje na wanainufaisha nchi yao. Sasa hapa kwetu mbona haijapewa uzito unaostahiki kwenye bajeti hii ambapo hivi sasa kumezungumzwa maelezo mengi kuhusu hii Diaspora.

Kwa kweli mimi napenda nikubaliane na mawazo ya wataalamu wengi wanaosema kwamba kukua kwa uchumi sio kukua kwa mifuko ya wananchi, lakini kuna ukweli kwamba ukuaji wa uchumi unaweza kukuza mifuko ya wananchi vile vile. Tuangalie sana suala zima la namna ya ugawanaji wa rasilimali, yaani tuangalie sana nmna tunavyogawana rasilimali kwa kupitia mitandao au miradi mbali mbali, hivi ndivyo ambavyo uchumi hata kama utakua kidogo kidogo, kwa sababu uchumi unapokua kidogo kidogo na ikiwa hatushughuliki na ugawanaji wa rasilimali, basi wale walioko juu watajinyakulia.

Kwa mfano, tuumeona hivi karibuni kwa sababu haya mambo yalikuwa yakionekana na fedha hazionekani ndio ikawa haijaonekana, lakini ardhi, viwanja vya *open spacies*, mashamba yote yameonekana kwamba wakubwa wamejinyakulia mashamba ama ardhi bila ya mpangilio maalum. Kwa hivyo,

inaonekana kuwa hata fedha zilikuwa zikifanywa hivyo, lakini kwa sababu zimeshatumika au hazikufanyiwa mahesabu mazuri haioneshi.

Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja atueleze ni namna gani bajeti hii inapanga kugawa rasilimali. Napenda kumpa shukurani za pekee kabisa kwa mara ya mwanzo yule ambaye unataka kwenda kumpiga vijembe basi anakupa mwenyewe kile kijembe.

Mhe. Spika, ulichelewa kidogo kutokana na shughuli zako nyingi, lakini juzi tulipewa zana nzito na Wizara yenyewe ya Fedha. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba ile nia njema niliyoisema ipo pale, kwa sababu walitaka hasa watu wajue wanachokifanya katika Baraza. *(Makofi)*

Katika hatua za kuimarisha uchumi wetu, mimi nakubaliana na vipaumbele vilivyotolewa hasa sehemu ya kilimo. Lakini kuna mwega mmoja haukutajwa na sisi tulipitisha sheria hivi karibuni ya Uhakika wa Chakula na Lishe, kwa hapa lishe kubwa hapa ni kitoweo, sasa ile kilimo ingechangwanjwa mifugo na uvuvi basi mambo yangekuwa mazuri zaidi.

Mhe. Spika, mimi naamini bahari inaweza kuleta matunda ya haraka zaidi kiuchumi kuliko hata kilimo kwanza, kwa sababu kilimo kina changamoto nyingi ikiwemo wadudu waharibifu. Kwa mfano, hivi sasa kwenye kila zao tunaandamwa na wadudu na mazao rahisi yao katika nchi hii ilikuwa ni embe, kwa sababu muwembe haitiliwi maji, yaani ukesha kuupanda basi unakuja zake na unasubiri msimu kwa ajili ya kuvuna embe. Lakini tokea tulipoingiliwa na washambuliaji wadudu au mafunza, basi imekuwa hakuna tena kula embe sisi wenyewe wala zile za kusafirisha.

Kwa hivyo, kilimo kina changamoto nyingi, lakini kama tungeliingiza na bahari, yaani uvuvi wa bahari kuu, uzalishaji wa chumvi ya kusafirisha, nadhani ingelikuwa ni mambo ambayo yangeweza kusaidia uchumi kwa haraka, ili kuweza kuki-*support* hiki kilimo na kuweza kwenda sambamba. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, katika njia za kukuza uchumi kuna eneo moja kama nilivyolitaja ni kuhusu utazamaji wa matumizi na mapato ya serikali. Kwa kweli bado hatujakuwa tayari kufuatilia namna gani matumizi na mapato ya serikali yanavyokwenda. Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi aje atupe maelezo.

Vile vile nampongeza kwa kuanza kazi hii kwa kufuatilia misamaha ya kodi pamoja na ukwepaji wa kodi na pia kuna kipengele cha Matumizi Mabaya ya

Fedha za Serikali. Kwa kweli hiki namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kipengele hiki akifuatilie ili serikali iwajibike na iwawajibishe wale ambao wanachukua mali za serikali au za umma.

Mhe. Spika, naipongeza wizara kufikiria kwamba twende katika *E Government*. Kwa kweli ni suala zuri kwa sababu ndio tunakwenda kisasa. Lakini namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atupe mwelekeo kuwa wamejitayarisha vipi, ili hao wafanyakazi ambao waliomo kwenye mawizara watapambana na mtandao huu.

Kwa mfano, hizo *Internet* zenyewe bado hazijawa na nguvu, kwa kweli wengi wetu katika maofisi hatujui namna gani ya kutumia mitandao hiyo. Kwa hivyo, si rahisi serikali kusema iende kwa *E Government* wakati hao watu wenyewe hawajui. Kwa maana hiyo, lazima kwanza tupange namna gani ya kutoa hiyo taaluma, namna gani ya kufikishwa pale pamoja na *challenges* zake zilizomo.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nichangie kuhusu suala la nishati. Katika kuweka bajeti ambayo ina uhai ni lazima suala la nishati tulitie katika uhakika wake. Kwa mfano, tumeelezwa kwenye kitabu kwamba kuunganishwa kwa mkonga wa *Mega Watts* 100 ndio kutatoa uhakika wa umeme, lakini huko kunakounganishwa hakuna uhakika wa umeme. Kwa hivyo, sijui sisi tutatoa uhakika wa umeme gani. Hilo ni jambo la kwanza.

Suala la pili kuna tatizo la kitaifa hivi sasa na bado halikujibiwa kwenye bajeti hii. Mhe. Spika, sisi tunanunua umeme *TANESCO* ambao ni wa *bulk*, umeme ambao *ZECO* ndio wanaousambaza pamoja na kuuhudumia. Lakini *TANESCO* inataka kuwauzia umeme *ZECO* wa reja reja.

Sasa pamoja na hayo, si wa reja reja tu, walitupandishia mpaka asilimia 168, kwa taarifa tulizonazo hata yale maamuzi ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete bado hayakuheshimiwa na *TANESCO*. Namuomba Mhe. Waziri atueleze kupitia kwako Mhe. Spika kabla hatujaingia kwenye deni jengine kubwa zaidi, hili limefikia wapi na linatatuliwa vipi. Kwa hivyo, kama ni kupelekwa mahakamani basi twendeni kwa ajili ya kudai haki yetu umeshafika wakati na sio kustahiyana hivi hivi tu, kwa sababu deni hili likiwepo watakaolipa ni watoto wetu na sisi wenyewe.

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze hili deni la asilimia 168 ambazo tunapewa taarifa kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ali- *ruleout* kwamba lisilipwe hilo, lakini *TANESCO* bado wanalileta, yaani bado ni deni, pamoja na hiyo asilimia wanauziwa reja reja lakini hiyo ni reja reja ya juu na hivi si ndio wanatufukuza tusiende kule.

Mhe. Spika, suala la nishati yetu mbadala, lakini kuhusu deni la *TANESCO* tunataka bajeti hii iwe ya mwisho na tuelezwe lilipofikia na ikiwa tunalilipa basi lilipwe na kama hatulilipi tukashtakiyane japo huko Geneva.

Ahsante sana.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa mchango wako huo. Waheshimiwa Wajumbe, kuna matangazo mawili kabla ya kuahirisha kikao hiki.

Tangazo la kwanza kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, Wajumbe wa Kamati hii wanaombwa wakutane kwenye Chumba Nam. 2 cha Kamati watakuwa na mkutano mara baada ya kuahirisha kikao hiki hivi punde.

Tangazo la pili wapo baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe hasa wale Wabunge wanaotuwakilisha kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanategemea kuondoka leo kwenda pale Bungeni, ili kumaliza kazi ya kupitisha Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote hao wawe wamesharudi hapa tarehe 22 siku ya Jumatano, ili kazi kama hiyo ambayo waliokwenda kuifanya huko waje kuifanya hapa. *(Makofi)*

Vile vile kwa ujumla Waheshimiwa Wajumbe wote siku hiyo ya tarehe 22 Jumatano wiki hii tunategemea kupitisha bajeti yetu. Kwa hiyo, kwa jumla Waheshimiwa Wajumbe wote tunategemea wawepo Barazani, ili tuweze kupitisha bajeti yetu kwa ufanisi mkubwa.

Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuchangia bajeti yetu hii, vile vile nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ametuletea hapa na sisi leo tunaichangia katika mtiririko wetu huu wa maendeleo kwa Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, bajeti yetu imetutajia wavuvi, wakulima, vijana, wazee na wafanyakazi na jumla ya wananchi, Serikali yetu ni serikali ambayo sasa hivi inataka kuwaweka wananchi katika hali nzuri, hali ambayo wanaondoka katika

umasikini. Bajeti yetu inatuhimiza sana kushirikiana, kupendana, kufahamiana na kwenda katika nguvu kazi. Tukitekeleza mambo haya nahakikisha kwa muda mfupi sana tutakuwa katika Zanzibar njema.

Mhe. Spika, nchi inategemea sana rasilimali zake, sisi rasilimali zetu ni ardhi, bahari na wananchi katika bajeti yetu yote imetaja mambo hayo, bahari imetajwa, ardhi imetajwa na wananchi wametajwa. Kwa hivyo serikali kama itatumia ardhi hii tukufu kama ilivyotaja bajeti kuhakikisha wakulima wanasaidiwa kwa kupewa vipembejeo, au kupatiwa matrekta kwa kulimia yaani uwezeshaji, wananchi kama watawezeshwa kupewa misaada na kukopeshwa mikopo nafuu ambayo haina masharti makubwa basi nahakikisha vijana kama tutawasomesha kwa uhakika ili na sisi tuwe na maprofesa ambao wataweza kuinua nchi hii.

Mhe. Spika, wajumbe wenzangu walizungumza sana hapa katika mafuta ambayo ni uti wa mgongo wa nchi, yaani nchi nyingi zimeegemea mafuta, hivi sasa sisi tunavua uvuvi wa kienyeji na uvuvi huu unatupa umasikini zaidi. Kwa hivyo naiomba serikali itumie uvuvi wa kileo ule ambao unatajirisha watu. Ili pweza yule anayeuzwa shilingi mbili azidi bei kwa sababu shilingi mbili itakuwa kilo ya mchele haijatimia, lakini kama serikali itachukua juhudi kweli kweli kuwasaidia wavuvi wake kwa kuwapa zana wananchi wetu wanaweza kuwa na mazingira mazuri sana.

Katika nchi zetu hizi za kimasikini viwanda ndio kitu ambacho kitaendeleza, hivi sasa serikali lazima itenge ardhi ya kujengea viwanda, sasa hivi Zanzibar ardhi hatuna yote tumeshaiuza. Je hivi viwanda tunavyovibuni katika nchi yetu tutajengea wapi, kwa hivyo naiomba serikali ihakikishe kwamba iweke ardhi maalum ya kuweka viwanda. Tunataka kuchimba mafuta hivi sasa na mafuta yanataka maeneo makubwa sana ya kuwekea matenki ya mafuta tutakwenda kuweka wapi, wakati ardhi yote imeshachukuliwa.

Kwa hivyo naiomba serikali ifanye juhudi ihakikishe kwamba inaweka sehemu maalum ya kuweka viwanda ili bajeti yetu ikija kuinuka tujenge viwanda, mimi bajeti yetu hii ninavyoichangia naona kwamba imechukua kila kitu imechukua maendele yote ya ukulima, uvuvi na vijana.

Lakini jambo jengine ambalo limetukumba sasa hivi naishauri serikali ifanye juhudi vijana wapate ajira, vijana wapate vipi ajira wajengewe nguvukazi ya kuwasomesha na maafisa wetu waingie katika vijiji kuwasomesha vijana mambo ya ajira, kwa sababu sasa hivi vijana wengi hawana taaluma ya kujiajiri. Kwa hivyo vijana wetu hawa kama watapata taaluma nzuri nahakikisha kwamba nchi yetu itaendelea.

Mhe. Spika, bajeti yetu vile vile imezungumza kuwasaidia wazee kuangaliwa na kutizamwa kwa kuhakikisha kwamba wanapata matunda ya serikali yetu, hivi sasa tuna wafanyakazi wengi sana katika madaktari wamekuwa walimu wazuri kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza, kwa sababu dasturi ya chungu ukikijaza nyama huwa kinapendeza hata ule mchuzi wake, kwa hivyo hiki leo kimejaa nyama kwa sababu hali ya nchi yetu sasa hivi imekuwa hawatizamwi vizuri wafanyakazi, kama madaktari na walimu wazuri. Kwa sababu mwalimu ndie anayeitwa daktari na daktari ndio anatibu wagonjwa, ikiwa mgonjwa yupo pale daktari hana mazingira mazuri na daktari ndiye anayeshughulikia wagojwa basi atamuwacha pale na yeye atakwenda zake.

Kwa hivyo mimi naiomba serikali kwamba iwatizame wafanyakazi wa nchi yetu hii katika hali ya mazingira mazuri, hata kuwajengea nyumba za kulala vile vile inafaa, kwa mfano kwetu Matemwe kuna walimu chungu nzima hivi sasa wanakaa Mjini au wanakaa Mkwajuni, sasa mwalimu yule kama angalijengewa nyumba pale Matemwe nahakikisha saa moja na nusu atakuwa amefika kazini barabara, lakini inahitajika akae mjini angojee basi aje Matemwe saa nne anasomesha kitu gani. Kwa hivyo bajeti yetu hii ikipita walimu waangaliwe kwa kujengewa majumba katika sehemu zao zile wanazosomesheya na madaktari vile vile wajengewe nyumba sehemu wanazofanyia kazi. Mfano daktari anakaa Mjini lakini anafanya kazi Kivunge atakwenda kumtibu mgonjwa saa ngapi itabidi akae foleni mpaka saa tano anapokuja daktari.

Mhe. Spika, jengine nchi yetu tulio wengi ni masikini naiomba serikali sasa hivi ishawishi mabenki iwakopeshe wananchi wetu fedha za kufanyia kazi, kila mwananchi akopeshwe fedha za kujiajiri na apewe vifaa vya kujiajiri kwa sababu vile vifaa ndivyo atakavyofanyia kazi, naiomba serikani na naishauri kwamba wananchi wa Zanzibar ifanye makusudi kuwakopesha wananchi wa Zanzibar zana za kufanyia kazi na fedha za kufanyia kazi.

Mhe. Spika, mimi kwa vile bado ni mwanafunzi kwa kuchangia nisiende mbali nikaja kukanyaga tope nikaroa, kwa hivyo nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kidogo na napongeza waheshimiwa wenzangu wote waliokuwepo hapa waliochangia na waliokuwa hawakuchangia, Mwenyezi Mungu awajaalie waliokuwa hawajachangia na wao awape nguvu wachangie.*(Makofi)*

Kwa kumalizia mimi kwa biana ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe naiunga mkono bajeti hii ambayo ni tegemezi, kidogo ningelizungumza neno tegemezi kwa kulitafsiri maana ya tegemezi sio kuomba lakini ni kujitegemea, tafauti kuomba na tegemezi sasa wale wanaosema bajeti yetu ni tegemezi kwa kuomba, tegemezi maana yake ni kuchunga kitu ujitegemee.

Mhe. Spika, na mimi naunga mkono bajeti hii mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya serikali, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii jioni ili na mimi nitoe mawazo na mchango wa wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini. Kabla sijaanza kuchangia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini

Tatu namshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba hii wiki iliyopita kwa umakini mkubwa na ustadi mkubwa kwa kutumia muda wa saa mbili na nusu bila ya kunywa maji, nampongeza sana kwa ukakamavu huo aliouonyesha.

Mhe. Spika, niipongeze serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta bajeti hii ambayo imewajali sana wananchi wetu, imejali wafanyakazi, wazee imejali jamii kwa ujumla kwa hivyo napongeza sana, lakini pia la msingi kwa kuweza kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa muda mfupi serikali imepiga hatua kubwa na serikali hii imeonyesha bayana na utekelezaji huo kwa sera mbali mbali na mambo mbali mbali ambayo yamekwisha kutekelezwa katika maeneo mbali mbali. Kwa hivyo naipongeza serikali.

Mimi katika bajeti hii nitazungumzia katika maeneo sita, eneo la kwanza kabisa ni ukurasa wa tano ambapo hapo imeelezea bajeti juu ya utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, katika uundaji wake serikali imeunda Wizara tatu moja Wizara inayohusika na Utumishi na Utawala Bora, hii imekusudia kuwanyanyua wafanyakazi kuwatengenezea maslahi yao kuwapanga katika kada zao na kuweza kupata haki zao zile zinazoruhusu, nadhani Wizara ikijipanga vizuri itaondoa matatizo ya wataalam kukimbia katika nchi yetu. Kwa hivyo mambo mengi atakuja kuyasema mwenyewe Waziri lakini nashukuru na bajeti kubwa imeeleza haya kwa ufupi.

Lakini pia imeunda Wizara ya Uwezeshaji yaani kusaidia wananchi walio duni ili waweze kujitegemea na kupunguza umasikini wa kipato pamoja na wakihali, wizara imeanza jitihada kubwa na wananchi tumepata baadhi ya sehemu tayari wameshaanza kupata mikopo ya kuweza kujiendesha kupitia SACCOS, vikundi vya ushirika pamoja na mtu mmoja mmoja. Sasa nadhani Wizara hizi zikifanya utaratibu mzuri basi tunaweza kufika kule tulikokusudia katika kipindi kifupi.

Lakini pia Wizara ya Kilimo imeonekana kubwa imemegwa na Wizara ya Mifugo na imewekwa pamoja na Wizara ya Uvuvi, tayari sehemu nyingi vikundi vimeweza kupewa vyombo vya kuvulia hawajafika bahari kuu lakini

wanakaribia kufika. Nadhani tukiendeleza utaratibu huu basi tunaweza kufika na bahari kuu na kuweza kuvua na mazao yakaonekana kwa jitihada ambazo serikali imeweka.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ambayo nitaizungumzia iko katika ukurasa wa kumi, hii inazungumzia muundo mkubwa wa sekta ya kiuchumi sekta ambayo inagusia zaidi wananchi wanaotumia kilimo, kilimo kimeelezwa humu kwa hivi sasa katika jamii yetu asilimia arubaini na nne ni wakulima na wavuvi na wafugaji. Serikali imeona jitihada kubwa kwamba wakulima nao wanachangia pato la taifa lakini kwa muda mwingi walikuwa hawajatizamwa, lakini bajeti hii safari hii imewatizama, kwanza imewaongezea matrekta waondoke kulima kwa vijembe kongoroka waweze kutumia majembe ya trekta kwa kuchimbua pamoja na kuburuga.

Lakini la zaidi pia zimetafutwa mbegu bora za kuwapa wakulima hao na zaidi nipongeze katika mbegu za aina mbili, mbegu za muhogo sasa hivi ziko nyingi za muda mfupi, zamani tulikuwa tunalima boma unalima kwa mwaka mzima pamoja na mbega au miezi sita, sasa hivi kuna mbegu ndogo ndogo sepidee na mwari unang'oa kwa miezi minne na wataalam wako Kizimbani mbegu zipo.

Lakini zaidi kwa kuwa petu Zanzibar tunapenda kula wali, kwa hivyo pia imetafutwa mbegu ya muda mfupi sana isiyo masharti makubwa kitaalam ambayo inaweza kupandwa hata juu kwenye migomba, kwenye majimbi ili wananchi waitumie mbegu hiyo kwa kuweza kupunguza makali ya kutafuta mchele kutoka nchi za nje.

Lakini pia bajeti imeeleza kwamba jeshi latu la kujenga uchumi JKU nao watawezeshwa ili waweze kuzalisha mbegu kwa wingi lakini wazalishe kilimo cha mpunga kwa kuweza kupunguza uagiziaji kutoka nje, hii pia itapunguza hata bei kupanda kuwa kubwa kwa hivyo naishukuru serikali kuona hili, kwa kweli kama masharti hayo yote yatatimizwa basi nadhani muda mfupi tu maendeleo yao tayaonekana.

Nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa kumi na tano hapa nashukuru kwamba serikali pia imeona, hapo siku za nyuma uchumi wetu mkubwa ulikuwa ni zao la karafuu lakini muda mrefu sana zao la karafuu tumeliacha baada ya kupata uchumi mwengine mbadala, suala la utalii kidogo pamoja na mwani, lakini nashukuru kwamba utalii una mazonge mengi na ukianza vurugu kidogo tu utakuta watalii hawaji, sio lazima vurugu ziwepo kwetu lakini nchi ya jirani tu za karibu wakiona kuna vurugu vurugu wanakuwa hawawezi kuja, na kama hawakuja uchumi wetu utakuwa chini zaidi. Sasa nashukuru serikali kwa kuweka nguvu katika kilimo cha mikarafuu.

Mhe. Spika, sasa nilikuwa na ushauri kwa serikali juu ya suala hili la kurudisha tena nguvu kwenye mikarafuu, mimi ni mkulima na mikarafuu nalima kila masika kwa sababu mikarafuu inataka mvua kidogo, mwaka jana nimelima mikarafuu ishirini lakini imeshika miwili kumi na nane imekufa. Mwaka juzi nimepanda kumi nimepata mmoja kwa hivyo miaka miwili hiyo nimepata mikarafuu mitatu, sasa nadhani tungejaribu kubadilika kidogo serikali pamoja na wenzetu wa Wizara ya Kilimo tukatizama ni tatizo gani linalosababisha, mimi kwa upande wangu sio mtaalam lakini nimeona uleaji wa mikarafuu kwenye nasari tunakuwa tunajenga mabanda tunaitia kwenye kivuli, sasa unautoa mkarafuu kwenye kivuli unaupeleka juani inakuwa mazingira mengine kabisa. Sasa ni tabu sana kutolewa kwenye kivuli ukaletwa kwenye jua nadhani hii ni sababu moja inayosababisha mikarafuu kufa kwa muda mrefu.

Sasa nashauri mikarafuu ikiatikwa kwenye nasari isifunikwe juu iwachwe tu izoee jua ikitoka pale ikienda pale hali inakuwa ni ile ile, utafiti mwengine watafanya wenyewe wataalam lakini wa haraka haraka nilioona mimi ni huo mkarafuu unaatikwa kivulini, lakini ukiwekwa juwani siku tatu tu ya nne unakufa. Sasa nashauri na hilo kama wataalam watalitia maanani wafanye utafiti, kwa sababu wakulima wengi sasa hivi mikarafuu hawachukui nasari wanachimba maboteya yale yanayoanguka chini ya mikarafuu, ukipanda kumi ile mitano inakubali kwa sababu yale mazingira tayari imeshazoea, sasa nashauri na hilo serikali walitizame.

Lakini kubwa zaidi mkarafuu ni mti ambao unajipenda sana tofauti na miti mingine, mimi katika upandaji huu nilipanda michungwa kumi haukufa hata mmoja, midoriani kumi haikufa hata mmoja, mipeya kumi haukufa hata mmoja kwa sababu haijipendi kwenye dhiki inaota tu, lakini mkarafuu unajipenda. Sasa huko nyuma kwenye miaka ya 1970 nakumbuka Wizara ya Kilimo ilianzisha timu maalum wanaita *dieback* tulikuwa tunapanda maeneo yote yaliyokuwa yawazi pamoja na kuitibu mikarafuu migonjwa. Sasa nadhani na hili serikali ingelifanya jitihada wakaweza kutafuta timu ikapanda mikarafuu maaneo wazi ambayo baadae wanaweza kuihudumia na kuweza kusaidia siku za mbele, kwa sababu hiyo mikarafuu mingi iliyopandwa na *dieback* ndio inayovunwa sasa hivi sasa na hili naona linaweza kuwasaidia.

Lakini la mwisho katika mikarafuu nashukuru serikali baada ya kuona bei za karafuu zinashuka sana ndio magendo yanakuwa makubwa sasa na hilo serikali wameliona, wamesema wataweka bei nzuri nadhani magendo yataondoka, sasa kama bei itakuwa nzuri hakuna mtu wa kwenda kuuza magendo kwa sababu kule wanafuatia bei nzuri, sasa kama serikali itaweka bei nzuri basi watu hawataweka magendo.

Mhe. Spika, mchango wangu mwengine nakuja ukurasa wa kumi na saba, huduma za kifedha nashukuru kwamba hivi sasa wananchi wetu wamehamasika pamoja na wawekezaji kwa kuweza kuja kufungua matawi mbali mbali ya benki katika nchi yetu, kwa sababu sasa hivi kuna matawi yasiyopungua kumi katika mji wetu huu wa Unguja pamoja na Pemba, wengi wanaofanya biashara benki hapa kwetu nimechunguza wanafuatia sana mikopo kwa wafanyakazi pamoja na baadhi ya wafanya biashara. Sasa utakuta benki zinanufaika zaidi kuliko wale wanaokopa, naomba na hili serikali itizame riba zimekuwa kubwa sana kwa wananchi pamoja na kuwa wanakopa lakini wanakopa kwa sababu hawana pa kupata pengine.

Sasa kama mabenki yameshafika kumi na riba bado ni kubwa haina manufaa kwetu ningeliomba serikali ikatizama suala hilo ili angalau zile benki zilizofungua hapa kwetu kwa nia ya kukopesha wafanyakazi basi kidogo riba waipunguze, lakini pia wafungue matawi mengine vijijini ambako ndiko waliko wakulima na wafanyakazi, Nungwi, Makunduchi lakini pia wafungue na benki za wakulima waweze kukopa wakulima pesa kidogo kidogo kwa kununulia mbolea, mbegu pamoja na kulimisha walimishe kwa pesa nadhani hizi benki zitasaidia sana zikenda zaidi na huko vijijini. Lakini zaidi riba iweze kupunguzwa.

Nikija kwenye ukurasa mwengine wa kumi na nane suala la ajira nashukuru kwamba serikali na hili nalo wameliona na wameonyesha jitihada waliyofanya, katika ongezeko la wafanyakazi katika taasisi za serikali pamoja na taasisi za watu binafsi. Lakini vile vile serikali imeunda wizara kutengenezea mishahara wafanyakazi wetu pamoja na taasisi nyengine mishahara ambayo itaweza kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.

Lakini pia kusaidiwa vitendea kazi pamoja na usafiri kama walivyozungumza wenzangu kuna wengine wanafanya kazi shamba lakini wanatoka mjini na wanakwenda shamba, sasa pamoja na mishahara hiyo lakini pia wasaidiwe usafiri kwa sababu ule usafiri kwa muda mrefu ulikuwa ni mia tano, sasa ukitoka Mjini mpaka Mkokotoni ni shilingi elfu moja na mia tano kwa maana hiyo elfu nzima aitafute yeye ndio utakuta muda mwingi wanakaa majiani kuomba lifti.

Sasa naiomba serikali pamoja na kwamba hili pamoja na mishahara wanaitizama lakini pia na vitendea kazi wapatiwe hasa usafiri kwa wanaokaa mjini na kufanya kazi mashamba, lakini pia kuna wengine wanakaa mashamba lakini wanafanya kazi mjini. Kwa hivyo sehemu zote mbili ziangaliwe kwa lengo la kuweza kusaidia wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu nije katika ukurasa wa ishirini na sita mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, mfuko wa JK na AK tunaishukuru serikali kwa kuleta mifuko hii miwili ambayo kwa muda mrefu tunayo lakini kitu chochote ukianza kina matatizo yake, mifuko imekuja kwa nia nzuri lakini bado haijafikiya walengwa.

Kuna wachache fulani wamefanya ujanja wale wenye biashara kubwa ndio wanaopewa, lakini pia na hao wachache waliopewa walengwa wanashindwa kuilipa mikopo kwa sababu hawakupewa utaalam wa kutosha wa kuzitumia zile pesa, mtu anapewa pesa anasema nitafuga kuku lakini hajajenga banda wala hajanunua chochote, sasa pesa ile aijengee banda halafu afuge kuku utakuta muda wa kulipa unafika na hawezi tana kulipa.

Sasa naiomba serikali itoe taaluma zaidi kwa wale ambao bado lakini wanataka mifuko basi waandikiwe mradi na waelekezwe ili pesa inapopatikana iweze kurudi kwa wengine na yale malengo ya serikali yapatikane. Matatizo yaliyojitokeza sasa hivi wale wote waliokopa mwaka mzima sasa hivi umepita lakini hata robo ya malipo hayajapatikana, sasa naomba serikali izisishe jitihada ya kutoa taaluma katika mikopo kama hii.

Lakini pia tayari imeelezwa mpango wa kukopeshwa wengine wapya, sasa ningelishauri kwamba kama serikali fedha zipo zisingojewe zile za kulipwa tutakaa muda mwingi sana, watoe fungu jengine waelimishe watu, wapewe mfuko ili waweze kujiendeleza na kujiondosha katika umasikini kwa kipato pamoja na kijamii. Nadhani ikifanywa hivyo itaweza kusaidia katika utekelezaji.

Ukurasa mwengine wa arubaini na tano unazungumzia juu ya suala la kuimarisha, kwanza nazipongeza serikali zetu zote mbili kwa kuweza kuimarisha muungano wetu na mpaka sasa hivi unakwenda vizuri na ishaalla Mwenyezi Mungu atajaalia uweze kwenda vizuri zaidi, lakini katika Muungano kuna kero ambazo tayari sehemu mbili wamekaa kuzijadili huku kwetu zinaongozwa na Makamo wa Pili wa Rais ambapo mwanzo alikuwa ni Waziri Kiongozi na kule anaongoza Waziri Mkuu.

Katika kero hizo za muda mrefu zimejadiliwa saba. Katika saba hizo zilizopata mafanikio mpaka sasa hivi ni mbili, muda umekuwa mkubwa. Nashauri kama kuna utaratibu mpya wa kuweza kuzipunguza hizi kero basi ungefanywa ili kero zikaondoka. Kero si jambo zuri si kwenye nchi, si nyumbani, si kwa jirani na si popote pale. Tungelizishauri serikali zote mbili zingekaa zikatafuta njia nyengine nyepesi tukazimaliza kero hizo.

Nimalizie mchango wangu nije kwenye suala la uchimbaji na utafutaji mafuta ambao wenzetu wameuzungumzia. Kwenye Bajeti yetu imeguswa sehemu kidogo tu, hata ukisoma huwezi kufahamu. Naomba Mheshimiwa atakapokuja kufanya majumuisho atuambie kwa uwazi kwamba suala la uchimbaji wa mafuta limefikia hatua gani.

Kama tayari kwenye kero limeshazungumzwa pia atwambie limefikia hatua gani. Wananchi wa Zanzibar tunakaa kwa matumaini gani na kwa muda gani, ili tuweze kupata haki yetu ya uchimbaji wa mafuta au ikiwa gesi. Wakati wenzetu tayari wameshachukua muda mwingi sana katika kuchimba gesi na wanaitumia.

Mhe. Spika, sisi tulibahatika kamati yako mwaka juzi nilipokuwa kwenye Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi, tumekwenda Songosongo wana visima sita, gesi inazalishwa pale inakuja Ubungo inazalisha umeme. Sasa sijui sisi kama tunachetu au vipi. Kwa sababu umeme huo sisi tunauziwa. Sasa na sisi tupate kibali kama serikali, wazungumze watuachie na sisi upande wetu tuchimbe kilichokuwa chetu tutumie kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache waliyonituma wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini naomba nitamke tena naiunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti ya serikali na naomba wenzangu tuichangie na tuipitishe. Nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu kuhusiana na jambo hili zito la bajeti ya mwaka huu wa 2011/2012.

Mhe. Spika, kwanza naomba nijikumbushe binafsi tafsiri halisi inayotokana na neno Bajeti. Kwa uelewa wangu Mhe. Spika, bajeti ni mpango wa serikali katika kukusanya na kutumia katika utekelezaji wa sera kwa kipindi cha mwaka mmoja. Yaani mpango wa serikali katika kukusanya mapato na katika kutumia. Kama hivyo ndivyo basi mimi binafsi nimeiangalia bajeti katika sura tatu.

- Sura ya kwanza ni sura ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya serikali.
- Sura ya pili ni utekelezaji wa sera pamoja na mipango ya serikali.
- Sura ya tatu ni Bajeti kujenga uchumi wa nchi.

Kama hivyo ndivyo basi naomba nianze na sura ya kwanza ya bajeti yaani ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, tunajadili bajeti ya mwaka huu ili kupata sura nzuri ya bajeti hii na utekelezaji wake. Ni vyema tukafanya mapitio katika utekelezaji wa mwaka uliopita. tutakapofanya hivyo tutajenga msingi mzuri ya kuweza kuamini kile kinachozungumzwa na kuweza kuona uhalisia wa mambo utakavyokuwa baada ya mwaka mmoja.

Mhe. Spika, mapitio ya mapato na matumizi katika bajeti iliyopita ya mwaka 2010/2011 ilituoneshea kwamba serikali ilikisia kutumia shilingi bilioni 161 na ilipanga kutumia bilioni 193. Hapo ni dhahiri utaona kwamba katika kipindi cha mwaka jana bajeti yetu ilikuwa na nakisi ya bilioni 21. Ili tuweza kutekeleza utumiaji kama tulivyopanga, serikali ililazimika kutafuta vianzo vyengine jumla shilingi bilioni 21. Tabaani hapa mara nyingi huwa tunaingia katika mikopo yenye riba ambayo kwa vyovyote vile inaweza kuumiza uchumi wetu.

Utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika bajeti ya mwaka jana serikali ilipanga kutumia bilioni 251 kwa miradi 94 na programu 25 kwa mwaka wa jana wa fedha. Ambapo SMZ ilitakiwa kutoa bilioni 39 na wahisani walipanga kutoa bilioni 211, SMZ mchango wake ilikuwa ni asilimia 15 na wahisani ni asilimia 84. Kwa mujibu wa ripoti ya Mhe. Waziri alitwambia hadi mwezi wa Machi utekelezaji wa upande wa SMZ ulikuwa ni bilioni 24 sawa na asilimia 62 na wafadhili wao walitoa bilioni 117 sawa na asilimia 52.

Hapa tutaona kwamba vile ambavyo tulikisia na utekelezaji halisi kulikuwa kuna mapungufu. Licha ya serikali kuahidi kutoa asilimia 15, lakini hadi mwezi Machi ilitoa asilimia 62 kuanzia Julai hadi Machi, hatukupata hesabu ya mwezi April hadi Julai kwa miezi mitatu ya mwisho. Hii kwa kweli si hali nzuri, ingawa ukiangalia tukiambiwa mwezi wa April, Mei na Juni, utaona kuna kitu kinajificha kwa sababu hesabu zake hazijapatikana.

Tukuchukulie uhalisia wenyewe wa utekelezaji katika mtindo wa miezi mitatu mitatu. Kama mambo yangelikuwa yanakwenda vizuri kuanzia Julai mpaka mwezi Machi serikali ilipaswa ichangie bilioni 29 ambayo ni sawa sawa na asilimia 74 ili miezi mitatu iliyobakia ndio tutasema hapo tunamalizia kwa miezi mitatu.

Kadhalika na wahisani nao walipaswa katika kipindi cha miezi tisa wachangie bilioni 158 sawa na asilimia 74, lakini hali ikenda tofauti hivyo. Hapa tunapata picha kwamba utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana kwa kweli haukuenda kama ambavyo licha ya serikali kukisia makisio madogo katika bajeti yake ya maendeleo. Kwa kweli upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kama vile ambavyo ilitegemewa.

Kwa bajeti hii ya mwaka 2010/2011 serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 221 ambapo bilioni 234 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Vile vile kuna nakisi, mwaka jana ilikuwa kuna nakisi ya bilioni 21, mara hii kuna nakisi ya bilioni 12. Ni dhahiri ukiangalia utaona kwamba waziri kafanya juhudi kubwa ya kupunguza nakisi lazima tumsifu. Tulitaka aondoshe kwa asilimia 100 lakini tunajua hali halisi ilivyo.

Mpango wa maendeleo nao Mhe. Spika, ulipangiwa mwaka huu kutumia bilioni 378 ambapo na ziada ya bilioni 127 sawa sawa na asilimia 44. Tutaona ni namna gani bajeti ya maendeleo mara hii ilivyokuwa kubwa. Ikiwa mwaka jana ilikuwa ndogo tukashindwa kuitekeleza mara hii sijui vipi tutafanya miujuza ya kuitekeleza. Katika hiyo SMZ imepanga kuchangia bilioni 37 na wahisani kuchangia bilioni 344 sawa na asilimia 90. Hapa tutaona ni namna gani ambavyo serikali yetu bado mchango wake katika sekta ya maendeleo ni mdogo.

Mhe. Spika, hili nadhani ni ajenda ya kuangalia, kwa sababu ikiwa shughuli ni yako na wewe uchangiaji wako ni huu siku yule mfadhali atakaposema keshanuna maana yake nikusema na wewe kwa asilimia yako 10 ambayo utekelezaji wake ni asilimia 50. Hilo ni tatizo ambalo linahitaji mjadala.

Katika hali hiyo Mhe. Spika, ya kuangalia bajeti ya mwaka jana na utekelezaji wake na makisio ya mwaka huu, tafsiri niliyoitoa ni katika mambo yafuatayo.

Kwanza tukubali ni kweli tuna tatizo la ufinyu wa makusanyo ya ndani. Makisio ambayo hayawezi yakakidhi hata matumizi ya kawaida kwa uendeshaji wa kiserikali. Kama hivyo ndivyo maana yake tunakusudia ili tuweze kutekeleza shughuli za kawaida za serikali maana yake tunahitaji sasa tuweze kukopa ili tukidhi kuiendesha serikali. Tukope katika mashirika na katika hili naomba nimuulize Waziri. Mwaka jana tulikopa katika mabenki, bilioni 3 mara hii tumepunguza kukopa mabenki bilioni 1. Tulipunguza kukopa benki tulikimbilia kuweka hati fungate maana tunajua kwamba tukikopa benki, benki ni zetu, benki zitawanufanisha wananchi. Lakini kuweka hati fungate kwa mashirika au pengine kwa wafanyabishara binafsi, watakaofaidika na riba ni wafanyabiashara binafsi.

Hebu tuambiwe hali ikoje, kwa nini tukawacha kukopa benki ya PBZ ambayo faida itakuja kuwanufaisha Wazanzibar, lakini matokeo yake tukimbilie kuwakopa wafanyabiashara binafsi ambao inawezekana hata Baraza lako halijui faida na hasara itakuwa ni ipi. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe elimu katika hili. Mhe. Spika, hiyo tafsiri inayoonekana katika bajeti hii ya mwaka huu.

Ushauri wangu wa kwanza Mhe. Spika, naiomba sana serikali kupitia Wizara ya Fedha na Waziri kujaribu kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato. Lazima tufike mahala sasa tufikirie kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato. Eneo la kwanza ni hili ambalo tayari linaonekana. Mara hii hakuna ongezeko la kodi, kwa kweli mambo yanakuwa ni mazuri. Tuamini kwamba tayari eneo la kwanza katika misamaha ya kodi napenda nimpe pongezi kwa anavyolisimamia eneo hili. Namuomba azidi kukaza buti katika eneo hili la misamaha ya kodi. Eneo hili linapoteza fedha nyingi sana za walipa kodi.

Mhe. Spika, eneo la pili katika kuimarisha wigo ni kodi kutokana na mashirika ya serikali na hili nampongeza waziri. Kwa muda mwingi tumekuwa na mashirika lakini yalikuwa yanaonekana kama ni mzigo. Hayalipi kodi, hayawezi kujiendesha, lakini waziri kaanza kuchukua juhudi ya kuyabana mashirika na mashirika kuanza kulipa kodi. Katika eneo hili namuomba Mhe. Waziri azidishe juhudi.

Eneo jengine ambao nashauri kuna taasisi ambazo zinajitegemea, naomba Mhe. Waziri liangalie eneo hili. Serikali ifike pahali hizi taasisi zinazojitegemea ziachie zisimame kwa miguu yake wenyewe. Tupunguze kadiri inavyowezekana kila mwaka ruzuku katika taasisi kama hizo. Kama taasisi haiwezi kujiendesha maana yake ni bora wafunge virago na watafute kazi nyengine wafanye.

Eneo jengine ambalo ni nyeti ambalo linaweza likatuongezea fedha katika uchumi wetu ni suala la mafuta. Suala la mafuta halina mjadala wala halina mbadala. Baraza lako hili ndilo lililokaa likaamua kwa kauli moja kwamba sasa hivi tunashughulikia suala la mafuta. Lakini leo inashangaza sana kuanza kusikia lugha za pembeni pembeni kwamba tunasubiri itolewe mpaka kwenye Bunge. Sivyo tulivyokubaliana katika kikao kilichopita. Tulikubaliana kwamba tuwache taratibu ziendelee lakini na sisi hapa tunaendeleza taratibu zetu. Lugha hii tusubiri kwamba mambo mpaka yatatuliwe katika kero za Muungano, hatutaki.

Mhe. Spika, suala hili Wazanzibar tayari tumeshaamua hatuna maelezo mengine. Katika hili nawaomba sana Wawakilishi wenzangu Mawaziri wasituhangaishe katika suala hili. Kama hawana uwezo waache kiti. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja. Hili linaanza kunipa wasi wasi kwa sababu hebu watueleze katika bajeti hii, maana bajeti nzuri ni ile ambayo ina muendelezo wa mipango iliyopita nyuma. Sasa ikiwa tayari tumeshaliamua hilo bajeti hii imetenga fungu gani katika kuliendeleza hilo.

Inawezekana jawabu likaja kwamba kuna watu ambao sasa hivi wanasoma huko. Wanaosoma waache wasome lakini ndani ya nchi kuna taratibu nyengine

ambazo ni lazima ziendelezwe. Kuna suala la sera, kuna suala la sheria, mbona hatujaziona hapa. Tunasema kwamba bajeti hii ya mwaka 2011/2012 lazima iwe na *component* ya kuliendeleza suala la mafuta. Vyenginevyo kama halimo humu, sijapekura vizuri lakini hapa patakuwa na kazi kweli kweli.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo namshauri Mhe. Waziri Mhe. Spika, ni kuhusiana na mgao wa mapato yanayotokana na muungano. Mhe. Spika, Katiba yetu ya Muungano, mtaalamu wangu wa Katiba Mhe. Salmini sijui yuko wapi hapa? Katiba imeelekeza kwamba serikali kuwe na mfuko wa *account* ya pamoja ambayo itahusiana na matumizi yanayotokana na shughuli za muungano.

Katiba ndivyo ilivyoeleza hapa. Maraisi wetu wote wawili wameapa kwa katiba hizi. Mbona hadi leo *account* hii haijafunguliwa tatizo ni nini? Kifungu cha 133 kutokutekelezwa kifungu hiki ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Hatungeliweza kutazamia kwamba serikali yenyewe iliapa, maraisi wetu waliapa, mawaziri wetu waliapa, kutekeleza Katiba hii iliyokuwepo leo tufikie katika kiwango cha kuvunja Katiba. Tunachotaka sasa hivi ni kuwepo hiyo *account* ya pamoja kama ilivyoelezwa, sijui Waziri atakuja kutueleza nini, lakini katiba hii ni ya zamani, haya mambo yapo zamani hakuna suala la kubabaisha kutafuna maneno, lazima sasa tuelezwe juu ya hili.

Mhe. Spika, katika jengine ni suala la *GBS (General Budget Support)* tunadhani hili ni eneo ambalo Serikali yetu ya Zanzibar inaweza ikapata fedha nyingi. Hatuna uhakika kwamba hii 4.5% inayoletwa hapa tulioambiwa kwamba tutapata bilioni 30 kwamba ndio asilimia ya mgao wa 4.5, hatuna uhakika.
Mhe. Waziri hebu utakapokuja tueleze mara hii serikali inategemea kupata kiasi gani katika eneo hili na mgao wetu katika 4.5 utakuwa ni kiasi gani. Kwa sababu sisi wengine tuliokuwa hatukusoma hesabu kwa kweli bado hatujaamini vizuri kama mgao wake utakuwa kwa Zanzibar ni bilioni 30. Mhe. Waziri atakapokuja hebu atueleze vizuri.

Mhe. Spika, la pili ushauri wangu ni lazima tudhibiti mapato yaliyokuwepo. Katika kudhibiti mapato ni lazima tufikie pahala tuboreshe mfumo wa ulipaji kodi. Mfumo wetu wa ulipaji kodi bado unamatatizo. Tuna vyombo viwili *TRA* na *ZRB, TRA* ni tatizo kwa Zanzibar.

TRA iondoke iende ikafanye kazi huko tufanye kazi ya *ZRB*. Lishakuwa ni tatizo kila anaesimama hapa *TRA, TRA*, hivi mambo haya yanakwendaje? *TRA* iondoke ili *ZRB* wachukue kila kitu ndio tukusanye kodi.

Mhe. Spika, vile vile utaratibu wa kwenda na mkoba au utaratibu wa kuwa Afisa wa Kodi kwenda kudai kodi kwa mkoba umeshapitwa na wakati. Sasa hivi hawa maofisa wetu wa *ZRB* na wengine wanakwenda kwa wafanyabiashara na mikoba.

Hii ni dalili moja ya rushwa na vitu vyengine. Hebu mfumo wa ulipaji kodi urekebishwe, kuna mfumo siku hizi tunausikia duniani wengine hatujawahi kwenda kwamba kodi zote unazolipa kila mtu alipe popote na watu wawe wanaona kwamba fulani aliyekuwepo Matemwe sasa hivi kalipa shilingi 50. tutafika lini huko.

Mhe. Spika, pia tupunguze matumizi ya serikali yaliyokuwa hayana lazima. Watu wamesema serikali kubwa. Mimi sitaki niseme hilo lakini hii *fashion* ya safari za nje zilizokuwa na hazina tija. Tunapenda sana mawaziri wetu waende nje kwa sababu bila ya kwenda nje hapa hakuna tutakachokipata.

Nataka kuiambia serikali kwamba hawa mawaziri wanapokwenda nje wasiende kwa kutembea tu kule tunataka kila anayekwenda aje atupe chumo alilolipata huko. Ili fedha zetu zionekana kwamba safari hizi zinatija fulani kwa nchi, vyenginevyo Mheshimiwa zuia safari za nje, safari za utalii zuia.

Mhe. Spika, la mwisho katika eneo hili ni lazima tufike pahala tudhibiti matumizi ya serikali. Hii tutaipata kupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, mimi naamini kwamba hichi kidogo tulichonacho iwapo tutakitumia vizuri naamini kwamba kinaweza kikapiga hatua. Lakini inavyoonekana kwamba hichi kidogo tulichonacho basi kinaingia katika mifuko na hakifiki kinapokusudiwa. Katika eneo hili naishauri serikali tuzingatie sana maelezo yaliyokuwemo katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na ripoti za *PAC*. Fedha nyingi sana hazifiki katika lengo lililokusudiwa.

Mhe. Spika, jengine kwamba kuna udogo wa mchango wa serikali katika maendeleo. Hilo tumeliona na hilo nadhani halina maelezo. Kwa sababu hata tukimtaka Mhe. Omar atoe maelezo hana maelezo. Ni kweli kwamba mapato ni kidogo, hana vya kuyafanya isipokuwa ni kuchukua juhudi hizi ambazo tunamshauri.

Lakini vile vile tatizo jengine tatizo la utekelezaji na upatikanaji wa fedha katika miradi. Hapa nashauri tusiwe na ufahari wa kueleza tu, kwamba mara hii tuna wingi wa miradi katika bajeti zetu. Ikiwezekana tuchague miradi michache kwa mwaka ambayo tunao uwezo wa kuitekeleza. Kadiri hali inavyoonekana ni

kwamba miradi hii nimeshaeleza mwaka jana tulikisia nini na kikapatikana nini. Mara hii *trend* inakwenda ile ile tunakisia lakini upatikanaji wake si mzuri. Tunachoomba basi angalau tuchague miradi michache ambayo tuna uwezo nayo ya kuitekeleza. Kuliko kusema kwamba mara hii tunazidisha aina ya miradi pamoja na program.

Mhe. Spika, sura ya pili ya bajeti ni utekelezaji wa huduma ya kiuchumi pamoja na kijamii. Mhe. Spika, kuna usambazaji wa maji katika bajeti hii imo, usafiri na mawasiliamo, biashara, elimu, afya. Tatizo ni kwamba mara hii kama ukiangalia katika kitabu hiki. utaona ni *item* mbili nayo ni *component* mbili ambazo zimeongezewa fedha katika fungu lile la miradi ya maendeleo.

Kuna usambazaji wa maji mwaka jana tulikisia kutoa bilioni 33 mara hii tutatoa bilioni 60 ikiwa ni ongezeko la asilimia 55. Tunajua kwa nini serikali ikafanya hivyo kwa sababu nguvu kubwa inataka ielekeze katika eneo hilo. Vile vile nguvu za asilia mwaka jana ni bilioni 23 mara hii ni bilioni 39 sawa sawa na ongezeko la asilimia 40, iliyobakia yote imepunguziwa. Mathalan usafiri na

- Mawasiliano 52 mpaka bilioni 3
- Biashara bilioni 2 mpaka Nil. Hii hatujui maana yake nini
- Elimu 46 bilioni mpaka bilioni 6
- Afya bilioni 10 mpaka bilioni 9
- Huduma za Kijamii 24 mpaka 497 na kadhalika.

Katika hili ingawa kidogo kuna matatizo. Ukichukua kitabu kile cha mwaka jana utaona kwamba *component* hizi zimepangwa vizuri. Ukija kwenye mawasiliano na usafiri utaona kwamba *component* zake zote ni zinazohusu Wizara ya Mawasiliano. Mara hii usafiri na mawasiliano kuna wasilisha mawasiliano ya Afisi ya Rais Ikulu, programu ya Miundombinu ya soko, kuongeza thamani ya misaada vijijini, programu ya kudhibiti malaria. Hiyo yote ipo katika *component* ya usafiri na mawasiliano. Na bahati mbaya hata ukipiga mahesabu utakuja kuta *total* yake imeingizwa. Tukija tukiliruhusu hili kufanyika maana yake bajeti yetu itakuwa tunapitisha kitu ambacho huko mbele hakitoweza kuja na Baraza hili ndilo lenye wajibu ya kulizungumza hilo.

Tukija kwenye suala la Elimu ukiangalia *component* za elimu ukichukua kitabu cha mwaka jana utaona kwamba ni mambo yanayohusiana na Wizara ya Elimu. Lakini mara hii mambo ni mchanganyiko, humo humo kwenye elimu utakuta kuimarisha Chuo cha Utalii, uimarishaji wa Uwanja wa Kimataifa Karume Air Port, uimarishaji wa Mazingira Tanzania, taaluma ya afya, imeingia katika *component* hii. Mhe. Waziri hebu hapa tuweke sawa na mahesabu yakae sawa ili tujue tunachokipitisha ni kitu gani.

Mhe. Spika, katika hili nadhani kuna mambo ambayo tunasema tunayapa kipa umbele lakini fedha yake imeteremka sana. Kwa mfano elimu bilioni 46 mpaka bilioni 6, afya halikadhalika imeshuka kwa *negative* 6 na mambo mengine. Hebu ufafanuzi wake unakuwaje.

Mhe. Spika, katika sura ya tatu ni katika Bajeti na utekelezaji wa Sera. Mhe. Spika, kwa vyovyote vile bajeti inataka kujibu matatizo ya wananchi, ndio maana ya bajeti. Wananchi wetu sasa hivi wana tatizo kubwa la ajira, hebu bajeti itwambie bajeti ya mwaka huu inakusudia kutengeneza ajira ngapi. Maana yake bajeti haikutwambia.

Vile vile tuna tatizo wananchi wetu wana kilio kikubwa sana kwa upandaji wa bei za bidhaa hasa chakula. Sasa hivi ni *crisis* kubwa huko nje. Katika hili hebu bajeti itwambie kwa tatizo hili ambalo linaikabili jamii yetu serikali imeliangalia vipi na kuliweka katika bajeti hii. Sisi tunadhani serikali ni lazima ifike pahali kwa *crisis* kama hizi i-*subsidize* mambo kama haya kwa sababu na hilo linawezekana. Inawezekana kwa sababu tayari imeshawezekana nyuma.

Mhe. Spika, utakumbuka kwamba kisiwa cha Pemba kipindi chote umeme uliokuwa ukilipwa Pemba ilikuwa haukidhi. Serikali ilikuwa ikifanya nini? Serikali ilikuwa ikitia mkono wake pale. Kwa nini katika hili hususan bei ya mchele, unga na sukari kwa nini serikali haiwezi kuweka mkono wake pale ili angalau wananchi wakapumua katika kipindi hichi ambacho serikali inajipanga katika kukabiliana na suala hilo. Mhe. Spika, hilo Mhe. Waziri aliangalie ili tuone kwamba wananchi wetu wanajipanga vipi.

Jengine ni uzalishaji katika kilimo na mifugo, watu wetu wanahitaji mitaji, wahataji elimu, wanahitaji masoko na suala zima la biashara ambalo kwa vyovyote vile bajeti hii ilipaswa itoe jawabu katika hali hiyo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumshauri Mhe. Waziri kwamba apambane na changamoto hizi. Naamini Mhe. Omar anao uwezo mkubwa sana. Kazi yake kubwa kwanza ni kuondosha nakisi katika bajeti yetu. Kazi nyengine ambayo atapaswa kuifanya ni kutanua wigo wa vyanzo vya mapato na kudhibiti mapato ya ndani. Tunaamini atakapofanya hivi utekelezaji bajeti hii ya mwaka 2011/2012 hauna shaka tutautekeleza kama ambavyo inakusudiwa. Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Tanzani na Mungu ibariki Afrika. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo tu katika bajeti hii. Mhe. Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo matatu. Nitaanzia katika mapitio ya hali ya uchumi.

Mhe. Spika, kitabu hiki kimetueleza kwamba kuna pingamizi kubwa ya kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni suala zima la umeme na mambo mengine. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri kwamba bado ningeliomba ufanywe upekuzi mkubwa mno na *research* nzuri kutokana na suala hili.

Mhe. Spika, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri atuambie bila ya kificho ni kitu gani hasa cha ndani kinachotuathiri kushuka kwa uchumi wetu, pengine kuna kitu ambacho kinatuathiri namuomba Mhe. Waziri atueleze jambo hilo.

Mhe. Spika, lazima tufikie pahala Wazanzibari tuwe na mambo tunayoweza kumiliki ndani ya bajeti hii. Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa umeme sisi hatumiliki, pia sera ya kodi hatumiliki, sera ya fedha hatumiliki. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ndio maana wakati tulipokuwa tukipitisha ile sera ya dira ya 2020 tulisema kuwa sera hii haitekelezeki.

Mhe. Spika, ndio maana hadi leo bado dawa ya kuondosha umasikini haijapatikana, kila siku hali, gharama za maisha zinazidi kupanda. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa lengo lile lile na nia njema namuomba atueleze ni kitu gani hasa cha ndani kinachotuathiri juu ya ukuaji wetu wa uchumi. Hilo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze.

Mhe. Spika, eneo la pili nataka niingie katika sehemu ya ajira, Mhe. Waziri hapa ametueleza takwimu za ajira. Mimi namuomba Mhe. Waziri kwamba takwimu hizi hazitoshi na takwimu hizi haziko sahihi hata kidogo kwa sababu penye salama pana alama. Mhe. Spika, niliwahi kusikia hotuba moja ya Mhe. Rais anasema wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege omba omba wote waondoshwe. Kwa hivyo, hii ni hali ambayo inaonesha kwamba hali ya ajira inasuasua. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe na mimi ningeliomba tuelezwe ni ajira ngapi zilizopangwa kuajiriwa mpaka mwakani.

Mhe. Spika, eneo la tatu napenda kuchangia kuhusu mfumko wa bei. Mhe. Spika, mpaka sasa hivi bado hatujaona dhamira nzuri hata kidogo kwa mabenki yetu. Kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu mabenki yanawakopesha walioajiriwa tu, hawajawakopesha wale wanaojishughulisha na kilimo. Lakini kushuka kwa wananchi wanaojishughulisha na kilimo bado hawajakopeshwa. Mhe. Spika, ukitizama hata kile ambacho kilichogeuzwa jina sasa hatuhalalishi riba kwamba sasa kimegeuzwa jina kinaitwa marejesho, hivyo hata yale marejesho yanayorejeshwa yamekuwa ni hali mbaya sana.

Mhe. Spika, hata ukija ukitizama katika hizi sehemu za wakulima juu ya mfuko wa wawezeshaji. Mimi namuomba Mhe. Waziri akija hapa atueleze juu ya Mfuko wa Uwezeshaji wa JK na AK ni wakulima wangapi ambao wako vijijini

wamepatiwa mfuko huo. Mhe. Spika, ni kwamba kitu hiki hata hiyo misaada wakulima haiwafikii, na ndio maana inaonekana kuwa kila siku mfumko wa bei unazidi kuendelea kupanda juu na kuathiri uchumi wetu.

Mhe. Spika, sasa niingie katika hii sehemu ya kumpongeza Mhe. Waziri. Mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhamira ambayo aliyokuwa nayo katika kitabu hiki na vitabu vilivyopita, inaonesha ana adhma ya kuanzisha viwanda, lakini hii itakuwa ni adhma endelevu. Mhe. Spika, matarajio yangu ni kuwa adhma hii kila siku kubakia itakuwa haitoshi, nilifikiria kwamba bajeti hii ingelitueleza kuwa mwaka huu tutaanzisha kiwanda cha maembe kule Pujini, hivyo tungeondokana kununua *juice* za Oman kila siku.

Je, Mhe. Waziri sisi kila siku tutakuwa tuko katika adhma mwakani tutakuja kukuhoji kitu gani? Mhe. Spika, mimi nadhani hii adhma ya kila siku basi tuone tunafikia kikomo, hivyo namuomba Mhe. Waziri tuhisi, tujue au tungelielezwa kwamba mara hii tuwe na viwanda na viwanda hivyo vitatumia rasilimali gani. Mhe. Spika, mimi kutokana na mchango wangu mfupi na mimi niseme naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti hii, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa nikiwa mzima wa afya na kuweza kuchangia bajeti hii.

Mhe. Spika, pia sina budi kumpongeza Mhe. Waziri kwa bajeti yake nzuri ambayo imelenga malengo ya mwaka 2011-2012, na tunaunga mkono kwa dhati kabisa mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani asilimia kwa mia.

Mhe. Spika, kwanza nataka kuchangia kuhusu utalii, hivi sasa tumekuwa na nafasi ya utalii kwa asilimia kubwa ambayo ndio tunaitegemea. Mhe. Spika, ni kwamba wananchi wengi wanategemea utalii kuweza kuendesha maisha yao pamoja na kuliendesha taifa letu. Lakini utaona watalii wamefika kuekeza matokeo yake wao wamekuja kukopa sio kuekeza. Mhe. Spika, watalii hivi sasa mpango wao mkubwa ni kuweza kukopa kwa wananchi, na katika kukopa kwa wananchi mategemeo yao ni kuendesha mahoteli yao ambayo wameekeza.

Mhe. Spika, tulitegemea wawekezaji watakuwa wakubwa wa kuweza kutoa fedha nyingi ili kuweza kuendesha taifa letu, lakini wao hivi sasa inaelekea ni watu wa kwanza kuweza kufilisi taifa pamoja na wananchi wetu. Mhe. Spika, wananchi wengi utakuta sasa hivi wana mikopo serikalini, lakini utakuta wanauza majumba yao kutokana na kukopa fedha nyingi na kupeleka vitu kwenye mahoteli na mahoteli yale hayachukui adhma ya kuwalipa wananchi. Hivyo, baada ya mwaka au miaka miwili utasikia Mkuu wa Hoteli fulani ameshaondoka na mwananchi yule hana kitu cha kulipa.

Mhe. Spika, kutokana na bajeti yetu imesisitiza sana wananchi kupewa kipaumbele, ni vyema serikali ikawaita wawekezaji wakapangiwa azma ya kuwa wameekeza na wafahamishwe jinsi gani juu ya kuweza kulipa wananchi, ili waendeshe maisha yao na taifa letu. Mhe. Spika, kama sio hivyo wawekezaji hao wataendelea kufilisi wananchi na kufilisi taifa letu lisiwe na malengo huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, kuhusu nafasi ya ajira kwa JKU ni kwamba tulitegemea ndio nguvu kazi sasa hivi kwa vijana kuweza kuendesha taifa kwa kilimo cha kisasa. Mhe. Spika, vijana hawa kwa muda hivi sasa maslahi yao yametupwa sana kutokana na kuwa walitegemea wanakwenda kujenga taifa huko JKU na watapata kujifunza mambo mengi na watapata ajira. Lakini utakuta ajira JKU zimefutika hata vijana kukata tamaa kabisa, kijana wa JKU anaajiriwa tena kutoka JKU anaambiwa sasa unaajiriwa kwenda JKT.

Mhe. Spika, ni kwamba vijana hawa utakuta kwa muda mrefu wameanza kuvunjika moyo kabisa kwa kuanza kuajiriwa JKT badala ya kuwa wameshakaa JKU kwa miaka miwili hivyo anaenda tena JKT hajui muda gani atapata ajira, na huko pengine atakaa kwa miaka miwili na matokeo yake anarudi Zanzibar bila ya kupata ajira yoyote.

Mhe. Spika, hivyo tunaomba zaidi kwa vijana wetu wanapokwenda JKT wapate ajira kama ilivyokuwa imepangwa mwanzo hapa Zanzibar ilikuwa JKU wanapata ajira moja kwa moja kwenda katika serikali. Lakini sasa hivi utakuta vijana wanachukuliwa moja kwa moja kwenda JKT na kule hakuna ajira ambayo inapatikana. Mimi naona ajira hizo zimeondoka kabisa hadi uweze kwenda JKT ndio uweze kupata ajira, hivyo tunaomba vijana hawa warudishiwe nafasi yao ya kutoka JKU hadi kupata ajira moja kwa moja kwenye vikosi vya ulinzi kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya kusoma hadi darasa la kumi na mbili ndio vijana wapate ajira kwa Zanzibar, naomba iendelee kama ilivyokuwa hapo awali vijana waweze kupata ajira darasa la kumi, kwani tunajua watu wote wanaokwenda JKU walikuwa ni darasa la kumi, darasa la nane na darasa la saba. Mhe. Spika, hivi sasa ikizingatiwa kuwa vijana hao walikuwa ndio nguvu kazi kubwa kwa ujenzi wa taifa letu.

Mhe. Spika, mwana 1978 vijana wetu waliweza kufanya jambo moja kubwa la taifa katika vita vya Uganda, vijana wengi waliopigana vita hivyo utakuta ni hao hao wa darasa la saba, la nane na la kumi. Mhe. Spika, iweje hivi sasa vijana hao wakose ajira kwa kuwa hawakumaliza darasa la kumi na mbili au Chuo Kikuu.

Mhe. Spika, hivi sasa vijana wengi wa Zanzibar wako katika vijiwe hawajui wafanye nini kwa sababu darasa lao ni la saba, la nane na la kumi, wao wanachokisema ni kuwa hawapati kazi hivyo wanasoma nguvu kazi ya wizi. Kwa hivyo, muda mwingi itakuwa tunakataza masuala ya kuvunja wizi na kueneza askari jamii kwa vile vijana wetu hatuwasaidii kwenye ajira na kama hatutoi ajira itakuwa ndio tunafuga wenyewe wizi katika serikali.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunaunga mkono bajeti hii mia kwa mia kwa yote ambayo yamepangwa na serikali.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii na mimi nikaweza kuchangia bajeti hii.

Mhe. Spika, pia nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake katika wizara yake. Pongezi zangu nyengine natoa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein) kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hii ni bajeti ya kwanza ya awamu ya saba na ina lengo la kuwahudumia wananchi kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, naiomba serikali iweke mkazo kwa mambo yafuatayo:

1. Kuimarisha ukusanyaji wa kodi ndani ili iweze kuwahudumia wananchi vizuri.
2. Serikali iwe makini katika kudhibiti matumizi yake.

Mhe. Spika, pamoja na serikali kufanya mazuri katika mwaka 2010-2011 bado hali ya maisha ya watu hapa Zanzibar ni ngumu, hivyo kumekuwa na mfumko mkubwa wa bei wa vyakula kama vile mchele, sukari, unga, mafuta ya kupikia na mafuta ya usafiri kila siku bei inapanda kupita kiasi.

Mhe. Spika, hali hii sisi wanawake inatusumbua sana kwa sababu ukiwa ni tegemezi wa watoto katika jamii na tukiwa ni walezi wakuu kwa hivyo tunaiomba serikali iangalie vyema masuala haya ya kupanda kwa bei ya mafuta kiholela.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba iwapo hali ya wanawake itadhoofika kutokana na ugumu wa maisha basi familia yote itayumba na kupoteza watoto kukosa malezi bora.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka huu naiomba serikali iendelee na mkakati wa kuimarisha huduma za elimu na afya. Mhe. Spika, tukija kwenye elimu kama bajeti yetu ilivyozungumzia kwamba itasimamia kuhakikisha madarasa yanazidi kujengwa mimi naiomba serikali hili suala ilisimamie ili tuweze kwenda sambamba na bajeti yetu.

Mhe. Spika, tukija kwenye afya ni kwamba kama ilivyozungumza bajeti kuhusu afya yale malengo yake yote yaliyokuwa yamejipangia naomba serikali ihakikishe kuwa imesimamia kama ilivyojipanga kuhusu huduma za jamii kwa wananchi. Pia iweke kipaumbele katika sekta ya miundombinu, kwani sekta hii kama vile umeme ni tatizo katika nchi yetu mpaka hii leo tunapata umeme kwa zamu baadhi ya mitaa. Kwa hivyo, suala hili ni tatizo katika jamii zetu.

Mhe. Spika, kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama, kama Mhe. Waziri alivyokuja kutuambia katika bajeti yetu hii kuwa vitachimbwa visima mimi naiomba serikali isimamie kama ilivyokuwa imeahidi kuhusu jambo hili. Mhe. Spika, nikija katika masuala ya usafiri ni kwamba mimi naomba hizi barabara zetu zihakikishe zinasimamiwa kuwekwa lami ili tuondokane na matatizo haya ya kuwa na barabara zilizokuwa sio nzuri.

Mhe. Spika, vile vile ni muhimu kwa serikali kutilia mkazo kilimo, uvuvi na ufugaji. Juu ya kuwa na hali ndogo ya ardhi lakini kama kutakuwa na mipango mizuri ya kilimo inaweza tukafanikiwa hapa Zanzibar. Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri alipotusomea bajeti hii kuhusu kilimo na mimi naomba kama alivyoahidi jambo hilo naomba isimamie ili tuondokane na tatizo hili na tuweze kupunguza utegemezi wa chakula. Hata hivyo, bado kuna malalamiko ya wakulima kwa madai kwamba bei ya pembejeo ya kilimo kama dawa, mbolea na bei za matrekta ziko juu na hivyo wakulima wengi wanashindwa kufanikiwa katika kilimo.

Mhe. Spika, kuna usemi usemao “ukimuelimisha mwanamke mmoja basi umeelimisha jamii nzima”. Mhe. Spika, usemi huu unajenga hoja ya kuona umuhimu wakutoa kipaumbele cha wanawake katika bajeti hii. Kwa hivyo, mimi naomba nikumbushie ahadi aliyoitoa Mhe. Rais wakati alipozindua Baraza la Wawakilishi mapema mwezi wa Novemba, 2010 kwamba serikali katika juhudi za kuwakomboa na kuwaimarisha kiuchumi wanawake itaanzisha Benki ya Maendeleo ya Wanawake. Hivyo, ni wakati muafaka kwa bajeti hii juu ya utekelezaji wa wazo hilo zuri la Mhe. Rais.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Spika, na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuamka tukiwa katika hali njema kwa mintarafu ya kujadili mambo ya dunia na hasa kwa taifa letu. Mimi sina budi nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wamemsaidia katika upangaji wa bajeti hii.

Pia nichukue nafasi hii nizipongeze wizara zote ambazo kwa kweli zimeingizwa kwa mtiririko wa aina yake.

Mhe. Spika, mimi nitaanza dondoo moja moja, lakini hasa nitakuja kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, kama tunavyoelewa mwenzangu aliyesimama punde tu hapa amesema kuwa ukielimisha mwanamke basi umeelimisha jamii, naomba sana tena sana katika shughuli za akina mama ambazo wanajishughulisha nazo na hasa niende katika mambo ya kilimo na pia nizungumzie mambo ya vikundi ambavyo kina mama wanajituma. Naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika na kwa Mhe. Waziri atupe jicho la huruma ili kutoa taaluma zaidi kwa akina mama hawa kwa jinsi wanavyojitolea kwa miradi yao na kwa kilimo.

Lakini pia nikiunganisha hapo hapo Mhe. Spika, naiomba sana serikali kuhusu habari ya huu ubakaji wa watoto, ningeiomba serikali kama suala lilivyojibiwa leo na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwamba kuna haja ya kukaa pamoja vyombo vinavyohusika, kwa kweli mtoto anapoharibiwa anaharibiwa maisha yake na umri wake.

Naomba sana suala hili litiliwe mkazo hakuna kuchukuliwa dhamana, dhamana isichukuliwe kabisa katika suala lolote, iwe ni mtoto wa kike au wa kiume ilimradi aina ya ubakaji tu Mhe. Spika, imekuwa ni suala sugu kwa Zanzibar hii. Naiomba serikali kupitia vyombo vinavyohusika vikae tena kwa haraka kwa pamoja ili kuhakikisha matokeo haya yanakomeshwa. Samahani kutumia neno hilo, lakini kwa kweli ni suala ambalo linatupa udhaifu mkubwa sana katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la mazingira, nitazungumzia kwa ujumla kuhusu mazingira. Mhe. Spika, sasa hivi tukiangalia Zanzibar kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira na kama hatukuwa aswahi basi tutakuwa tunakaribisha mambo mengi ambayo ni athari kwa kisiwa hiki. Wenzangu walizungumzia hapa asubuhi kwamba hiki ni kisiwa na tunamegwa na bahari kidogo kidogo, lakini na sisi wenyewe wananchi tunajimegea wenyewe yaani hiki kisiwa tunakimega sisi wenyewe. Naishauri serikali kuhusu suala hili la mazingira litilie mkazo ili kuhakikisha suala hili tunalipa kipaumbele.

Lakini sasa nije katika mazingira ya uchafu kwa sababu mazingira kuna ya aina nyingi. Mhe. Spika, niseme kwamba Zanzibar ni kitovu cha utalii nakusudia Mkoa wa Mjini Magharibi na kama ni kitovu kwa utalii tunatakiwa tuhakikishe usafi wa jiji hili la Zanzibar basi upewe kipaumbele ili kuhakikisha unakwenda sambamba na utalii.

Mhe. Spika, jambo la kushangaza, sitamtaja mtu jina nitataja sehemu ambayo inahusika, kwa kweli Manispaa haitimizi wajibu wake, nathubutu kusema Manispaa haitimizi wajibu wake, naiomba serikali na waziri husika, kwa sababu Manispaa ina wafanyakazi wengi sana, lakini huoni linalofanywa na pesa wanazopata Manispaa basi mji wa Zanzibar ungekuwa msafi kabisa.

Naiomba serikali kwa sababu tukifanya mchezo na Mwenyezi Mungu katusaidia mana sisi Waswahili maradhi yakikuganda basi ujue umefanya mambo makubwa, lakini unapokwenda sokoni Mhe. Spika, ukaona hali halisi ilivyo basi hata kile kitunguu hukinunui, lakini Mwenyezi Mungu ametupa mambo ambayo hutukinga katika miili yetu. Kwa hivyo, naomba sana suala hili la Manispaa litupiwe macho.

Mimi nasikitika lazima niseme katika Kamati yangu nimewaita lakini hakuja Mkurugenzi, Meya, hakuna yeyote aliyekuja nikaletewa watu wa chini na mimi nikasema rudini nyinyi siwahitaji. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, suala hili liangaliwe na litupiwe macho mambo ya ubadhirifu wa fedha, fedha nyingi sana zinapotea Manispaa.

Mhe. Spika, nikija katika utalii, wenzangu wamezungumzia kwamba sasa hivi tumeliacha lile zao ambalo limetulea likatujengea mambo sasa tumeingia kwenye utalii, lakini naona na huu utalii wenyewe utatushinda, kama hatukuwa na tahadhari na utalii ambao unakusanya watalii kutoka huko hawapitii pahala popote tukiacha wale watalii ambao tunawaita vishuka.

Kwa kweli serikali inakosa fedha nyingi sana kwa utalii wa namna ile. Naomba kuwe na *One Stop Centre* ya wizara zote husika, naiomba sana serikali hili Mhe. Waziri alifikirie na wakae kwa makini kuwe na *One Stop Centre*, kama kuna uwekezaji wa mambo ya viwanda basi kuwe na *One Stop Centre* ili yule anayekuja kuwekeza asibabaishwe huku na huku, huku akatoa hiki na huku hiki, naomba sana serikali ijipange vizuri sana katika shughuli zetu za utalii.

Nikija kwenye uwezeshaji. Niipongeze sana serikali kwa makusudi kuunda Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwa kweli dhamira ya serikali ni nzuri sana, lakini kama na sisi wenyewe hatukutilia mkazo kwenye suala hili la uwezeshaji na tukaipa kipaumbele wizara hii, najua wizara zote zina kipaumbele, lakini kwa wizara hii tunaweza tukawaondoa

watu wetu katika hali ya umasikini. Naiomba sana serikali pamoja na fedha iliyopewa wizara hii basi pale ambapo itakwama naiomba kwa heshima kubwa pale ikikwama basi serikali iwatilie fedha za dharura.

Nikitoa mifano nije kwenye Mfuko wa JK na AK. Dhamira ya Marais wetu hawa na karibuni kutakuwa na Mfuko wa Mheshimiwa Shein, dhamira ni nzuri, lakini kuna wenzangu wamezungumza hapa kwamba wale walengwa hasa haziwafikii hizi fedha. Kuna watu wanajitia kati kati wanashawishi watu wanakwenda kuzichukua wao fedha zile hawazifanyii miradi iliyokusudiwa.

Jengine la zaidi naiomba serikali riba ni kubwa na sisi tunataka kuwanyanyua wananchi, sasa kama riba kila unapokwenda mwananchi anazungumza kuhusu habari ya riba, basi naiomba serikali kupitia wizara husika kuwa tuzungumze na watu au niiombe serikali kwa nini hivi fedha hazipelekwi wizara husika ya uwezeshaji wananchi? Kwa sababu benki kuna matatizo Mhe. Spika, lazima tuseme ukweli, naiomba serikali kwa makusudi kwamba hivi fedha za AK na JK zipelekwe wizarani watafanya utaratibu ambao ndio utaowawezesha wananchi wetu kupata bila ya kuwa na riba kubwa.

Nije katika suala la ardhi. Mhe. Spika, tukifanya mchezo kilimo tunachokitaja tutashindwa, ardhi sasa hivi inavamiwa na kuvamiwa na kuvamiwa, naiomba serikali ijipange upya ifanye tathmini tuna ardhi ya kiasi gani ambayo tutaweza kujenga viwanda, tuna ardhi ya kiasi gani ambayo tutaweza kulima, tuna ardhi ya kiasi gani ambayo wananchi wetu na wao watapata kujenga vibanda vyao, lakini tukifanya mchezo Mhe. Spika, kwa kweli tutajikuta haya mategemeo tuliyoyapanga kwenye bajeti hayatekelezeki.

Naiomba serikali na naishauri kwamba tufanye tathmini kwa sababu lazima tukubali makosa yametendeka nyuma na tukikubali hivyo tukaweza kujirekebisha Mhe. Spika, basi imani yangu kwamba tunaweza tukafika pahala pale ambapo tumepakusudia.

Mwisho Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi niipongeze serikali vile vile kwa nia safi ya kuunda wizara hii naomba sana na naishauri serikali kwamba, wizara hii nayo ni nyeti na niwashuluru wananchi wa Zanzibar hii ambao wameshajiika kujiunga katika vikundi mbali mbali kuhakikisha wanafanya ushirika wa uvuvi kuchimba mabwawa katika sehemu mbali mbali.

Naiomba serikali kwamba tuangalie vizuri je, hawa watu katika kujiwekea mambo haya yanaweza kuwaletea tija? Kuna taaluma maalum ambayo inatolewa? Nasema nitadondoa kidogo kidogo tu sasa niende kwenye mifugo.

Niwapongeze sana wana vikundi vya ushirika hasa akina mama, wamejikita katika mifugo ya mbuzi wa maziwa. Mhe. Spika, niseme tu kwamba naiomba serikali iwasaidie kwa nguvu zote akina mama hawa kwa sababu hivi wana majumba, wanasomesha watoto wao, mbuzi wa maziwa tu, kwa hivyo naiomba sana serikali itupie jicho la huruma katika vikundi hivi ambavyo vinawajengea uhalali wa kuweza kujipatia maisha yao akina mama hao.

Mwisho naiomba serikali kuu ikae itathmini wizara zote ni yepi ambayo tuliyatekeleza katika kipindi kilichopita na ni yepi ambayo tunataka tuyaimarishe kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, ili tusiongeze utitiri wa mambo ambayo yatatushinda kuyatekeleza. Naiomba sana na ninaishauri serikali ili ifanye hivyo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima, salama na uhai, pamoja na kutuwezesha kuweza kufika hapa leo kuendeleza shughuli muhimu ambazo wananchi wetu wametutuma. Lakini kabla ya hapo nitakuwa mhaba wa shukurani kama nitashindwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye ameweza kutengeneza bajeti nzuri akishirikiana na wafanyakazi wake wote, bajeti ambayo ni tamu na nzuri sana na ambayo inalenga katika kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wao hususan tukiangalia asilimia 61 ya bajeti hii inagusa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sina budi kuchukua fursa hii vile vile kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na viongozi wote ambao tuko madarakani kutokana na juhudi za makusudi anazozichukua kuhakikisha kwamba tunaendelea kupata maendeleo endelevu kwa nchi yetu sote kwa ujumla.

Mhe. Spika, mengi niliyokuwanayo niliyotaka kuyazungumza naona wenzangu wamenitangulia hapa, ndugu yangu Mhe. Omar Ali Shekhe hapa amenipokonya kama kurasa 20 hivi, kwa hivyo mimi nitamalizia hapa palipobakia. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, nianze kwenye ukurasa wa 10 na 11 katika mwenendo wa Sekta ya Kiuchumi kwa kitabu hiki cha bajeti. Serikali imeeleza kwamba, kati ya ukuaji wa sekta ya viwanda imeshuka kwa asilimia 3.4 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 1.9 mwaka 2010. Wataalamu wameeleza kwamba sekta muhimu kuliko zote katika kuleta maendeleo ya nchi zinazoendelea ni zile ambazo zinaelekeza zaidi nguvu zake katika viwanda. Hata hivyo, pamoja na umuhimu

huo wa sekta hiyo ya ukuaji wake kushuka kiasi hicho, bajeti hii haionekani kulipa uzito suala hilo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, hii inatokana na sekta hiyo kutotajwa moja kwa moja katika vipaumbele vya serikali katika bajeti ya mwaka 2011/2012 kama vilivyotajwa vitu vingine katika ukurasa wa 73 wa kitabu cha hotuba ya bajeti yetu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka kulizungumzia ni ukurasa wa tisa ambapo kuna maelekezo ya pato la taifa kwa wananchi. Katika eneo hili kidogo nataka tuzungumze, mimi kila siku huwa nasikia tu ukuaji wa uchumi, pato la wananchi linaongezeka na mambo mengine.

Mhe. Spika, ukiangalia pato la uchumi wa mwananchi wa Zanzibar kwa kweli linahudhunisha sana, hali ya kipato cha mwananchi katika kuendeleza maisha yake ni duni mno. Mwananchi wa Zanzibar anashindwa hata kumiliki mlo mmoja kwa siku, hili ni jambo ambalo linahuzunisha sana. ningelipenda sana Mhe. Waziri kuliangalia suala hili na kuweza kutengeneza utaratibu muwafaka utakaoweza kuwasaidia wananchi wa Zanzibar ili kuweza angalau kuwasaidia katika harakati hizi za kuondokana na umasikini katika nchi yetu.

Pili niingie katika suala la ukusanyaji wa mapato. Katika ukurasa wa 46 na 47 pamoja na mapato kuongezeka lakini kuna malalamiko mengi ya kuvuja kwa mapato ya nchi kwa maeneo.

Mhe. Spika: Mhe. Mahmoud Mohammed ukisikia makofi sio kusifiwa kutupu isipokuwa unavunja kanuni. Hutegemewi usome, chukua dondoo uielezee kanuni inakataa kusoma moja kwa moja isipokuwa labda uwe unanukuu. Endelea.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, kwa kuongezea, umenipoteza katika mudi Mhe. Spika. katika ukurasa wa aya ya 121 vile vile nimeangalia kwa makini kabisa tatizo linalowakabili vijana pamoja na ndugu zetu hususan katika suala la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya kwa kweli ni tatizo kwa watoto wetu ambao wanakaa katika maeneo yetu. Katika eneo letu la Jimbo la Kikwajuni hususan katika maeneo ya Miembeni na sehemu nyengine vijana wetu wameathirika sana na madawa ya kulevya, na katika uchambuzi ambao nimeufanya kwenye kitabu hiki cha bajeti sijaona eneo linalozungumzia suala la madawa ya kulevya, tungeliomba sana waziri atapokuja kutoa majumuisho kuhusu suala la madawa ya kulevya aje na mipango endelevu ambayo itaweza kuwasaidia ndugu zetu watokane na janga hili la madawa ya kulevya. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono bajeti hii.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nitangulize shukurani zangu za dhati kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kutia baraka zangu. Kwa sababu mengi ambayo nilipanga kuyasema tayari waheshimiwa waliotangulia wameshayasema, lakini kutokana na umuhimu wake basi si vibaya na mimi nikashindilia msumari hapo hapo.

Mhe. Spika, pia napenda nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi kubwa sana waliyoifanya katika kututayarishia bajeti hii ambayo ndani yake ina mambo mawili, kuna matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Mhe. Spika, juzi tulipata mafunzo na aliyeyatoa ni Mhe. Waziri, lengo ni kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuiangalia Bajeti ya Serikali, sasa kupitia mafunzo yale mimi nimeangalia taswira nzima ya bajeti na taswira ya bajeti hii unaiona katika ukurasa wa 79 Mhe. Spika, wa kitabu cha Mhe. Waziri, ukisoma ukurasa ule kwenye jadweli mambo yote yako pale.

Sasa kwa kadiri nilivyoangalia Mhe. Spika, nimeangalia maeneo mawili ambayo kila moja lina a na b. kwanza niliangalia taswira ya mapato ya serikali, ambapo ni kupitia mapato hayo ndio sasa serikali inaweza kupanga matumizi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri mapato ya serikali ni shilingi 221.24 bilioni ambayo hayo shilingi 210 bilioni ni kutokana na kodi na shilingi 11 bilioni ni tozo nyengine. Lakini kwa upande wa pili kuna mapato ya nje ambayo tumeambiwa ni shilingi 340.96 bilioni, hayo nayo yamegawika tena, kuna ruzuku shilingi 124.95 bilioni na mikopo shilingi 216 bilioni.

Mhe. Spika, ukienda upande wa pili kuna matumizi sasa, matumizi yamegawika sehemu mbili, kuna matumizi ya kawaida ambayo ni shilingi 234.18 bilioni na kuna matumizi ya kazi za maendeleo ni shilingi 378 bilioni. Sasa Mhe. Spika, mapato ya serikali ni shilingi 221 bilioni lakini matumizi ya kawaida peke yake ni shilingi 234 bilioni, ukifanya hesabu hapo utapata picha kwamba haya makusanyo ya serikali yote hayakidhi mahitaji ya serikali yale matumizi ya kawaida, hapo hujaenda kwenye matumizi ya maendeleo. Sasa sura hii kwa tafsisi yangu mimi Mhe. Spika, nisiyekuwa mtaalamu lakini nasema ni sura ambayo hairidhishi kabisa.

Kepteni kule alisema utegemezi maana yake ni kujitegemea mwenyewe, lakini mimi tafsiri yangu hii bajeti ni tegemezi tena kwa asilimia kubwa. Tumepanga mipango mingi na miradi mingi ya maendeleo. Ukisoma hiki kitabu cha mwelekeo wa hali ya uchumi kuna mipango mingi na ukisoma kwa kweli unapata moyo sana, lakini kumbe mipango yetu imetawaliwa na *risk* kwa asilimia karibu 50. Sasa tukishafika hapa Mhe. Spika, lazima niungane na wenzangu waliotangulia kuwa hali yetu ni mbaya sana na tunahitaji kujitutumua tuondoke hapa.

Mhe. Spika, hali hii inajitokeza miaka mingi huko nyuma tunakuwa na nakisi nyingi kila mwaka tunapanga bajeti. Mimi nadhani nchi yetu inakuwa wataalamu wetu sasa hivi wanakuwa. Juzi mimi nilifurahi sana pale kwenye mafunzo kwani mtaalamu wetu mmoja aliyekuwa akifanya uchambuzi wa bajeti kwa kweli ni *access.* Kwa hivyo, mimi siwezi kumwambia Waziri afanye hivi kwa sababu si mtaalam wa uchumi. Sasa wataalam anao nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla wakae watafute namna ya kujinasua lakini hali hii hairidhishi hata kidogo wala haileti matumaini. Ukisoma kitabu utaona uchumi umekua kwa asilimia ngapi, sijui pato limekua hivi, lakini kwa kweli ni nambari kiuhalisia.

Mhe. Spika, ushauri wangu wa kwanza Mhe. Waziri akae na wataalam watafute namna ya kujinasua, wala mimi sisemi lazima aongeze kodi kwa sababu hivi sasa kuna vilio vikubwa sana vya kodi. Wanasema kuna utitiri wa kodi, sasa kama kuna utitiri wa kodi maana yake ni kusema suluhisho ni kuongeza kodi nyengine sasa unazidisha lile tatizo la watu kukwepa kodi. Mhe. Spika, mimi sisemi kwamba lazima waziri aongeze kodi lakini kwa kweli akae na wataalam wake watafute namna ya kujinasua.

Mhe. Spika, ushauri wangu mwengine kama wengi walivyosema sasa kuna ulazima wa kutumia rasilimali zetu tulizonazo. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu katujaalia tuko hapa Zanzibar, Mwenyezi Mungu mwenyewe ndie aliyetupangia ratiba ya maisha yetu katika visiwa hivi katuwekea rasilimali tuzitumie. Wakati umeshafika sasa wa kutumia rasilimali zetu.

Mhe. Spika, kama Mwenyezi Mungu atatupa taufiki ya kuchimba mafuta katika nchi hii tuchimbe na gesi yetu tuliyonayo hapa, mimi nafikiri tutakuwa tumetatua matatizo yetu kwa karibu asilimia 90.

Mhe. Spika, niungane na wenzangu kwamba sasa hivi kwa kweli hakuna sababu ya kusubiri subiri. Wenzetu walipokuwa wakichimba gesi yao walijua kwamba gesi ni jambo la Muungano lakini hawajatushauri wala hawatupi ripoti zozote za gesi yao na wamechimba gesi na wanatumia. Kwa hivyo, sisi tuwe watu wa aina gani maana yake kwanza mpaka tupate ruhusa. Gesi yetu, mafuta yetu.

Mhe. Spika, hii nyimbo tumeshaimba siku nyingi na tumeshaamua mimi sidhani kama kuna sababu ya kukaa tena tukisubiri suala litoke kwenye kero za Muungano. Kwanza hili halikuwa kwenye kero sijui kwa nini likawekwa huko. Suala hili tulilijadili katika Baraza tukaliamua, hivi sasa sina hakika lakini nasikia limepelekwa kwenye kero kwa hivyo tunasubiri watu waamue kero zao. Mhe. Spika, hii si sahihi kabisa.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na serikali awe *firm* kabisa kabisa. Tuendelee na *process* zetu za kushughulikia mafuta yetu na tukifika pahala kwa kweli tuyachimbe wenzetu wakitaka kuyatoa sawa hawakutaka kuyatoa sisi tunachimba na wao si wanachimba gesi. Mhe. Spika, hilo halitaki mjadala nafikiri Mhe. Omar Ali Shehe kalizungumza kwa nguvu sana na mimi naunga mkono sana.

Mhe. Spika, mimi baada ya kuona sura hii ya bajeti kwa kweli nilivunjika moyo sana na nikasema kweli hata nikiamua kujituma kusoma sana hivi vitabu miradi ile ya kisekta nitakuwa sipati matumaini. Kwa sababu mipango mingi inapangwa lakini pesa hatuna tunategemea pesa ya mjomba, mjomba akikataa hakuna litakalokuwa hapa. Mhe. Spika, nafikiri ushauri nimetoa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo labda nilisema niliguse kidogo kuna *cluster* ya uimarishaji wa huduma za jamii na katika hili siwezi kuzungumza kwa sababu kila *cluster* ina mambo mengi sana ya kufanya ukisoma kwenye kitabu. Lakini nataka nigusie jambo moja tu ambalo nililiona kidogo lina tatizo.

Mhe. Spika, miongoni mwa wadau wakuu wanaotoa huduma za jamii ni pamoja na Baraza la Manispaa. Huduma za Baraza la Manispaa ni muhimu sana sambamba hivyo hivyo na Mabaraza ya Miji yale yaliyoko kule Pemba. Kwa sababu yapo katika macho ya watu kwa hivyo huduma zao pale ndio zinazoleta sura ya nchi ilivyo.

Sasa nimeona kuna miradi hii, kuna mpango wa kuimarisha huduma mijini na kuna dola za Kimarekani zaidi ya milioni thalathini zimetengwa. Lakini kilichonitia mashaka kidogo ni uwiano Mhe. Spika, yaani manispaa ya mji wa Zanzibar imetengewa dola za Kimarekani milioni 31.2 lakini miji mitatu yote ya Pemba imetengewa dola za Kimarekani milioni 3. Sasa hii kidogo inaleta sura si nzuri na tumo katika kujenga mustakbali mwema na kwa kweli miji yetu ya Chake-Chake, Mkoani na Wete iko nyuma sana kimaendeleo, kuna mambo mengi yanahitaji kufanywa. Sijui Mhe. Waziri hapa aliangalia kigezo gani hata akafanya mgao huu. Nadhani kuna haja ya kufanya marekebisho kidogo.

Mhe. Spika, nikiacha hilo labda niende kidogo kwenye sekta ya usafirishaji. Mhe. Spika, usafirishaji ni kitu muhimu sana kwa sababu ni miongoni mwa miundo mbinu inayokuza uchumi, uwe usafirishaji wa anga, uwe wa baharini, uwe wa nchi kavu alimradi ni nyenzo moja muhimu sana ya kukuzia uchumi.

Mhe. Spika, kuna miradi ya barabara kule kusini Pemba kuna barabara karibu 5 kule zinajengwa. Sasa katika hili nina mambo mawili ya kusema. Kwanza Mhe. Spika, ile taaluma inayotumika katika kujenga barabara zile teknolojia ile sijui kama itatuletea faida sana. Mhe. Spika, wananchi wa maeneo yale wana kero

hii ya barabara kwa karibu miaka 40 sasa. Leo tumepata mpango wa kujenga barabara lakini hakuna matumaini kama barabara zile zitadumu hata kwa miaka mitatu mimi sina tamaa hiyo na tumesema sana barabara zile hazina viwango.

Mhe. Spika, juzi nilikwenda barabara ile ya Mwera inayokwenda Dunga sijui ndio huko huko. Ile barabara nilikwenda kuiona katika *stage* inayoitwa fusi sasa hivi, sasa mimi nikapita na gari yangu pale nakanyaga fusi lililokwishawekwa. Lakini upande wa pili wa ile barabara kuna fusi jengine linawekwa juu yake kwa kukisia ni kama wastani wa mita moja, ile *fitness* ya lile fusi karibu mita nzima limetandikwa pale na huku chini sijui kumeshawekwa tabaka ngapi. Lakini unaweza kuona kama ile barabara inajengwa katika kiwango kizuri na ni barabara ya kudumu utasema hivyo.

Lakini Mhe. Spika, barabara zile kule Pemba na tumeshasema sana kwamba ile *fitness* ya lile fusi linalowekwa halifiki hata sentimita 20 wanatandika kama wanaotandika chapati tena ndani ya tope. Unatarajia barabara hiyo *life span* yake itakuwa muda gani. Kule Wambaa walitia fusi wanajitayarisha kutia lami wakapita na gari lile fusi likenda chini tope zikaja juu.

Sasa Mhe. Spika, wananchi wanapiga kelele wanatwambia bwana tunadanganywa hapa. Nakumbuka mara moja tuliwahi kumwita Mhe. Waziri tukamueleza ile hali na kwa kweli lazima tumshukuru alichukua hatua kwa kiasi fulani akenda akakaa na wataalam wake wakatafuta namna ya kusuluhisha. Lakini inaonekana kuna mtu mkorofi, kuna injinia nilitajiwa jina sijui anaitwa nani, ningekuwa nalikumbuka lile jina ningemtaja hapa mtu wa Kenya huyu. Mhe. Spika, huyu mtu ni mkorofi barabara zile fusi anatia jembamba sana hata mimi nisiyekuwa mtaalam najua kama fusi linalotiwa ni jembamba kweli kweli.

Mhe. Spika, hata ule upana wa barabara tulisikia zile barabara zinajengwa mita 5 upana wake, mita 5 bado ni nyembamba sana lakini tukasema haya, ndio haya yaliyomo katika makubaliano ya ujenzi wa zile barabara. Leo injinia huyu anapunguza anajenga mita 4.

Mhe. Spika, hivi sasa wanaendelea na barabara ya Tundauwa kule juzi nilipigiwa simu kapunguza kang'oa zile alama kuna vijiti wanachomeka mle, kaving'oa kavipunguza kwa karibu mita nzima. Wale wafanyakazi wanaotawanya lile fusi wakitawanya nene kidogo anawaambia nakukata posho kwa sababu wanajenga jingi. Hivi kweli Mhe. Spika, huyu mtu sisi anatufaa. Ikipita gari moja hakuna gari nyengine inayoweza kupishana na ile gari maana yake.

Sasa hali ile Mhe. Spika, si nzuri na kwa kweli nilipokuja hapa nilikuja na *speed* ya kumtafuta Mhe. Waziri nimwambie kwamba watu wa Tundauwa wanasema ile barabara hawaitaki kabisa kabisa maana ni kudanganywa. Mhe. Spika, nasema hapa Mhe. Waziri yupo na hii ni miradi ya serikali, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri achukue juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba yale mambo kule hayaendelei kuchafuka.

Lakini la pili katika hilo, moja katika zile barabara 5 ni barabara ya Chanjaani/Pujini. Kwa bahati nilisoma katika hichi kitabu Mhe. Waziri kaitaja humu kwamba ni miongoni mwa barabara ambazo zitajengwa katika ule mradi.

Lakini hivi juzi nilipokuwa Pemba wafanyakazi wa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu walininong'oneza wakanambia bwana barabara ya Chanjaani/Pujini imeshakatwa haijengwi tena. Sina *information official* lakini hilo suala nimenong'onezwa. Sasa Mhe. Waziri atwambie hilo suala ni kweli barabara ile imeshakatwa haijengwi tena, kama haijengwi tena fungu la fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara ile zitakwenda wapi.

Mhe. Spika, leo tuseme kwa sababu Mhe. Waziri ameshataja kama miongoni mwa barabara ambazo zinashughulikiwa ni barabara ya Chanjaani/Pujini, lakini itakapofika mradi ule ukamalizika na barabara ile ikawa haikujengwa na ikawa Mwenyezi Mungu kanipa maisha hivi hivi mpaka bajeti inayofuata, nitakuwa mkorofi sana na nitakuwa na maneno makali ya kusema kwamba Mhe. Waziri kumbe alitudanganya katika bajeti ile. Sasa naomba sana kama kuna wazo la kuifanya ile barabara isije ikakatwa sitokubaliana nalo hilo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hilo muda kama ukiruhusu naomba niseme jambo moja. Mhe. Spika, kuna kero katika kero hizi za Muungano, vyovyote itakavyoitwa kama ni kero, kama ni bughudha, kama ni tatizo.

Lakini Mhe. Spika, jambo hili la kutozwa ushuru mara mbili linakera. Wenzangu wamesema hapa starehe afadhali ihame na mimi naunga mkono.Kuna mtu Mhe. Spika, yeye ni mfanyabiashara analeta magari, pikipiki, juzi alinambia kenda Japan kanunua pikipiki zake kazigawa mafungu mawili. Fungu moja kaliteremsha Dar es Salaam kachajiwa kila pikipiki moja shilingi laki mbili na sitini elfu kama hivi ule ushuru pale, fungu moja kalileta Zanzibar moja kwa moja hilo halikupita Dar es Salaam, likachajiwa kila pikipiki moja shilingi laki mbili nafikiri na hamsini elfu ni wastani huo huo.

Sasa pikipiki alizoziteremsha Dar es Salaam ziliuzwa zikamalizika mara moja, vijana wake wakamwambia hizo ulizozipeleka Zanzibar kama hazijapata wateja zilete huku. Akazisafirisha kutoka Zanzibar kuzipeleka Dar es Salaam na *document* zake zote za *bill of lading* na nyenginezo kazichukua. Kafika pale

bandari ya Dar es Salaam kaonesha kama hizi pikipiki nimeziteremsha Zanzibar na zimeshachajiwa kila kitu, wakamwambia hatukubali na wakamchaji tena kila pikipiki moja shilingi laki mbili na sitini elfu kama walivyochaji zile za mwanzo. Hawakujali kama Unguja kuna *TRA* ile ile imeshafanya kazi yake, kwa hiyo pikipiki moja ikamgharimu karibu shilingi laki tano na kumi elfu zile ambazo zimekuja hapa Zanzibar kwanza.

Sasa Mhe. Spika, ninachotaka kusema huu ni udhalilishaji wa makusudi tunaofanyiwa na *TRA*. Mazungumzo mengi yamepita katika kero hizi nakumbuka Waziri wa Fedha ni Mhe. Mwinyihaji Makame alitwambia kuna vikao tofauti vinafanyika mpaka kwenye makaazi ya mawaziri, mpaka sijui wapi na jambo hili limekwisha, kila mara tulikuwa tunauliza tukaambiwa limekwisha, hiyo imefanyika juzi.

Mhe. Spika, mimi tafsiri yangu ni kwamba kama Mhe. Waziri anakaa na waziri mwenzake wa kule wakishaamua halafu huyo waziri anawaambia watendaji hapana kubadillika fanyeni hivyo hivyo. Maana mtendaji ikiwa kweli mkubwa wake kama waziri kaamua jambo hawezi kufanya vyengine si atafukuzwa kazi. Lakini kwa nini waendelee kufanya, maana yake msimamo ni huo huo. Sasa Mhe. Spika, kama hivi ndivyo sisi tuliomo humu ni wawakilishi wa Wazanzibari wote, sekta ya biashara kwa visiwa vyetu ni muhimu sana. Ukisikia watu wanakwepa kulipa kodi ni kupitia misingi hii, mtu anabinywa mpaka inakuwa ile biashara anayofanya haimsaidii yeye wala mtu mwengine, asiipige chenga kodi kwa sababu gani.

Halafu hapa *ZRB* ipo ni chombo cha bodi. Sasa mimi nataka niungane na wale waliosema *TRA* hapa Zanzibar Mhe. Spika, hatuitaki tena, ihame hapa kama ilivyohama *SUMATRA*. Hii nyimbo Mhe. Spika, tutaiimba sana mpaka hili lifanyike kwa sababu inaonekana wenzetu hawana kheri na sisi. Kila jambo wanalolifanya kuwa ni la Muungano kumbe madhumuni yake ni kuhakikisha kwamba Zanzibar haiendi mbele na hili hatukubali kwa hivyo *TRA* hapa ihame.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie jambo la mwisho dogo tu katika kushughulikia ule mradi wa kuua wale nzi dume wanaoshambulia matunda. Nakumbuka mwaka jana serikali iliufanyia kazi ule mradi na wakaleta mitego mingi katika baadhi ya wilaya. Kwa kiasi fulani mle ambamo iliwekwa ile mitego wale wadudu waharibifu wa maembe na si maembe tu sasa hivi mpaka mapera, mafenesi kila kitu wanaingia wakawa wamepungua kwa kiwango fulani. Lakini hivi sasa ule mradi Mhe. Spika, mimi nadhani serikali ilipoteza pesa bure kwa sababu katika yale maeneo ambayo waliweka wale wadudu wamerudi kwa kasi tena kuliko ile ya kwanza, matokeo yake embe zetu tulizokuwa tunazipeleka nchi za Arabuni tukapata soko hazitakiwi tena. Wao hawazitaki na sisi kuzila hatuwezi maana haziliki.

Mhe. Spika, nitoe ushauri hapa kufanya utafiti kwanza ni kitu muhimu sana, tukitaka kufanya jambo kama lile ambalo linagharimu pesa nyingi za serikali kwanza tufanye utafiti tuone *impact* ambayo tutaipata tukifanya lile jambo. Tulifanya maeneo fulani maeneo fulani hatukufanya, kumbe wale waliobakia sasa walienea na huku ambako tayari tumeshafanya kwa hivyo sawa sawa na sifuri. Sasa Mhe. Waziri katika kitabu chake kimoja nimeona kataja humu. Nilikuwa nashauri kama pesa zilizopo hazitoshi kutolea mitego ile kwa nchi nzima ni afadhali tusifanye tutakuwa tunapoteza pesa bure. Tukifanya tuhakikishe kama nchi nzima inaenea ile mitego wakiondoka wale nzi iwe hakuna sehemu ambayo imebakia.

Mhe. Spika, nafikiri haya niliyosema yanaweza kuwa yanatosha kwa leo. Mhe. Spika, niungane na wenzangu kuunga mkono bajeti hii, pia ushauri ambao nilimpa Mhe. Waziri autilie maanani. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata fursa hii ya kuchangia bajeti hii ya serikali. Mhe. Spika, kwanza kabisa nishukuru Mhe. Waziri kutuletea bajeti hii ambayo kwa mtazamo mzima ina mwelekeo ambapo kama yatatekelezwa yale yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, Zanzibar sasa imefika wakati wa kufika hatua ya maendeleo kwa sababu ina utulivu wa kutosha, hatuna mgogoro wa kisiasa, wananchi wote tunafanya kazi pamoja, hakuna sababu ya kutofikia maendeleo.

Mhe. Spika, nitaanza na mwenendo wa bei kifungu cha 19 ukurasa wa 13 maelezo yanayoonesha namna ambavyo kasi ya mfumko wa bei ilivyoshuka mwaka 2009/2010. Lakini jambo hili limeonesha kama ndani yake halina ukweli wa kutosha. Kwa sababu ukiangalia mfumko wa bei hasa ukifanya marejeo ya hapa nchini basi siku hadi siku vitu vinapanda bei. Ukiangalia vitu muhimu vinavyopendwa na wananchi wengi hapa Zanzibar kama mchele, unga na sukari vinapanda bei ambayo huwavunja moyo wananchi wetu.

Mhe. Spika, sasa hivi tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo wananchi wetu wanaamini kwa dhati tutafikia hatua. Lakini kama alivyozungumza mwenzangu pale kama mlo wa mara moja mtu huumiliki, ukiangalia vitu vyote hakuna kitu hata kimoja chenye unafuu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atueleze katika bajeti hii wananchi wawe na matumaini gani ili kufikia maendeleo na kupata lishe iliyo bora kama ilivyoainishwa kwenye muhtasari huu.

Mhe. Spika, kwenye uvuvi nashukuru kifungu cha 41 ukurasa wa 26 kwanza nipongeze kwa kutambua na kubainisha kama mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa limechangia vizuri pamoja na mtu mmoja mmoja.

Mhe. Spika, vile vile nitoe pongezi kwa waziri kutoa leseni 16 za uvuvi wa bahari kuu hii ni hatua muhimu. Kama ni hatua muhimu lakini pia napata mashaka kidogo katika leseni zilizotolewa hakuna hata mmoja aliyefaidika katika nchi yetu. Hii ni kwa sababu wavuvi wetu hawana zana za kisasa na hapa tumeambiwa kama kutakuwa na posho. Kwa kweli Mhe. Spika, nchi yetu ni ya kisiwa kilichozungukwa na bahari na tuna wavuvi wengi tena walio mahodari lakini kwa bahati mbaya hatujawawezesha wavuvi kama inavyotakiwa. Kama tutawawezesha wavuvi basi sekta hii binafsi ya uvuvi inasaidia sana serikali kwa sababu inawaajiri watu wengi binafsi.

Mhe. Spika, nazungumza hili kama mvuvi na mimi, basi boti moja kwa mfano kule kisiwani Kojani inawaajiri kama wavuvi 50. Sasa boti kama hizo zikiwa 40 zitaajiri watu wangapi. Kwa hivyo, jambo hili pamoja na kwamba kimepewa kipaumbele kilimo lakini na hili liangaliwe kwa kina kabisa.

Mhe. Spika, kama kweli tutajipanga vizuri katika sekta hii ya uvuvi basi wananchi wetu watafikia maendeleo. Japo hatutakuwa na uwezo wa kupeleka nchi za nje huko lakini kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara soko la kimataifa liko pale sokoni feri tunaweza kupeleka samaki na tukapata tija iliyo nzuri kwa wavuvi wetu.

Mhe. Spika, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kifungu cha 42 mpaka 44 ukurasa wa 26 hadi 28 kama ilivyoelezwa kulikuwa na mfuko wa JK na AK lakini mfuko huu haukutumika vizuri kwa walengwa. Hii ilikuwa umimi au *graft* iliyojaa, lakini kama zingetumika vizuri basi tungepiga hatua nzuri kwa wananchi wetu. Wananchi wetu wamejipanga wana vikundi vya kufanya biashara na kuwezesha lakini hapa haikufikia malengo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri na hili ajipange vizuri sana likitokea hilo fungu liende vizuri na liwafikie walengwa isiwe linaishia mikononi kwa wengine.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kilimo ambacho kimetajwa hapa kimepewa kipaumbele. Sasa kama kimepewa kipaumbele lazima kuwe na wataalam ambao wanawawezesha wananchi kielimu kwa sababu ardhi yetu ni ndogo na inatumika kwa mambo mengi, inatumika kwa kilimo, inatumika kwa kujenga na mambo mengine kadhaa. Lakini tuwaige wenzetu wa Tanzania Bara mabwanashamba wetu wasiwe wamelala maofisini tu wawapitie wananchi na kuangalia nini hatua za kuchukuliwa ili kufikia hayo malengo ya kupata chakula.

Mhe. Spika, sasa hivi kama mabwanashamba wetu hawajaleta ripoti basi kuna mpunga ile mbegu nimeisahau kidogo, lakini ukiiangalia mbegu ile sasa hivi ukiuona ule mpunga utauona umeiva, kumbe ndio umeshaharibika wote,

utasema tayari kwa kuvuna kumbe wote umeharibika sijui kama hilo linaeleweka. Mhe. Waziri na hili uliweke bayana kama mabwana shamba au wafanyakazi waweze kupiga hatua ya kilimo, bila hivyo kila siku tutapanga lakini hatufiki kwenye maendeleo.

Vile vile Mhe. Spika, lazima watu wenye kufikia maendeleo lazima wawe na malengo na wakishakuwa na malengo wajitume kwa bidii, bila kujituma hatuwezi kufikia maendeleo. Mhe. Spika, mchango wangu ulikuwa mfupi tu, nasema ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti yetu hii. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nadhani kwa leo nitakuwa ndio kitinda mimba kwa leo.

Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti hii kwa umahiri aliouonesha katika kuwasilisha bajeti hii. Hii ni ishara nzuri kabisa ya kuonesha nia njema ya utekelezaji ya ilani ya chama cha Mapinduzi katika bajeti hii.

Baada ya kusema hayo nianze kuchangia kwa kuipongeza serikali kwa kutokupandisha kodi. Naipongeza serikali sana kwa kutokupandisha kodi yoyote, kwa sababu kumekuwa na mazoea kodi ikipanda kidogo tu kwa sababu basi mfumko wa bei nao unakuwa mkubwa sana na wananchi wanapata matatizo. Kwa kweli niishukuru sana serikali kwa kuangalia na kuliona hili kwamba isipandishe kodi na ijikite katika kuweka mkazo wa kuweza kukusanya mapato zaidi, ili iweze kukidhi haja yake ya matumizi pasi na kupandisha kodi. Hii kwa kweli itatusaidia sana kwa wananchi wetu waweze kuendelea kujipatia hicho hicho kidogo wanachokipata, maana hakuna kinachopatikana.

Mhe. Spika, mimi nitatembelea kwenye maeneo kama manne au matano hivi. Nianze kwenye hili eneo la uchumi wa kikanda. Eneo hili mimi nafikiria sisi kama Zanzibar sijui tumejipanga vipi, labda Mhe. Waziri atakapokuja atatueleza tumejipanga vipi kwa sababu kuna *East Africa Community* pale inakuja, je sisi kama Zanzibar tumejipanga vipi katika hili. Maana wenzetu wanaingia hapa wakiwa wamejiandaa kweli kweli, lakini sijui sisi maandalizi yetu yakoje, hasa kwenye suala zima la mambo ya utalii haya.

Mhe. Spika, zamani tukipata wageni wanakuja wanakagua, lakini tunapoingia kwenye kanda hii kwa kweli *competition* itakuwa kubwa kweli kwa wale wawekezaji. Tunapata wawekezaji lakini tunapoingia kwenye *competition* mimi nina wasi wasi wawekezaji wetu wengi wale wazito wazito

hunyang'anywa tukabakia na wawekezaji vishuka, matokeo yake badala ya uchumi wetu kukuwa ukawa unadidimia, matokeo yake badala ya uchumi wetu kukua ukawa unadidimia. Mimi nafikiria hili Mhe. Waziri aje atueleze vizuri namna gani serikali ilivyojiandaa katika eneo hili.

Mhe. Spika, nije kwenye pato la taifa. Sehemu hii mimi nilikuwa nataka kutoa rai tu kwenye hili Mhe. Waziri atusaidie kidogo wananchi wetu kwenye kuelewa hili kidogo wagumu hawajafahamu. Kwa hivyo, ningeiomba wizara yake isaidie kuelimisha wananchi ili waelewe lile pato la taifa yaani ile *GDP* yenyewe waielewe. Sisi tulipata darasa kidogo, lakini wananchi wetu hawana uelewa wa hilo. Unapowaambia uchumi unakua hawakufahamu kwa sababu mfukono hakuna kitu hilo ni tatizo.

Mtu wa Mkwajuni ukimwambia hivyo kuwa uchumi unakua, anakuambia unakua kwako tu kwangu mimi haukuwi maana yake hata pesa ya samaki sina. Kwa hivyo, nafikiria ningemuomba Mhe. Waziri akatusaidia hili na ikiwezekana hata kutolewe elimu kwa wananchi ili waweze kujua ule utaratibu wa *GDP* unakuaje.

Baada ya hapo nisogee mbele kidogo kwenye vipaumbele vya bajeti. Bajeti hii imesogeza kwenye mambo ya maji, elimu na afya. Naona sehemu hizi ndio Mhe. Waziri alikosogea zaidi. Mimi nilikuwa naangalia kukusanya vitu vingi kwa pamoja na ukiliangalia lile pato la uchumi la taifa, nahisi hatutofika mahala tukaweza kutekeleza yote haya na hili linakuwa ni tatizo. Mambo kama haya sisi huko majimboni tunayapata.

Kwa mfano kama mimi kwenye Jimbo langu la Mkwajuni katika kipindi kilichopita kulikuwa kuna pesa zile za tunaziita pesa za Mbunge. Pesa zile zilipoletwa zilikwenda kwenye ya Halmashauri kule kwetu, zilipofika kule ikawa usimamizi wa pesa zile ukawa kwa masheha, kwa hivyo kila sheha akataka shehia yake ndio ijenge labda skuli na vitu vyengine, lakini ukitizama ule mgao wa zile pesa unakuwa ni mdogo.

Matokeo yake kila shehia kama iliamua kujenga skuli ya chekechea basi utakuta imepata msingi au na kozi nne tu badala ya kumaliza. Lakini kama ingekuwa wamekaa pamoja na wakaelekeza kwenye mradi mmoja au miwili basi pesa zile zingeweza kutosha kumaliza ile miradi miwili halafu na mwaka unaofuata wakatafuta miradi mingine kumalizia.

Kwa hivyo, mimi nataka kuishauri serikali iangalie imeweka vipaumbele hivi, lakini ukilitizama na lile pato utakuta kama haliwiani na kuweza kukidhi haya ya kukamilisha miradi hii yote ambayo wanasema itafanyika. Kwa hivyo, nilikuwa nashauri hapa ni vyema tukaelekeza nguvu zetu labda kwenye miradi

miwili, mitatu au minne kwa mujibu wa zile nguvu zetu tulizonazo, tukajikita pale ili tuweze kuikamilisha mwakani tuanze na mingine. Lakini kama hatukufanya hivyo Mhe. Spika, tunaweza tukajikuta kila mwaka tunaendeleza miradi ile lakini ukamilisho wake unakuwa uko mbali sana.

Nije kwenye suala la kilimo. Mhe. Spika, suala la kilimo hapa naona limezungumziwa sana kwenye mpunga au mchele. Suala hili mimi nahisi serikali kwenye suala la kilimo hasa hiki cha mpunga sisi tumejikita kwa kiasi kwamba mkulima aweze kulima na kupata chakula chake, lakini kwenye suala la kwamba aweze kulima na kupata ziada ya kuuza, mimi naona kama kidogo tuko nyuma.

Ninashauri serikali tujielekeze kwenye kilimo cha biashara, wakulima walime mpunga lakini waelekeze na kwenye kilimo cha biashara, hasa kwenye masuala ya maua na viungo vile. Sisi kule kwetu Mkwajuni tunalima manjano au bizari, basi wangewashajihisha wakulima wetu hawa wakawa wanaweza kulima kwa wingi wakaweza kuuza zao lile, kwa sababu wanalima lakini kilimo chao wanamalizia ile ile mtu kikataa chake chini ya nyumba kalmia anapata kwenda kuuza kidogo imekwisha hadithi. Ule uwezo wa kulima zaidi na kuweza kuuza haupo.

Kwa hivyo, na hiki kilimo cha mpunga nacho ukikitizama utaona hawa wakulima wanaelekezwa katika kulima na kujitosheleza angalau wapate wao kwa chakula tu, lakini ile ziada ya kulima kama wanavyolima wenzetu sijaiona. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atusaidie ili kidogo walime mpunga, lakini na vilimo vyengine vya biashara.

Mhe. Spika, nimetoa mfano hapa kama vilimo vya maua, kwa sababu nimewaona wenzetu kule Arusha wanalima maua kweli kweli na yana bei nzuri kwa wenzetu. Nafikiria na sisi uwezekano wa kulima zao hilo hapa kwetu upo. Kwa hivyo, wizara hapa iwashajihishe wananchi ili waweze kuingai huko, watakapokuwa wanaweza kulima maua basi wanao uwezo wa kupata kiasi na kule mpunga wakawa wanapata chakula na huku wakawa wanapata ili waweze kujisaidia katika mambo mengine.

Mhe. Spika, niingie kwenye suala la rasilimali za serikali. Suala hili kwa kweli Mhe. Spika, ni tatizo kidogo, kwa sababu rasilimali za serikali zinakwenda ovyo. Kuna watu wana hodhi au wanachukua pasi na utaratibu wowote, serikali ipo lakini wachukuaji ndio hao hao, sasa hili ni tatizo. Huku Mhe. Waziri atalalamika sana kuhangaika na vianzo vya mapato na mengineo, lakini kama tutakuwa tunakusanya tunapeleka na matumizi yake yanakuwa sio sahihi basi hatuwezi kufika Mhe. Spika, tutakuwa tunakusanya zinatumbukia kwenye shimo, lakini maendeleo yatakuwa hayaonekani.

Kwa mfano kwenye matumizi na hasa kwenye matumizi na zile rasilimali zenyewe *asset* za serikali zinahaulishwa ovyo bila kufuata taratibu na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio msimamizi mkuu wa hilo, lakini utakuta yeye mwenyewe ukimuuliza baadhi ya mambo atakuambia wizara hii, ukenda wizara ile utaambiwa liko wizara hii hupati lile jawabu sahihi. Kwa hivyo, rasilimali za serikali zinapotea ovyo kabisa, kwa sababu usimamizi wake hauko sahihi.

Mhe. Spika, tukiangalia hapa wizara zote zilitakiwa kufanya *asset register*, lakini ni wizara chache tu ambazo zilifanya hivyo, kujua angalau ile mali yake. Kwa hivyo, serikali yenyewe inaonekana hata zile mali zake kuzijua zenyewe haizifahamu. Kwa sababu kama wizara imeambiwa itengeneze *asset register* hakuna, basi ndio haipo hiyo mali, maana ukimwambia iko wapi mali yako haijui. Kwa hivyo, hilo ni tatizo na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio msimamizi wa hili.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kidogo katika hili wapi amefikia, hizi mali za serikali zinahifadhiwa vipi au wapi zipo. Yaani leo serikali ikitaka kujua mali zake hasa mimi nina hakika haiwezi kupata jawabu, itashindwa kwa sababu itabidi aiulize wizara na wizara haijafanya haya, kwa hivyo ni tatizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye suala la uvuvi. Nakwenda haraka haraka kwa sababu naona unaangalia sana muda. Katika bajeti hii kumezungumziwa suala la uvuvi wa bahari kuu, lakini ukiangalia serikali hapa imejipanga katika ukataji wa leseni kwenye bahari kuu na mambo kama hayo, lakini sijaona ilivyojikita zaidi katika kuwawezesha wananchi wakaweza kwenda kuvua katika hiyo bahari kuu. Wananchi wetu wanavua katika hii bahari ya karibu karibu tu na samaki wameshaanza kukimbia kimbia.

Mhe. Waziri atusaidie ili kidogo wananchi wetu wawezeshwe kwenda kuvua kwenye hiyo babari kuu. Tukiwaachia hawa tunaowapa leseni kwenda kuvua tu peke yao kule, hatukijui wanachovua ni nini, sisi tunawapa leseni ya mwaka wanakwenda kuvua, lakini hatuwezi kuwadhibiti tukaona kile ambacho wanakivua, tutatahamaki ile rasilimali kule baharini imekwisha na huku sisi hatuna kitu, kwa sababu sisi pato letu ni leseni, lakini lile pato lenyewe linalopatikana katika ule uvuvi wenyewe huku serikali haina kitu, kwa sababu wale wakishavua hawarudi kusema kuwa tumevua tani fulani, wanakwenda mpaka muda wao umalizike wanakuja kukata leseni.

Kwa hivyo, nahisi kwa hapa serikali inakosa mapato mengi sana kwa kutokujua kile ambacho kinavuliwa kule bahari kuu. Kwa hivyo, ningeshauri serikali

ikaweka utaratibu mzuri wa kuweza hata kujua kile kinachovuliwa katika bahari kuu ili ikaweza kukusanya mapato yake zaidi.

Mhe. Spika, mimi namalizia kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na bajeti yake hii na niwashukuru watendaji wake kwa kutayarisha bajeti yenye matumaini kwa wananchi.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkwajuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda uliobaki ni mchache hautasaidia kumwita mjumbe mwengine kuchangia. Lakini nichukuwe nafasi hii kuwaombeni Waheshimiwa Wajumbe jambo moja, kuna maneno mazuri sana ambayo yametolewa na Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe kiasi cha kwamba wajumbe wanafurahi, kupongeza na kutilia mkazo kwa kupiga makofi. Lakini makofi yenyewe mengine hayafurahishi ni makubwa mno kiasi cha kwamba nidhamu inaharibika, na pengine sio nidhamu tu hata haya ma-*desk* inawezekana hayatadumu kwa muda mrefu.

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tukipiga makofi kwa kupiga meza zetu ambayo inaruhusika, kwa utaratibu na nidhamu, itaeleweka madhumuni yetu kuwa tunapongeza au kutilia mkazo jambo ambalo mjumbe analizungumza au waziri amelisema.

Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe sana basi tufuate utaratibu huo ili wanapoingia wageni wasione ajabu. Maana kuna wakati fulani nilipata mgeni, aliposhuka kule juu aliniuliza hivi ile ni nini. Nikamwambia na nikasifu kwamba wajumbe wamefurahi mno, lakini kwa kweli yeye aliudhika, na wakati mwengine halisaidii sana kwa sababu anachokisema waziri au wanachokisema mjumbe basi hakisikiki vizuri kwa sababu ya makofi yanayopitiliza nidhamu ya kawaida.

Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe, tupige makofi kwa kupiga meza zetu kwa utaratibu na nidhamu, na yote itakuwa inaeleweka kwamba tunakusudia kupongeza. Waheshimiwa Wajumbe nilitaka nitumie nafasi hii niseme hilo, ili tuweze kwenda vizuri katika shughuli zetu. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. *(Makofi).*

Sawa, kitu kama hicho. Nawashukuru sana na baada ya hapo basi naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 21/06/2011 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 21/06/2011 saa 3:00 asubuhi)